# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KALOLENI CONSTITUENCY, KALOLENI WOMEN'S SOCIAL HALL,

## ON

TUESDAY, APRIL 30, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KALOLENI CONSTITUENCY TUESDAY, APRIL 30, 2002, AT KALOLENI SOCIAL HALL**

**Present:** Com. Ibrahim Lethome Asman
Com. Isaac Lenaola
Com. Hon. Phoebe Asiyo

**Secretariat Staff in Attendance:**

Bw. Joash Aminga - Programme Officer
Bi. Patricia Mwangi - Verbatim Reporter
Bi. Rachel - Rapportuer

Meeting started at 9.50 a.m with Com. Lethome in the Chair. Councillor Charo welcomed participants.

**Com. Lethome**: Kwa kawaida yetu mikutano yetu huanza kwa kutaka baraka za Mwenyezi Mungu. Ningependa Reverend na kuna mzee mmoja wa Kiislam hapa? Kuna ye? Hakuna, basi Reverend tuombe Mwenyezi Mungu tuanze mkutano wetu.

**Reverend**: Tuombe tafadhalini. Mwenyezi Mungu Baba wetu wa mbinguni uliyeumba nchi na mbingu na vyote vilivyomo, kila kitu kimepaswa kukutukuza wewe kwa kuwa wewe ndiwe unaongoza amani tuliyeo nayo. Inatoka kwako. Hekima na busara na elimu ya kimbinguni ni mali yako. Wakati huu ambao umekubali wewe mwenyewe tufike hapa kwa yale tunayotaka tupange, Mungu wetu uwe pamoja nasi. Utusaidie uweze kutuongoza, tuwe na amani katika akili na mioyo yetu, hila ya shetani iwe nje

mahali hapa, kwako pekee yake tupate usalama. Bariki serikali yetu katika utulivu tulionao uendelee. Umbariki Rais wetu, mawaziri wake wote na wote wanaohusika kwa kutawala Kenya na hasa, katika Tume hii. Uiongeze katika hekima na busara yako ya kimbiguni, ili yote watakaotenda yawe yataleta manufaa kwa raia na nchi ya Kenya, na wageni wao na zaidi sana jina lako lipate kutukuzwa mahali hapa tulipo, tuwe tunalindwa na wewe mwenyewe na kubarikiwa. Kwa Yesu Kristo na Mkombozi wetu. Amina.

**Com. Lethome**: Asante sana Reverend. Na kawaida katika mila zetu tukiingia bomani kwa mtu kwanza mpaka lazima mwenyewe akukaribishe. Kuna mama Councillor ambaye ni member kwa sisi na pia ni Councillor hapa tunamuomba atukaribishe ili tusiambiwe tumeingia bila kukaribishwa. Kwa hivyo mama tunakuomba kwa maneno mawili ukaribishe.

**Bi. Priscillar Charo**: Mabibi na Mabwana hamjambo? Hapa kwanza nataka kuwajuisha kamati hii ya katiba hapa kwetu. Bw. Samuel Mbogo ndiye Chairman - simama uwasalimie.

**Bw. Mbogo**: Hamjambo?

**Bi. Charo**: Kuna Rev. Singala. Simama useme jambo baba.

**Rev. Singara**: Hamjambo?

**Bi. Charo**: Kuna Bi Constance Zero.

**Bi. Constance**: Hamjambo

**Bi. Charo**: Na mimi ni Bi. Priscilla Charo, area Councillor, Kaloleni ward. Karibuni nyote,hasa Tume tunaikaribisha karibisho la pekee mno. Jisikieni nyumbani kwa mazugumzo yote. Msijisikie mko na wasiwasi mko ugenini, hapa mko nyumbani. Mjisikie nyumbani kabisa. Mkiwa mna matatizo ya kisiri, twambieni tutawasaidia hata hali ya kujisaidia kwa ajili ya choo, hall hili ni jumba la kina mama na halina vyoo, lakini mtakapo sikia hali hiyo muwe munatunongoneza na tutajua vile tutafanya. Karibuni. ( **clapping**)

**Com. Lethome**: Sasa tunajisikia nyumbani kabisa.Tunajisikia tunafuraha, tutafanya kazi vizuri kabisa. Kama mnavyo jua kikao hiki sio chetu cha kuja kuzungumuza. Hiki ni kikao cha sisi kuja kuwasikia nyinyi watu wa Kaloleni. Tumekuja hapa kuweza kuchukua maoni yenu. Tutakuwa hapa siku nzima na nyinyi na mbele yangu hapa ni nao Macommissioners. Kwa upande wangu wa kulia, Hon. Com. Bi. Phoebe Asiyo, anawakilisha sehemu za Karachuonyo. Kwa upande wa kushoto ninaye Com. Isaac Lenaola. Halafu pia kutoka makao makuu ya Tume tunaye Programme Officer Bwana Aminga, yeye atashugulikia kazi zote za kiidara zinazotajika kufanywa hapa. Kisha tunaye Bi. Patricia Mwangi. Kazi yake ni kunasa sauti za wale wenye

kuzungumza. Kisha tunao wale wengine Bi. Rachel, kazi yake ni kurekodi. Tunaye pia mwingine na kazi yake nikutafsiri lugha kwa wale ambao hawasikii; utatujulisha ili yule Bibi aweze kufanya kazi yake. Yeye anazungumza kwa ishara (interpreter), tuna Esther pale ambaye ni msaidizi wa District Coordinator wetu na pia mfasiri wa lugha ya Kigiriama.

Ikiwa kuna mtu yeyote anayetaka kuongea kwa lugha ya mama, usione haya. Zungumza kwa lugha ya mama itafsiriwa. Tutaipata bila wasiwasi. Kuna Binti wa Kigiriama pale anafahamu lugha vizuri kabisa. Haya asante. Na mimi jina langu ni Com. Ibrahim.

Nitakuwa mwenye kiti wa kikao cha leo na kama nilivyowaambia kikao ni chenu sio chetu na kuna sheria; hata mpira una sheria. Ama hauna sheria? Bila sheria watavunjana miguu, ama sivyo? Kuna mambo ya red card na yellow card na firimbi itapigwa. Kila mmoja atapatiwa nafasi ya kuzungumza. Kama una maandishi (memorandum) tutakupa dakika tano tu ueleze ya muhimu katika hiyo memorandum yako kisha utaikabithi. Kama huna na unataka kuzungumza, tutakupa dakika kumi usimame hapa. Usianze kupa mifano na matatizo, mambo mengi. La. Pendekeza. Napendekeza hivi, napendekeza hivi, Polisi wasivae uniform yale yote unayoyataka. Halafu pia nawaambia hivi, jana niliambia watu Mariakani yale mambo yakusema sijui nitasema nini, hakuna. Zungumza kile unachotaka kuzungumza. Usiwe na uoga wowote. Hata ukiona Polisi wamekuja hapa wamekuja sababu ya kuifadhi amani. Sio kwa sababu ya kusikiza nani anasema nini. Sheria ambazo imebuni tume hili imetupa ruhusa. Imewapa wananchi uhuru wa kuzungumza wanavyotaka. Watoe maoni yao tuweze kupata sheria ya watu wenyewe, maoni ya watu wenyewe. Ile sheria tulitoa kwa mkoloni hatukuweza kushauriwa. Hii tumeshauriwa, ni sheria yetu wenyewe. Kwa hivyo watu wa Kaloleni na mimi husikia watu wa Giriama hawana uoga, sema utakacho bora tu usivunje amani ama sivyo? Tumesikizana? Halafu kuna kitu kingine, hata nyumbani mama hutoa maoni ambayo baba hakufurahia lakini wanaendelea kuishi chini ya paa moja na hawapigani. Kila mmoja anuhuru wa kutoa maoni yake. Kwa hivyo ikiwa mtu atakuja hapa atoe maoni yatakukera, wewe mwachie, ni maoni yake, ama si hivyo? Nafasi yako ukipata njoo nawe utoe yako Bwana. Kwa hivyo tuheshimu maoni ya watu wengine. Tumekubaliana? Sasa hizo ndizo sheria. Referee ni mimi, firibi itapigwa na mchunga-wakati Com. mwenzangu hapa. Sasa bila kupoteza wakati tunaanza moja kwa moja. Tunaanza na Bwana Ngala Kibanzu.

**Ngala Kibanzu**: Asante sana Bwana Commissioner. Kwanza kabisa ningependa majimbo yaliyo na serikali kuu. Uchumi wote uwe mikononi mwa jimbo. Utalii wote uwe mikononi mwa jimbo. Koti iwe mikononi mwa jimbo. Port hiyo Kilindini isiuzwe. Ardhi ya watu walioko ng'ambo iwe mikononi mwa jimbo.

Serikali kuu itapokea 10% kutoka kwa jimbo. Serikali kuu inapopata mkopo huko nje igawanye sawa kila jimbo. Mbunge awe ni mtu wa Form Four, Councillor aliyeko mamlakani aweze kushindana na Councillor mpya aliye Form Four. Polisi waandikwe sawa, na jeshi liandikwe sawa kila jimbo. Asanteni.

**Com. Lethome**: Asante sana (inaudible). Tunakaribisha Mbunge wa sehemu hii Mhesimiwa Bwana Matheas Keah.

Leo ako na sisi na tuko na raha sana. Karibu Mheshimiwa. Haya tuendelee. Stephen Mwandaro. Yuko? Haya Kisau Kenga.

**Kisau Kenga**: Mapendekezo yangu mimi ningetaka Machief na Masub-chief wawe wanapigiwa kura na wananchi wenyewe. Kusiwe na kwamba (inaudible). Wale wazee wa kijiji wawe watakiwa maanani katika kile kijiji chao. Kusiwe na kwamba hawatambuliwi. Watambuliwe kama wananchi wana fanya kazi. Ni hayo sina mengi.

**Joshua Kasuku**: Asante sana Chairman na watu wenzangu wote hapa. Mimi napendekeza majimbo. Serikali kuu ya Kanu iwe inapendekeza majimbo na nataka kampuni zote ama idara zote za serikali wawe wanachukua watu wa sehemu ile ile sio mtu mgeni. Ni hayo tu.

**Com. Lethome**. Sasa hayo majimbo mapendekezo unataka yawe ni ngazi gani? Ngazi ya Wilaya, Mkoa, Location?

**Kasuku**: Kazi ya Wiraya.

**Com. Asiyo**: Sio kwa District (inaudible)

**Kasuku**: Hiyo ngazi itakuwa kwa mkoa.

**Com Lethome**: Kwa mkoa wa Pwani?

**Kasuku**: Ndiyo hivyo.

**Com. Lethome**: Mwadziwe Tinga. Karibu

**Tinga**: Kwa jina mimi ni Mwandziwe Tinga. Ningependelea majimbo. Serikali iwe ya majimbo kwa wilaya mzima ama mkoa mzima kwa jumla. Kusiwe na mapendeleo yoyote ya ukabila lakini iwe ya wilaya nzima.

**Com. Lenaola**: Ungependa kiongozi wa jimbo aitwe nani? Aitwe PC, Governor, President….

**Tinga**: Kiongozi wa jimbo aitwe Rais.

**Com. Asiyo**: Atakuwa na bunge lake la jimbo au katika (inaudible) kama yeye ni Rais?

**Tinga**: Rais yule atakuwa akiongoza lile jimbo lake.

**Com. Lethome:** Kutakuwa na wabunge katikalile jimbo?

**Tinga**: Ikiwezekana kuwe na bunge katika lile jimbo lake.

**Com. Lethome**: Sasa nakuuliza hivi kwa mfano, ikiwa katika jimbo la Pwani kuna mtu ambaye si wa Pwani kwa mfano, Maasai kama mimi au Mluo ako pale ana ardhi yake amenunua pale ameishi pale miaka mingi, ungependekeza mtu kama huyo afanye nini, katika hayo majimbo unapendekeza?

**Tinga**: Mtu kama huyo huwa kawaida anajiandikisha kama mwenyeji wa pale.

**Com. Lethome**: Haya Asante.

**Com. Lenaola**: Umesema ya kwamba jimbo liwe na tourism, liwe na policy, ungependa pia hii region iwe na mambo gani mengine? Ishughulikie nini?

**Ngala Kibanzu**: Kwanza sababu ya kutaka majimbo ni kwamba tangu tujitawale hata National schools kuja, hapa jimbo hatuna. Hatuna hata chuo kikuu (university) moja hakuna katika pwani nzima. Tatu, Utalii College uliyoko hapa pwani na Utalii college unawekwa hapo Nairobi. Tunataka iwe hapa Pwani.
Nne. Madaktari tunajua ni waganga, wanaweza toka pahali popote. Wanakaribishwa, Asante.

**Com. Lenaola**: Na ungependa kuwe na bunge katika jimbo ama kuwe na bunge moja tu nchini?

**Kibanzu**: Nataka jimbo liwe na bunge lake.

**Com. Lenaola**: Ungependa mkuu wa jimbo aitwe nani?

**Kibanzu**: Zamani tulipopendeza katiba hii hapo zamani tulikuwa na President wa jimbo lakini hatujui kama anaweza kuchaguliwa jina lingine. Huyo ni mkuu wa jimbo na anaweza kuwa president wa jimbo hilo na wajumbe wake.

**Com. Lethome**: Kwa sasa namuita Bw. Emmanuel Gona. Karibu.

**Gona**: Ningependa hii serikali iwe ya majimbo.

**Com. Lethome**: Iwe kwa daraja gani?

**Gona**: Katika ngazi ya kwanza.

**Com. Lethome**: Iwe katika wilaya, mkoa au location; jimbo lenyewe litakuwa ni mkoa?

**Gona**: Mkoa wa Pwani.

**Com. Lethome**: Bwana Omar Taka.

**Taka**: Kwa jina ni Omar Taka. Maoni yangu ni kwamba napendelea serikali ya Kenya iwe na vyama vingi lakini zile pesa ambazo zinatoka kupigania ubunge ama siasa, kila mtu atafute pesa zake kibinafsi.

**Com. Asiyo**: Kila chama?

**Taka:** Kila chama. Pili, Machief na Madiwani wawe wa Form 4 lakini wachaguliwe na wananchi. Hiyo ndiyo maoni yangu.

**Com. Lethome**: Jobik Arome.

**Arome**: Kwa jina naitwa Jobik Arome. Mapendekezo yangu ningesema kwamba serikali nataka ya majimbo kwa mkoa. Pili kutaka serikali ya majimbo ni kwamba tunataka ugawanaji wa kazi ama wa kijeshi uwe kila mkoa wanachukuliwa watu sawa kwa sawa. Kama kwa mfano ni watu mia wote wagawanye nusu pahali pengine nusu. Kila jimbo lilete watu sawa, kama ni kumi hivyo. Kwa hivyo kwa akina Kyalo ni kumi, kwa akina Kamau kumi, isipokuwa wote wasionekane Kamau, - hapa Mombasa ni Kamau. Hatupendi hivyo. Hiyo ndiyo chaguo langu.

**Com. Lethome**: (inaudible)

**Arome**: Tuwe tukisoma wenyewe.

**Com. Lenaola**: Kwa percentage gani?

**Arome:** Ya majimbo 50% na serikali 50%.

**Com. Lethome**: Na watu wasiokuwa ni wa kutoka lile jimbo lakini wana riziki, mali, ardhi na mijengo katika jimbo fulani wafanywe nini?

**Arome**: Hao watakuwa kama watu wa hapa kwa sababu mali yao iko hapa na wamezaliwa hapa.

**Com. Asiyo**: Kazi hizo ungependa iwe serikali ya jimbo (inaudible)

**Arome**: Kazi kama ya jeshi, kazi kama ya kampuni, zingine kama Power unaona kwa kawaida utapata, Personnel Manager ni Mluo. Ataenda kwao achukuwe watu kutoka kwao aje awaandike kazi hapa na sisi hapa hatuna kazi. Ningependa serikali ya majimbo isimamie mambo kama haya.

**Com. Lenaola:** Na je Navy utasema nini juu yake?

**Arome**: Navy hata hivyo ina viongozi wengi. Tungelitaka viongozi wawe ni watu wa hapa wenyewe wasimamie wenyewe pengine upande wa Navy awe ni Kyalo upande wa D.O awe ni Garissa upande wa Kiisi awe ni Kaingu …

**Com. Lethome**: Na ungependekeza katika hilo jimbo, je idara ya mkoa tulionao hivi sasa kwanzia Kisii mpaka juu, je wana wajibu gani katika kazi au katika hili jimbo?

**Arome:** Kazi zao watakuwa nikutuzoesha sisi hapa juu wao ni wazaliwa hapa kuliko mtu mwingine.

**Com. Asiyo**: Basi mtawachagua ama watachagua naye?

**Arome**: Tunataka kuwachagua machief. Ni lazima tuwachague sisi wenyewe kwa mlolongo.

**Com. Lethome**: Na kiwango chao cha elimu?

**Arome**: Kiwe ni Form 4.

**Com. Lethome**: Na Sub-Chief?

**Arome**: Form 4.

**Com. Lethome**: Na Councillors?

**Arome**: Vile vile.

**Com. Lethome**: Na MP?

**Arome**: Form 4 kuendelea mbele.

**Com. Lethome**: Asante Bw. Arome. Evans Arome.

**Evans Arome**: Kwa jina mimi najulikana Evans Arome na ningependekeza majimbo. Mkoa wa Pwani unaweza kujisimamia wenyewe. Isiwe pengine ni mtu wa kutoka juu huko bara aje atusimamie si hapa maanake tunaona udhaifu ya kwamba wengi hawana kazi hapa na wako na elimu zao. Kwa hivyo ningependekeza hayo majimbo na mkoa wa Pwani uwe unaweza kujisimamia wenyewe.

Nikirudi upande wa hizi kampuni ziko hapa, ningerudi mpaka port. Pia ningeliomba jimbo hili letu la Pwani liwe linajisimamia lenyewe maanake tuko na wasomi ambao wangeweza kusimamia pale port. Kwa ufupi ni hayo.

**Com. Lenaola**: Ungependa mapato katika jimbo asilimia gani ibaki katika jimbo?

**Arome**: Kwa serikali kuu kwa kila jimbo liwe linaweza kupelekea kama asilimia kumi.

**Com. Asiyo**: Na umeongea juu ya serikali ya majimbo ya kumi hujatueleza bado kama ungependekeza serikali za majimbo ziwe kwa province, mkoa au kwa nchi?

**Arome**: Ningetaka kama hii Coast iwe inaweza kujisimamia yenyewe.

**Com.Lethome**: Na kuhusu elimu katika jimbo?

**Arome**: Kwa mfano kama hao Ma- councillors tuwe tunaanzia Form 4 kuendelea na Machief tutawasimamia mlolongo. Ni lazima wachaguliwe huku. Tunaletewa mtu na hata hatumjui ametoka wapi, mtu mwenyewe pia kuandika hajui.

**Com. Lenaola**: Na masomo gani je?

**Arome**: Kwa Chief pia tunataka Form 4.

**Com. Asiyo**: Je vipi mambo ya elimu, afya na kathaika, ungependekeza kwamba mambo haya yaangaliwe na serikali ya jimbo ama ya juu?

**Arome:** Kwa mfano kwa sababu kila jimbo litakuwa linajisimamia itatakikana pia kuwa serikali kuu iwe inaweza kuangalia kwa sababu tutakuwa tunapeleka kitu kidogo. Itakuwa ni lazima iwangalie lakini jimbo litakuwa linaweza kujisimamia lenyewe.

**Com. Lethome**: Asante Bw. Arome Evans. Sasa naona tusikize akina mama pia. Mariamu Kazungu.

**Mariamu**: Kwa majina naitwa Mariamu Kazungu. Mimi maoni yangu nataka serikali ya majimbo na kila jimbo liwe linajisimamia kwanzia kwa mkoa mpaka wilaya. Na pia kama mama wa Kaloleni ningependa elimu idumishwe zaidi kwa watoto wetu hata kwa wazee pia kwa sababu kuna zile za ngumbaro. Na wakina mama wapewe uwezo sawa na wazee. Kama vile sisi tumeolewa basi saa ingine tuna shida, na mzee akisema watoto ni wangu, ama shamba ni langu, sasa akina mama kama sisi saa ingine huwa tunapata shida, kwa hivyo kama ni mama na pengine ameletewa shida na mzee kama vitu viko pale wagawanye sawa kwa sawa ili naye ajisaidie. Si kwachia mzee peke yake watoto na mali zote. Ni hayo tu. (**Clapping**)

**Com. Lethome**: Kuhuzu elimu umesema watu wote wapewe elimu sawa. Unajua kuna watu wengine wangetaka kupata hiyo elimu lakini hawawezi kujigharamia hawawezi kulipa karo ya shule. Unapendekeza nini?

**Mariamu:** Ningependekeza ya kwamba kama vile majimbo zile watasimamia pia wangalie wale ambao hawajiwezi wawe wata wasaidia nao wapate elimu kwa njia yoyote. Hata kama ni harambee lakini sote tuhakikishe watoto wanapata elimu.

**Com. Lethome:** Gharama ya school fees isimamiwe na nani? Serikali ama wananchi wenyewe?

**Mariamu**: Serikali na wananchi pia

**Com. Lethome:** Kwa hivyo cost sharing?

**Mariamu**: Eeeh.

**Com. Lethome**: Na upande wa health, matibabu unasema nini?

**Mariamu**: Matibabu pia tungeomba izidi kwa sababu bila matibabu hatuwezi kuendelea. Kwa hivyo mahospitali yawe ya kutosha yaende hata kama ni kila kijiji ili tuwe tutapata usalama zaidi.

**Com. Lenaola**: Na gharama ya matibabu?

**Mariamu**: Wananchi wajisimamie pamoja na serikali.

**Com. Lethome**: Ujumbe kama huu ni kuhusu wakina mama na utawala?

**Mariamu**: Wakina mama pia ningetaka tuwe mstari wa mbele akina baba wawe wako mbele na pia wakina mama wawe wako mbele. Pia na sisi tuangaliwe vizuri.

**Com: Asiyo**: Na nani?

**Mariamu**: Na serikali kama vile kuna viti vya bunge basi kuna wale wamechaguliwa sasa wale ambao wanachaguliwa hata kama wasaidizi ni akina mama watano watoke kila mkoa pia wawe watashirikiana na wale wengine.

**Com. Asiyo**: Kwa kazi gani?

**Mariamu**: Kwa kazi ya huko bunge.

**Com. Lethome**: Na katika Council na baraza la jiji unasema aje?

**Mariamu**: Mabaraza ya Council pia wakina mama wahusike.

**Com. Lethome**: Sasa wahesabiwe viti ama wapiganie kura na wanaume pia?

**Mariamu:** Wanaweza kupangiwa kama wakina mama.

**Com. Lenaola**: Kama ngapi?

**Mariamu**: Kama ni ishirini basi wakina mama wapewe vitano eh..

**Com. Lethome**: Asante Bi. Mariamu **(clapping).** Tunataka mama mwingine pia. Hilda Watella.

**Hilda**: Asante. Mimi kwa jina naitwa Hilda Mwatella. Kwanza naonelea majimbo maoni yangu kwa sababu wakina mama hasa tuko na shida sana na maneno haya ya ufa. Kuna mila ya huku ambayo ukifiwa na bwana wako lazima uchukuliwe na bwana ako mdogo ama mkubwa. Sasa siku hizi ni za ukimwi unampata yule bwana wako kumbe amejaa ukimwi. Mambo hayo mimi maoni yangu naona yaondolewe kabisa yasiweko.

Pili, kuna mambo ya kunajisi. Wakina mama wananajisiwa ovyo ovyo na watoto pia wananajisiwa na na wazazi wao. Sasa watu kama wale maoni yangu, wakipatikana wale wakatwe ule mdudu wao (**laughter**) utupwe kabisa! (**laughter**) Maoni mengine Rais akiwa mume, Vice awe Mama naye, iliwaonekane akina mama nao wanaendelea. Ni hayo.

**Com. Asiyo:** Ningependa kuuliza hivi. Yule Rais mwanamume atakuwa amechaguliwa na wananchi. Je, huyu mama kama

hakusimama na hakuchaguliwa na wananchi, awezaje akawa makamu wa Rais?

**Hilda:** Tunaonelea hata akina mama pia wafae kuchaguliwa na wananchi.

**Com. Asiyo**: Kwa nchi zingine za Kiafrica wanaweka uchaguzi wa wanawake. Kila chama kinasimamia mwanamke; wanakuwa na uchaguzi wao pekee yao. Halafu mwanamke moja akichaguliwa na chama chake anaweza kusimamia wanawake. Halafu tena kunakuwa na uchaguzi wa watu wote. Wanawake wenye nguvu pia wanaweza kusimama wakachaguliwa. Je ungesema namna gani kwa uchaguzi wa namna hiyo?

**Hilda:** Uchaguzi kama huo pia ni sawa.

**Com. Lethome**: Mama umesema kuna mila kama hiyo ya ufa ipigwe marufuku. Sisi kama tume ya marekembisho ya katiba tumeabiwa tuheshimu mila za watu, na tuendeleze mila na tamaduni za watu. Sasa sijui ungesema nini ikiwa ufa ni katika utamaduni au mila za Giriama na sasa unasema zipigwe marufuku. Hii tutawezaje kuweka pamoja haya mawili, huku twataka mila idumishwe na utamaduni udumishwe na huku twasema tupige vita. Vipi?

**Hilda:** Sasa kwa mfano kuna mila ya msitu usikatwe, hiyo tutaiacha. Lakini kama haya yaeneza magonjwa lazima tuyaondoe. **(clapping)**

**Com. Lethome:** (inadible) Bwana Gideon Kaingu.

**Kaingu:** Mimi kwanza kuna maswali nilikuwa nataka kuuliza sijui kama itawezekana. Jina langu ni Gideon Kaingu. Mimi kwanza nina hii memorandum ya watu kama kumi na tano ambao tumependekeza tayari. Lakini kuna mambo mawili matatu hivi yanichoma. Hayo ni maswali sijui kama itawezekana.

**Com. Lethome:** Yaulize.

**Kaingu:** Sasa maswali yangu ni kuwa hii elimu ya civic education ya kurekebisha katiba. Kuna sehemu nyingi katika hii sehemu ya Kaloleni Division. Kuna wengine hawajaipata, na hii nafikiri kuna ulegevo fulani katika tume. Maanake kuna vijana wengine ambao wametumiwa kufanya hiyo kazi na mpaka dakika hii hawajapewa chochote ambapo hiyo imerudisha nyuma. Watoto wale wamefanya hiyo kazi wakitegemewa watapata chochote na ni watoto ambao wametoka maskuli na mpaka sasa wamefanya mpaka nyinyi mumefika na hawajapata kitu. Sijui tatizo hilo mtaweza kutatua namna gani?

Na katika hii memorandum yetu tumeandikisha kila kitu kwa watu kumi na tano lakini tulikuwa tumesahau kitu moja, wananchi. Katika kwa wananchi tulikuwa tunataka mtu akiwa mwananchi ambaye amezaliwa hapa Kenya wakati wa kubatishwa anapewa kitabulisho maanake akiwa mchanga atapatiwa ile Birth Certificate. Lakini akifikisha miaka kumi na nane tunaomba

serikali iwe ikimpatia passport, visa, ili akitaka kwenda kule anahitajika iwe si tatizo kuitafuta tena. Akipata kitambulisho anapata na ile passport kabisa. Kwa hivyo yangu ni hayo na yale mengine yote yako hapa ndani.

**Com Lethome**: Sasa ungependa nini iwe udhibitisho wa uraiya - Birth Certificate, kitambulisho au passport?

**Kaingu**: Birth Certificate na kitambulisho itaonyesha uraiya lakini hali ya kwenda nje tunaona vijana wetu wanapata taabu wakati yeye anatakikana kwenda kule akianza kufuata yale mambo ya kupata passport, ule muda unafika wa kwenda nje passport hajapata. Kwa hivyo tulikuwa tunaonelea hiyo irekebishwe ili wakati ukifika anafuatilia vitu vidogo tu, kile kitabu yu ncho tayari. Lakini, kama anaanza application mpaka hiyo ipatikane mpaka habari ya visa, hiyo inachukua muda inakuwa mtu anapewa mwezi mmoja passport inachukua karibu miezi tatu. Kwa hivyo ile nafasi yule kijana anakosa.

**Com. Lethome**: Lakini pendekezo lako hapa ni kila Mkenya awe na passport au utalatibu wa kupata passport urahisishwe?

**Kaingu:** Mimi nafikiria kila Mkenya awe na passport.

**Com. Asiyo:** Umesema kwamba memorandum mulioandika imeshika kila kitu lakini hatujui ni nini tungependa. Pengine tungependa kuuliza maswali. Unaweza kukieleza kwa kifupi sana mambo muhimu kwa hiyo memorandum ili na sisi tuweze kukuuliza maswali kulingana na yale yako?

**Kaingu**: Katika memorandum yetu kwanza tumependekeza majimbo na hiyo majimbo tulikuwa tunataka pia vile vile katika uchaguzi wa kuenda bunge mtu awe na elimu kiwango ya Form 4 kuendelea mbele. Pia Councillor wawe namna hiyo. Na pia katika uchaguzi wakina mama inasemekana wanaonewa kidogo. Lakini tulikuwa tumependekeza mama ambaye ataweza kupigania mwenyewe kupata kura kwa wananchi kuenda bunge aende, lakini pia vile vile katika ile nomination tulikuwa tumeonelea kwa vile itakuwa viti kumi na mbili nomination nusu wawe akina mama na nusu wawe wanaume. Tena ile nomination tunaonelea iongezwe badala ya kuwa 12 iwe 14 hivi ama 16.

**Com. Lethome**: Ni nani raia wa Kenya, ni mzaliwa wa Kenya au ni mtu ambaye mzazi wake ni wa Kenya?

**Kaingu**: Mzaliwa wa Kenya na pia mzazi wake awe pia hapa Kenya na vile vile mbari (clan) inasimama na mume. Sasa tuseme mimi nikioa Muhindi sasa ule mama wa Kihindi nikiwa naye hapa yeye sasa amekuwa Mkenya. Sasa hata wale watoto tukiwazaa wale ni wa Kenya.

Na yule Mujerumani labda anaye, yeye tuseme amezaliwa nyumbani, sasa yule mtoto atakuwa automatically ni Menya.

**Com. Lethemo/Asiyo: (not clear)**

**Kaingu:** Mujerumani akuje hapa? Kama amependa kuketi hapa itabidi apply ucitizen.

**Com. Lethome:** Hawezi pewa moja kwa moja?

**Kaingu:** Asipewe moja kwa moja.

**Com. Lethome:** Na ule mke wako wa Kihindi ata apply ama apewe moja kwa moja?

**Kaingu**: Ule mke wangu wakihindi apewe moja kwa moja sababu ni wangu **(laughter)** ule ni wangu bwana, apewe moja kwa moja. Lakini yule maanake kimila tunajua mume ndiye anaowa bibi kwa hivyo bibi hawezi kuowa bwana.

**Com. Lethome:** Bwana anaweza kumpa mke wa nje uraia, lakini mke Mkenya hawezi kumpa bwana wake uraia?

**Kaingu:** eeh mke hawezi kumpa bwana uraia wa hapa mpaka aolewe.

**Com. Lethome**: Asante. Akina mama wasikia? Tuendelee, Richard Tsuma.

**Richard Tsuma**: Mimi naitwa Richard Tsuma. Nazungumza upande wa kubandilisha Katiba. Mimi nazungumza upande wa Pension. Ukiangalia watu wa pension kwa malipo yao, inaletwa kimwezi lakini inakuja kuchelewa, kwa hivyo katiba inaweza kubadilishwa kwa sababu kuna watu wanapata kama tarehe ishirini, ishirini na nne ambao wachelewa. Na upande mwingine, ukishtukia kwamba upande wa pension wa maongezo ya pesa, halafu hii pesa ikiwa imeongezwa, imepangwa kama mara tatu. Hiyo mara tatu haiji ile kawaida. Kwa hivyo pendekezo ningelipendelea iwe kama ni kuongezwa ama ni ile ya jumla wataletewa jumla watu wa pension kuliko mafungu matatu Yangu hayo.

**Ngonzi:** Kwa majina naitwa Mwinga Ngonzi. Mimi ningependa pendekezo langu liwe la serikali ya majimbo. Maana ningesema hivyo, vitu vingi hapa kwetu haviko, viko Nairobi ambavo tunavikosa hapa, kama University na shule zile kubwa kubwa tunakosa maana ndio tunataka serikali ya majimbo. Na serikali ya majimbo tukisema hivyo si kusema tu tunataka majimbo ndivyo ndugu zetu wa bara waende kwao, la, tunataka tushirikiane pamoja, ule usawa uweko. Ikiwa ni kazi tunafanya pamoja lakini ajuwe huyu ambaye ana jimbo lake ajuwe kwao ni wapi na sisi kwetu ni wapi. Hiyo ndiyo na penda mimi.

Na nikirundi upande wa mahospitali, sisi tunaona kidogo kuna utesi katika siku hizi kwa mahospitali. Mgonjwa pengine akikaa pale kwa siku nyingi kwa hospitali halafu ule mgonjwa atakufa, hatapona halafu unaambiwa utalipa bill ya hospitali na yule mtu hayuko. Ningetaka hiyo iangaliwe. Kama mgonjwa amepona basi tunaweza kulipa, lakini kama amekufa hiyo ifikiriwe.

**Com Lethome:** Tuambie wewe unataka iwe aje?

**Ngonzi:** Tunataka yule ambaye amekufa isilipwe kama imebaki pesa, isilipwe, maanake amekufa.

Langu lingine ni kuhusu mambo ya lisensi. Lisensi, kuna biashara ndogo ndogo na utaona pengine mtu amelima tomato zake, amelima mhogo wake, pale pengine atakwenda ang'owe mhogo ule pale aje achukuwe chuma lake, pengine na afanye fanye apate chochote cha kumsaidia anaambiwa atowe lisensi pale, na ni kitu ambacho kimetoka shamba. Hiyo ningetaka iondolewe, hiyo haifai. Haja ingine sisi hapa kwetu tuna kazi ile ya kupanda juu, kazi ya kugema. Tunataka yule mtu ambaye ananunua ile pombe mnazi kutoka kwa mgema yule ndiye akate lisensi, lakini ule mgema kazi yake ni ngumu. Akitoka kule juu akianguka mambo imeharibika juu amekufa kabisa asiwe na lisensi. **(laughter/clapping).** Kwa hivyo yangu ni hayo tu.

**Com. Lethome:** Na muuzaji?

**Ngonzi:** Muuzaji awe na lisensi tu.

**Com. Lethome:** Tuambie kidogo kuhusu mambo ya polisi **( not clear )**

**Ngonzi:** Polisi akifika pale akimuona yule mtu anauza ile pombe na an na ile lisensi asimsumbue kabisa maanake yeye ana kibali cha kuuza ile pombe.

**Com. Lethome:** Asante Bwana Ngonzi. Danda.

**Danda:** Asante. Jina langu naitwa Danda. Natoka Mwanamwinga location. Pendekezo langu la kwanza. Lengo langu ni kwamba nasikia kwanzia clasi cha nane, ndiye ambaye anaweza kusimamia katika udiwani. Mimi pendekezo langu, mtu akiwa anapendwa, ninaona kutoka wakati wangu mpaka wakati huu nimeona madiwani waliokuwa wakiongoza walikuwa wengi, wengine hawakusoma na walikuwa wakiongoza vizuri sana. Hata machief, walikuwa wakiongoza, tena walikuwa wengi hawakusoma. Hii ni kusema kwamba, mpaka mtu wa kusoma inamaanisha kwamba, wale ambao hawakusoma basi wakati wa kura wangeachwa nje **( laughter )** wangeachwa nje---- tusijaribu mapendekezo, kujaribu kuona kubagua kiundani, nituseme, yule ambaye anapendekeza kuchaguliwa kutokana serikali hii tunayoipenda ya majimbo ni mtu ambaye anapendwa na wananchi. Hiyo ni ya kwanza.

**Com. Asiyo:** Lakini wewe hujatuambia kama unapenda serikali yako?

**Danda:** Lengo langu ni la majimbo mama. Lengo langu mimi hata naweza kusimama kwa sababu kule kukaa kunaweza kuwasha. **( laughter )** Mimi ni majimbo. **( clapping )** Mimi ni majimbo. Majimbo haya ni kila kitu chochote abacho kiko hapa

ndani ya majimbo. Tukione wenyewe. Kwanza, mama na nyinyi ndugu Macommissioners nashukuru. Ikiwa majimbo haya tumepata si majimbo ya kufukuza mtu, ni Majimbo ya kuona kila zao la, la majimbo liwe linakutana na wenyewe mwanzo. Kwa sababu tuseme majimbo alafu majimbo haya tukikuta katika chuo kikuu kiwe kiko Nairobi la. Chuo kikuu majimbo kiwe kiko pale. Bandari iwe inatoa kitu cha kutufaidisha, ni sisi wenyewe tunafaidika hapa. Ninaona mambo ambayo sasa katika ki majimbo kuna nchi hii ardhi yetu tunauza. Kwa mfano, nitatoa mfano wa mtambo wa mabati Mariakani. Mtambo wa mabati pale pakiwa pameuzwa imefanya katika wale familia pale ambao wameuza, wamekula wamemaliza lakini pale kama kumekodisha, wale walio pale wangepewa ule uridhi mpaka vizazi vingine wanapokea, akiwa yule ametunda anaona amechoka aondoke pakodishwe na mtu mwingine. Sisi pale tungekuwa sisi wenyewe tunaona raha sana. Lakini lengo ni kwamba tuone furaha hiyo ya kimajimbo. Lakini hatuna majimbo ya kusema mtu tumfukuze sababu hatumtaki, la. Lakini hii majimbo ikiwa sisi tuna majimbo, si mtu ajenge hapa anunue hii ardhi aone ameshiba mpaka sisi wenye majimbo atudharau. Nakufukuza mimi ( laughter ) nakufukuza dada kabisa kwa sababu mimi nimekupatia wewe umetunda, umefaidika kila kitu sasa unaona mimi tayari nimekuwa panya. Hapana. Wewe umeshiba hapa ikiwa una heshima chache, nenda bwana! Maanake tulijuana wewe umekuja huku kwenye majimbo, na mimi nikienda kule kwenu na mimi nisiheshimike nikileta dharau nirudi huku mkoa wa pwani.

Tatu. Pombe. Tunagonganagongana kwa sababu ya pombe. Macho yangu ilipokuwa nikikuta Pombe chapacha hata kule Mombasa ilikuwa chupa kubwa sana shilingi mbili. Mimi macho yangu nilipokuwa ninakuta, nilikuwa sikuti kwamba pombe ina matatizo. Sisi wenyewe ndio tulikuta pombe tukaifanya ina matatizo.

**Com. Lethome:** Tupatie pendekezo lako.

**Danda:** Pendekezo langu ni kwamba watu wakitumia pombe saa kumi mpaka saa tano inafungwa. Kama ni kilabu kinafungwa saa tano ya usiku ili waende lala.Asubuhi twakimbilia kazi hatukimbilii pombe. **( clapping )** Twakibilia kazi. Tukimaliza mambo ya kazi ni jioni starehe viredio vyetu na mambo yetu, tunaweza kupata chupa zetu. Chupa zetu tunywe pale. Tustarehe pale. Lakini hii ya kila siku tuseme pombe ikinunuliwa tupigane nini haina 'time' mimi kimajimbo nakataa. Kwa hivyo naomba kwa hayo machache. Mungu atubariki.

**Com. Lethome:** Hebu tuambie kidogo kuhusu elimu katika hili jimbo lako.

**Danda:** Asante. Elimu. Elimu mwanzo nilisikia kwamba kutoka skuli, shule ya msingi ya chini kabisa kutoka classi cha kwanza, wacha nursery, classi cha kwanza, mpaka cha nane bure, lakini bure hiyo mimi 'nangalaza'. **( laughter )** 'Inanangalaza' namna hii.
Mimi nina watoto wangu hata sasa.

**Com. Lethome:** Hebu ngoja utwambiye “kinangalaza” ni jina…………..

**Danda:** Eeeh, linanitatiza………. Kinangalaza ni kimijikenda sawa sawa. Kwa hivyo elimu hata mimi nina mtoto wangu yuko standard 6, standard 4, standard 5, enough. Lakini saa yote mtoto wangu akija anasema mzee tunatafutwa mia. Mia ya nini? Sijui mzee, nimeambiwa niende nayo. Bila hivyo basi nikae. Ah! Hii elimu ni bure? Baba nimeambiwa kama sitaenda na mia mimi nisiende shule.

Sasa pendekezo langu nasema hii elimu ni mia akili hii bure pendekezo langu ni kwamba hakuna bure. Kwa hivyo mimi naona ikiwa ni bure kutoka classi hicho ya kwanza, kalamu, kitabu, eeh.. uniform, mpaka classi cha nane. Basi huko mbele tuguzwe guzwe angalao kwamba kuna kitu gani lakini hapa tujue narudia hiyo elimu kwa watu wazima. Kule kwetu Mwanamwinga, tunapenda kusoma watu wazima, tunataka, lakini juzi nilipokuja hapo offisi ya watu wazima, elimu ya wale wazima, nauliza nilishangaa, utampata wapi huyo mwalimu ambaye atufundisha, leo afundishe, asifundishe tena mpaka ijumaa wale wazee watashika kitu kweli? Eeh tena nauliza mimi nataka alete vijana wako kule waje wachukue walete na sisi tukasome kule. Kutoka ianzishwe na serikali hii elimu ya watu wazima wengine huko juu wameendelea.

Pendekezo langu ni kwamba, wale waalimu tuwapate kwa serikali walipwe mshahara mzuri na sisi watu wazima tusome lakini kwa mia tano kwa mwezi hatutapata waalimu. Maanake yasemekana mia tano mwalimu wa ngumbaro atufundishe ndipo hata sisi watu wazima tusome waalimu mimi nimewatafuta nasi kuwaleta wanarundi kutoka huko wakija mwezi moja wanasema; "Danda sitaki kwa sababu mimi nikifundisha naende Kilifi kwa mia tano. Hiyo tikiti kutoka itamalizika mia tano"(**clapping**).

**Com. Lethome**: Asante sana Bw. Danda. Kitsao Ngumbao.

**Kitsao Ngumbao**: Mimi Kwa majina naitwa Kitsao Ngumbao. Kwanza ningependekeza kuwe na serikali ya majimbo. Kila jimbo liwe linajisimamia mambo ya elimu, uchumi, mambo ya hospitali na vitu vingine vidogo. Halafu serikali kuu iwe inashughulika na mambo ya ulinzi, foreign policy na polisi. Kila jimbo liwe na bunge lake na wabunge wa majimbo wawe wanachaguliwa na wananchi katika wakati tofauti; iwe jimbo linapanga lenyewe tutafanya wakati fulani uchaguzi wa wambunge wa jimbo. Halafu katika serikali kuu tusiwe tunategemea sana mambo ya Urais tuwe na kitu kingine kitakuwa likisaindiana na rais kuongoza, hasa nataka kuwe na kama baraza kuu hivi ya kitaifa. Hili baraza litakuwa linashauri rais hivi mambo ya foreign policy na mambo yoyote ya kuhusu hiyo serikali kuu na yale majimbo yako. Na kila jimbo liwe linatoa kiasi fulani kwa serikali kuu ile hazina yake kama 15% hivi kugharamia shughuli za serikali kuu. Halafu urais uwe kama vile ilivyo saa hii kusiwe na waziri mkuu kuwe na Rais na achague mawaziri wake vile ilivyo saa hii.

Kitu kiingine ni ule uhusiano wa serikali kuu na serikali ya majimbo. Kama kuna tofauti yoyote maanake serikali kuu itakuwa na policies zake. Sasa kwa mfano iwe serikali ya majimbo haiendi kulingana na policy ya serikali kuu iwe hii serikali kuu inashauriana na hii serikali ya majimbo kutekeleza hilo jambo.

Kwa mfano, elimu pengine katika sehemu fulani kiwango chake kiko chini ilhali katika majimbo fulani elimu yao iko juu. Serikali inaweza ikachukua "resources" kutoka sehemu hizi zingine kuhakikisha kuwa kile kiwango cha elimu katika jimbo hilo kimeongezeka.

Halafu sasa katika wabunge wa serikali kuu, wabunge wa nchi nzima sasa, kiwango kiwe ni form four, na rais awe pia ni form four bora achaguliwe na wananchi. Katika Tume ya Uchaguzi, iwe inachaguliwa na yawe ni hayo majimbo yanayotuma watu wao katika hiyo Tume ya Uchaguzi. Kusiwe na pengine watu wapelekwe kwa vyama. La. Sio Commissioners waende kwa vyama; Commissioners wachaguliwe kutoka majimbo. Vile vile katika mahakama. Hii National Council ya kitaifa iwe inachagua 'Judge' mkuu. Judge mkuu awe anachaguliwa na hiyo council ya kitaifa. Halafu 'Majudge' kuchaguliwa katoka kwa kazi iwe kuna Judicial Commission ambayo Commissioners wanatoka, wanachaguliwa kutoka kila jimbo. Jimbo hili linatoa mtu mmoja ambaye atasaidia Judge mkuu kuchagua wafanyi kazi wa katika mahakama. Halafu katika hii National Council sasa wawe ni watu ambao si lazima wawe wameeleweka sana katika siasa. La. Hao ni watu ambao wana hadhima kuu katika nchi. Wawe pengine wamefanya katika forces na wana nidhamu nzuri, wachaguliwe. Kila jimbo iwe inatuma mtu mmoja katika hiyo Council. Hao watu wanahudumu kama miaka themaninini hivi. Akichaguliwa huko anahudumu maisha. Watu ambao pengine wamefanya kazi katika private sector, wamefanya vizuri katika banking, watu kama hao wawe wanachaguliwa, ama kama ni mabalozi, ama watu wa kuhudumu katika hizi international organizations wawe wanahudumu katika hiyo National Council. Kazi yake iwe ya kumshauri Rais na jinsi ya kuendeleza hii serikari kwa mfano, mara ingine utakuta wabunge kule bunge wanalalamika kuhusu jambo fulani lakini halitatekelezwa chochote. Wanasema: “Oh pesa ziliibwa hapa …”. Kazi yao ni kulalamika ilhali wale wengine kazi yao ni kujificha ili wasitambulike. Sasa hakuna kitu kinafanyika lakini hapa wakilalamika iwe hii National Council itachukua hatua kuhakikisha lile jambo linalamikiwa linatoka wazi. Kama kuna makosa serikali ichue makosa yake.

Na katika hao wabunge wa majimbo sasa, kuwe 'areas' ni kama hizi ambazo zinawakilishwa na Councillors. Hao Councillors ambao tunachagua wawe tunawachagua sisi, wanawakilisha County Council. Wakifika kule kwa County Council sasa wanachaguana kama watano hivi katika kila County Council wawe wataenda kwa bunge la jimbo sasa. Hivo ndivyo napendekeza.

**Com. Asiyo:** Kwa hivyo unasema kwamba kila District ichague mbunge wao kulingana na vile kamati za local authorities mara tuna mwenye kiti wa local authorities alafu tuna municipalities. Sasa hapo wasema je watachaguliwa kutoka ….. (inaudible)?

**Ngumbao**: Kwa mfano tuchukuze mfano wa Pwani kuna manispaa na 'municipals'. Sasa kama ni manispaa kuna Councillors ambao wamechaguliwa pale. Wale wakienda pale wanakaa, wanachagua kama ni watano wao waende kwa ile bunge ya juu…….. Kila County Council. Hao ndio wataunganisha watengeneza hii bunge ya juu.

**Com. Asiyo**: Kwa hivyo hutawapatia wananchi wa jimbo hile la pwani nafasi ya kuchagua watu wao wenyewe. Unataka wachaguliwe na Councillors?

**Ngumbao**: Councillors wanachaguliwa na watu. Sasa wakifika kule wanachagua mwakilishi wao. Bali na hivyo ningependekeza pia kuwe kuna mtu kama mmoja hivi katika kila Constituency ambayo itakuwa inatuma mtu direct kwa hiyo bunge ya juu.

**Com. Asiyo:** Lakini unasema kutakuwa hawa Councillors watakuwa tena MPs kwa jimbo. Watakuwa ………… inaudible

**Ngumbao:** Hapana. Yeye akichaguliwa kule sasa tunachagua mbunge halafu anakuwa waziri. Hiyo kazi ya ubunge anaifanya na ile ya waziri anaifanya. Kwa hivyo kile nasema huyu mtu atachaguliwa kama Councillor huyu. Lakini kulingana na umaarufu wake na vile ataweza kutafuta hiyo kazi kwa council anaweza akachaguliwa akaenda kwa hiyo bunge ya juu.

**Com. Lethome**: Ulizungumzia maneno ya Urais ulisema ungependa kuhifadhiwe vile vile kulivyo lakini ningependa uzungumzie kuhusu mamlaka ya Rais. Una nini ya kusema kuhusu mamlaka ya urais?

**Ngumbao:** Mamlaka ya rais kwa hivi sasa ni makumbwa sana. Sasa kitu cha kwanza ningependekeza ni haya majimbo yawe yanapunguza yale mamlaka ya Rais kwa sababu badala ya Rais ahakikishe jambo fulani lafanyika huku serikali ya jimbo huku ndiyo itafanya hivyo. Halafu kuna hii National Council, kama huyu anafanya makosa kulingana na mapenzi ya waKenya hii Council inaweza ikamwambia hapa unafanya makosa. Kwa mfano kama budget ya serikali, lazima ipitie kwa bunge na tena ipitie kwa hiyo National Council. Hii National Council ndiyo itahakikisha kama hao jamaa wanafuata makandilio waliowekewa ama wanafanya makosa. Kama wanakosa wawe na uwezo ya kuwanyima pesa za hii serikali.

**Com. Lenaola**. Na je, National Council na Cabinet huoni kama wanafanya kazi moja?

**Ngumbao:** Ah ah, Cabinet vile nionavyo sasa, maanake tunaangalia kama ingekuwa hii cabinet ya Kenya inafanya kazi 'independently' maanake sasa hivi wanafanya kazi kulingana na vile rais anavyotaka. Sasa unaona Kenya mzima inaenda kulingana na vile mtu mmoja anavyotaka. Lakini tunataka tuwe tuna uwezo wa kuwa hata sisi mapendekezo yetu pengine hayaambatani na yeye vile anataka. Sasa huyu rais atachagua cabinet yake kutoka kwa bunge kama vile ilivyo saa hii. Lakini hawa kiasi kama watu kumi hivi watu ambao kwa Wakenya ni macho yetu ni watu ambao wamesoma, wana ujuzi wa kazi tofauti tofauti.

**Com. Lethome**: Rais ndiye atakeyechagua mawaziri?

**Ngumbao**: Mawaziri anateua.

**Com. Lethome**: Na je, hii National Council inachaguliwa na nani? Na wananchi?

**Ngumbao**: Nimesema kila jimbo inatuma mtu mmoja kwa Council halafu Rais anatuma mwakilishi wake kwa Council.

**Com. Lenaola**: Asante sana. Ningependa tupate Margaret Mkalle.

**Margaret:** Asante. Akina baba na akina mama hamjambo? Mimi kwa majina yangu ni Margaret Mukalle. Nimetoka Jimbana location. Ninazungumzia juu ya serikali ambaye ningetaka ituongoze. Nataka serikali ya majimbo tukiwa na rais na makamu wake. Halafu tuwe na wabunge katika jimbo na pia tuwe na bunge letu la jimbo. Sana sana, mimi nazungumzia juu ya akina mama. Kina mama ningetaka wapewe urithi sawa na mtoto wa kike na kiume wapewe urithi sawa. Urithi wa mali, elimu na heshima. Halafu ningetaka nizungumzie juu ya kurithiwa. Kina mama huku kwetu kuna tabia ya wanawake kurithiwa kama wamefiwa na waumeo. Mimi ningependa kusiwe na hali hii. Hiyo najua ni hali ya utamaduni lakini hali ya utamaduni huu ningetaka uondolewe kusiwe na kurithiwa kwa sababu ya magonjwa kadha ambayo yana tumalizia watu - ugonjwa kama AIDS.

Kunajisiwa. Kumekuwa na kesi nyingi za kunajisiwa kwa wanawake. Watoto, kina mama, wasichana na wakina mama wakongwe. Ningependekeza kwamba yeyote atakayepatikana amemnajisi mtoto, mama, msichana au mama mkongwe, afungwe kifungo cha miaka kumi. Na kuna wanaowanajisi watoto wao. Huyu ningependekeza kwamba aadhiliwe milele.

Uongozi. Uongozi wetu kama nimesema tutakuwa na Rais ningependa tuwe na Rais kama atakuwa mwanamke makamu wake awe ni mwanamume. Kama atakuwa mwanamume makamu wake awe ni mwanamke. (**clapping**)

Kazi. Ningependa kuwe na magawanyi sawa ya kikazi. Kazi aina yoyote ipatiwe mtu yeyote mradi awe anaweza. Kusiwe na ubaguzi. Mtu aina yoyote wa kila kabila na pia hata walemavu. Kwa hivyo kuwe na usawa kusiwe na ubaguzi wa aina yoyote.

Kikanisa. Ningependa (sasa hapa nitasema ni madhehebu tulionayo) madhehebu tuliyonayo Kenya yamekuwa mengi mno, kiasi ya kuwa tumeenda tumepindukia hata tunaabudu shetani sasa. Ningependa kuanzia sasa tunapoanza serikali mpya, kuwe na kiasi. Ikiwezekana madhehebu yaliyo hapo yachungwe vizuri na yapewe uongozi. Ikiwa ni watu wa Pentecostal wapatiwe kichwa moja wote wawe ni wa Pentecostal na matawi yao. Kama ni wa Methodist wao hivyo, wa Anglican hivyo, wa Catholic hivyo. Tusiwe na dini nyingi kwa sababu yametuharibia nchi. Ule uhuru wa kuabudu umeharibika. Na pia katika uongozi wa kanisa nimeona kuna makanisa mengine hayataki kuona wanawake wakiwa viongozi, wakiwa mstari wa mbele, kwa hivyo tunapoitisha mkutano wa viongozi tunakuta wanaokuja wengi ni waume. Ningependa akina mama wapewe vyeo katika kanisa, wawe wenye viti, wawe hata makasisi na wawe viongozi kwa sababu kina mama tumewaona wanayo mawazo ya juu, hata wakati mwingine washinda akina baba.

Utamaduni: Utamaduni wetu ni mzuri sana lakini maombi yangu ninataka tuchague katika utamaduni wetu kwa kuwa utamaduni mwingine ni mzuri na mwingine ni kama ule nilitaja mwanzo, kama wa kurithi wanawake. Ningependa kwamba tuchunguze hali yetu ya utamaduni kwa sababu utamaduni wetu umepotea hata heshima hakuna kwa sababu tumeingiza tabia za kigeni na tunaona hata mavazi yetu yamebadilika. Unaona watoto wanaenda bila nguo mbele ya wazazi wao. Ningependa kuwe na mavasi rasmi ya kutoka mkoa wa Pwani na Kenya mzima kwa jumla. Wanawake na wanaume tuwe na mavasi ya kufanya ajulikane yule ni mwananke wa Kenya, mwanamke mwenye heshima.

Usalama. Katika usalama ninaona wakati mwingine usalama wetu polisi wetu wanatutatiza mara nyingi. Kwa hivyo ningependa kuwe na hatua kamili ambayo itachukuliwa juu ya polisi ambao wanatatiza wamama wakienda na biashara zao ndogo ndogo. Hatungependa kuwa na polisi kama hawa tulionao sasa kwa sababu wamejaa sana hongo. Kwa hivyo kule kuendelea kwa watu kumezorota kwa sababu unakuta mtu amenunua matatu yake anakula sawa sawa na polisi. Kwa hivyo na polisi usalama. Na pia tuwe na usalama mahali popote kwa sababu siku hizi nikiwa nasafiri hata nikikuta polisi njiani siwezi kumuuliza njia au kumwambia pengine anisaidie kwa sababu unamsaidia na yeye pengine atakunajisi. Kwa hivyo tunataka tuwe na polisi ambao wana nidhamu ya hali ya juu.

Matibabu. Tungetaka tuwe na madaktari waliosoma sana na matibabu ikiwezekana yawe ya bule hata katika dispensaries. Dispensaries, Health Centres zitoe matibabu ya bure ili tuweze kusaidia watu wetu na kuokoa maisha ambayo mara nyingi inapatikana kwa kukosa kutibiwa vyema. Na pia haya madawa ya tembe wakati yanapotengenezwa yachunguzwe kwa sababu tunaona watu wengi wanakufa kwa sababu hawana pesa za kugharamia yale matibabu. Ni vizuri wale wasio na kitu, mtu akija aeleze hana kitu kabisa aangaliwe.

Shamba (Land): Mashamba yetu tungetaka kwamba, kama tutakuwa na serikali ya mkoa tunajua ya kwamba kila kitu kitakuja katika mikoa, kwa hivyo "title deeds" zitolewe kwa wanaume na wanawake. Kila aliye na haki ya kupata apatiwe "title deed" bila kutatizwa. Na hii iwe ya haki kabisa.

Dawa za kulevya: Dawa za kulevya zimezidi na tunaona vijana wetu vile wamekuwa hali ambayo hatujui kama tutakuwa na viongozi. Hata hatuna matumaini ya kwamba tutakuwa na viongozi. Hata tukiangalia naona tuna vijana pale. Ni viongozi lakini hatuna matumaini ya kuwa na viongozi wazuri kwa miaka mitano inayokuja kwa sababu watoto wote ambao ni “graduates” hata wale ambao hawakusoma sasa wote wameharibiwa na dawa za kulevya. Kwa hivyo ninapendekeza tuwe na adhabu kamili juu ya wale watakaopatikana wakiuza vitu hivyo. 'Agents' wachukuliwe hatua ya hali ya juu. Alafu na wale wanaouziwa nao, waadhiliwe kiasi ya kuwa mwenzake akisikia ataogopa. Mungu awabariki. (**clapping)**

**Com. Lethome:** Ungependa mwananchi akidhulumiwa na polisi, au akinyanyaswa na polisi, akalalamike kwa nani?

**Margaret:** Akalalamike kwa mkuu wa polisi katika ile 'area'. Kila mahali wako na mkuu wao alalamike pale na ikiwa atapatikana na hatia polisi huyo afungwe ikiwezekana maisha.

**Com. Asiyo:** Kuna wengine wametueleza ya kwamba kwa vile polisi (not clear) na Polisi mwenzake ungependekeza kuwe na polisi kila mahala?

**Margaret:** Napendekeza kuwe na ofisi katika Head Office ya mkoa ambayo itakuwa inangalia hali hizo katika kila sub-location.

Com. Asiyo: Lakini (not clear) mambo ya afya.

**Margaret:** Nimesema kwamba mambo ya afya iangaliwe na ikiwezekana matibabu yawe ya bure, ndivyo nilisema. Kuwe na matibabu ya bure katika dispensary na health centers. Mtu akienda pengine kulazwa huyu ndiye sasa hali yake iangaliwe na uwezo wake wa kuweza kugharamia iangaliwe. Kama hawezi serikali ichukue jukumu la kumlipia huyu mtu kwa sababu tunataka aendelee kuishi na atusaidie. Na yule mwenye uwezo afanye tu kwa sababu kuna watu wenye pesa millioni moja anaweza toa.

**Com. Lethome:** Asante sana Bi Margaret. Na sasa ningependa kumualika Mheshimiwa Matheas Keah aweze kuja atambie machache aliyo nayo na zaidi aliyotuahidi jana. Karibu Mheshimiwa.

**Com. Lethome**: Asante sana Bi. Margaret. Na sasa ningependa kumualika Mheshimiwa yuko na shughuli nyingi na jana alikuwa na sisi kwa hivyo ningependa kutoa nafasi hii kwa Mheshimiwa Matheas Keah aweze kuja kutuambia machache aliyonayo na kama anayo zaidi na pia kukabithi aliyotuahidi jana. Karibu Mheshimiwa.

**Hon. Keah**: Asante Macommissioners, karibuni Kaloleni Constituency. Leo naendelea kutoa pendekezo ambayo mapendekezo haya yanachanganya mawazo yaliyotolewa na baathi ya wananchi wa Kaloleni waliokutana tarehe ishirini na sita na pia ishirini na nane katika ukumbi huu huu na kwa hivyo hapa ni mchanganyiko wa maoni tofauti tafauti ambayo yametoka kwa wananchi na wananchi wale kuna wengine ambao hawakukubaliana na maoni haya wako na uhuru watatoa mapendekezo yao wenyewe binafsi.

Basi sisi tulikubaliana kwamba tutafuatia msururu ulioko ama uliotolewa na muongozo wa Tume ya Katiba. Kwanza, utangulizi unahitajika na uweko katika Katiba mpya. Na utangulizi huu useme maneno yafuayo. Kwamba hii ni katiba yetu inayotengezwa na wa- Kenya wenyewe sio kama ile ya '63 ambayo inataka amani, upendo na umoja kwamba wananchi watawaliwe kidemocrasia na kwamba mapendekezo wa wananchi ndio yafuatilizwe ni serikali, utangulizi huu usimulie jinsi tulivyotoka uhuru mpka sasa na ukiatambua maendeleo yaliofanywa na ufanisi ambao hujapatikana hasa katika upande wa

uchumi, katika upande wa social hayo yote yawe katika utangulizi ule.

Sura ya pili ambayo itazungumza katiba iseme filosofia yetu na mwongozo wetu uwe serikali hii ni ya watu wenyewe kwa manufaa ya watu wenyewe na iwe ni kwa wao wananchi wenywe. Kwamba demokrasia au jinsia za kidemokrasia ziwe na mambo ya "Human Rights" haki za mwanadamu, uhuru wa kuabudu Mwenyezi Mungu na sio kuabundu "devil worship" ah ah hiyo uhuru wa kuabundu Mwenyezi Mungu na uhuru wa kujiassociate vile inavyowezekana. Kwamba nchi yetu ni jamhuri na iheshimike kijamhuri na mamo haya yote basi yaweko katika katiba.

Sura ya tatu, kwamba katiba ndiyo sheria kuu kuliko katiba zote zingine na kwamba kwa sababu tuna vyama vingi viko vitakuwa vikitutunza katika mabadiliko ya katiba.

Bunge iwe na ruhusa ya kuweza kubandilisha katiba mradi tu asilima sitini na tano ya wa bunge wote waweze kuipigia kura hiyo - minimum 65%. Lakini, hata pamoja na hivyo hii sio kibali cha Wabunge waichezee chezee katiba na kujaribu kuibadilisha mara kwa mara.

Kuna viwango fulani vya katiba hii ambavyo kubadilishwa kwake ni lazima ziende kwa wananchi kama kwa mfano sisi hapa pwani tumependekeza au tutapendekeza hapa serikali ya majimbo. Na hilo ni fungu langu moja ambalo serikali ya majimbo ikiwa na ibadilishwe basi ni lazima nchi iende kwa 'referendum' ni kiwango kama hicho ndicho kinataka referendum lakini mambo mengine bunge linaweza kubadilisha katiba.

Wananchi (citizenship). Hilo “automatic citizenship” ni ya mtu mzaliwa ambaye babake Mkenya na mamake ni Mkenya. Hiyo ni automatic. Bibi mgeni aliyeolewa na Mkenya citizen au Mkenya citizen aolewe na bwana mgeni yule mgeni atapewa uraia wa Kenya akiomba maombi na ikiwa tabia yake yafaa na ikiwa yeye ana manufaa fulani kwa nchi. Yani kuoa tu mgeni sio automatic. Pia vile vile ikiwa foreigner, kama Mjerumani amepata mtoto na bibi ambaye ni Mkenya au vice verse bibi Mkenya amepata mtoto na Mjerumani, mtoto yule awe na haki ya kuwa Mkenya. Awe na haki. Na pia vile vile katiba iseme ya kwamba, Mkenya atabaki kuwa Mkenya hata aende ulimwengu gani au awe na citizenship ya nchi ingine Mkenya anabaki na hati yake ya Kenya. Mfano ulitolewa kama wa Kipketer yule aliyeko Sweden. Yeye sasa ni Mswedish lakini sisi wa Kenya tutabaki na yeye kama huyo ni Mkenya wetu tunamhesabu kama Mkenya wetu.

Usalama na National Security. Wakati wa recruitment, recruitment ipewe quota sawa sawa, army navy na airforce. Kila jimbo lipatiwe sawa recruitment sawa sawa quota yake na tena watu wale wawe ni wa Kenya. Pia polisi iwe ni ya wa -kenya na polisi haswa wawe recruited katika kila jimbo lakini wote wapelekwe huko Kiganjo. National Youth Service iendelee na pia iwe na quotas katika kile jimbo. Na President aendelee kuwa Commander-in-Chief wa Armed Forces.

Political Parties - kazi yao kubwa ni kuhamazisha kwamba mambo ya kisiasa na kuona ya kwamba wananchi wa Kenya wa

mefahamishwa kisiasa zaidi. Hata hivyo vyama vya kisiasa vitasaidia pia katika miongozo wa kisocial na economic katika kuendeleza nchi. Pia vyama vya kisiasa visajiliwe hata kama ni vyama mia moja viendelee kusajiliwa mradi tu viweze kufuata sheria na mwongozo ya vyama iliyoko. Kwa mfano kama mtu ni bankrupt, asiruhusiwe kuanzisha chama. Mtu akiwa ameiba mamillioni asiruhusiwe kuanzisha chama. Na vyama viambiwe ni katiba kwamba wahakikishe kuna nidhamu katika vyama vyao, na vyama vijigharamie wao wenyewe na kwamba pia vile vile watu waongozwe ni nidhamu katika vyama badala ya kuhama chama hiki leo, kile kesho kutwa mtondo chama kile kingine basi vyama vyenywe viwe na sheria ya 'kuregulate' uhamaji ule kwa sababu hatutaki watu wengine waliita "political prostitution". Hiyo haidhibiti democrasia.

Structures na Systems za Government. Yaani serikali za aina gani? Sisi hapa tunataka serikali ya majimbo na kutakuwa na serikali ya majimbo au Regional Government ambayo inalingana na Province kwa hivi sasa na pia kutakuwa na serikali ya National kama iliyoko sasa kule Nairobi. Serikali hizi Wabunge wake watachaguliwa na wananchi wenyewe na haya yatasaidia kuendeleza mambo ya 'governance', uabijikaji na utawala kwamba kila Mkenya ahusike katika utawala na keki iliyoko katika nchi hii.

Kuwe na 'checks na balances'. Pia kuwe na 'accountability ya public funds'. Tuheshimu ethnic, regional diversity yaani mambo yale yote ya regional yaheshimiwe, communal rights of culture and identity zote ziweze kuheshimiwa. Na uchumi uendelezwe kila mahala nchi nzima sio tu sehemu fulani fulani. Power should be shared between the National Assembly and, Regional Assembly. Kuwe na mpangilio wa kugawanya kazi maluum. Na hapa tuna mifano kadha wa kadha kwamba kazi ya fedha, kazi ya ulinzi, kazi ya international relations hizo zitapewa serikali kuu. Lakini serikali ya majimbo inapewa mambo yanayohusu lile jimbo pale kama local government mambo ya social services, mambo ya kilimo na mambo yanayohusu watu wenyewe pale. Regional assemblies – mapato. 10% ya mapato yanayotokana katika regional ndiyo yapelekwe serikali kuu na 'region' yenyewe iwe na 90%. Kukiwa na chochote kinachotoka nje basi kigawanywe sawa sawa.

Lands/Ardhi iwe chini ya mamlaka ya 'Regional Authority'. Kilindini Port 'specifically' mapato yake yawe hapa Pwani. Mapato ya port ya Kisumu yatakuwa ni ya watu wa Nyanza na wengine ambao wana kahawa mapato yao yatabaki huko huko na only 10% iende kwa serikali kuu. Ma-DDC Chairmen na Heads of Depts. (i.e. District Development Committee) wawe na mamlaka na watokane na kule jimboni. Katiba lazima itunze haki za wale walio hawajiwezi (marginalized groups).

Katiba pia vile vile ijapo tuna serikali ya majimbo lakini kuwe pia na National Unity itakuwa ni kazi ya serikali kuu kuhamazisha National Unity. Tunataka committee maalum siyo ya wabunge ambao watakata mishahara ama wataamua wabunge wapewe mishahara namna gani. Sio wabunge wenyewe wajipangie mishahara yao. Representation - bungeni, kina mama tuna majimbo manane, kina wamama watano kutoka katika kila jimbo (automatic) na akina mama watajichagua wao wenyewe. Hakuna mtu atakayewaingilia (**clapping**) pia vile vile kila jimbo litakuwa na disabled angalau mmoja na ia vile vile youth mmoja hiyo ni automatic (**clapping**). Na vijana wa jimbo wawe wenyewe ndio watakaochaguana kinamna hiyo hiyo.

Mbunge ana miaka mitano bungeni kwa hivyo akiwa ni mlaghai wananchi watamuona baada ya miaka mitano (**clapping**) sio baada ya miaka miwili ama ni tatu aletwe apewe barua ya kustaafisha ah ah. Yule amechaguliwa atabaki kule miaka mitano na ikimalizika miaka tano wananchi wenyewe wataamua kama watamregesha au namna gani. Kuwe na 'tests' ili Mbunge akienda kule na hata vile vile diwani aweze kuwa anachangia.

Legislature tunaingia huko sasa- Parliament. Parliament. Uwezo wa parliament utakuwa namna gani? Parliament itaangalia qualification, competence na ujuzi wa watu ambao watakuwa na Constitutional offices kama Majudge, Permanent Secretaries, Ministers, Commissioners kama nyinyi na Heads of Government parastatals. Wao Parliament ndio watakaokuwa wata 'vet' na kuona ya kwamba hawa watu wanafaa au hawafai, ni mazungumzo kutoka Kaloleni. Parliament iendelee kwa kujitawala na mambo yao ya kindani ya bunge through standing orders. Mbunge awe kwa ile miaka mitano kule na entry age, umri wake watu wa Kaloleni wamesema ishirini na tano. Entry ya President iwe miaka alubaini, na akifikia miaka sabini na tano basi astaafu. Mbunge awe na elimu ya form four, na President awe na elimu ya Bachelor degree na pia kuwe na moral na ethical considerations. Kama mtu, kwa mfano, alishikwa na kunajisi kama ilivyoitamkwa, awe mtu amekuwa bankrupt, au mtu ameshtakiwa na akahukumiwa na kupatikana na kosa la ulaghai ama corruption, mtu yule hafaai kuwa Mbunge, mtu yule hafai kuwa Rais.

Kusimamia urais ni lazima watu wasiopungua hamsini kutoka kila Constituency, waweke sahihi kwamba wewe tunakuhitaji katika kila Constituency kuwe na watu angalau hamsini ili huyu Rais awe ni mtu wa kitaifa. Tunatambua hivi sasa ni watu elfu moja kutoka kila jimbo lakini sisi tunasema ukiwa utakuwa Rais, usiwe tu Rais kule jibana lakini uwe Rais katika kila Constituency uwe na angalau watu hamsini.

Parliamentary powers to veto the executive ziweko yaani Parliament iwe pia supreme na President awe na powers zake vile vile za kudisolve Parliament. Members of Parliament na Rais ni lazima wawe ni wacha Mungu. Wawe wanamcha Mungu. Na tena waseme rasilimali yao na madeni yao yako kivipi tusije tukaaibishwa ni Raisi ambaye amejaa tele madeni na ashtakiwe kwa madeni yake.Na pia defections kutoka chama hiki mpaka kile kwa wabunge na hata raia. Kuwe na amri ngumu zaidi katika kila chama cha kuzuia mambo kama yale lakini watu wa Kaloleni wanasema mbunge kama anataka kudefect basi lazima apate angalau kura elfu moja, watu signature elfu moja kuonyesha yeye kweli si mtu wa kurandaranda tu ni kweli anapewa idhini na watu waliomchagua kwamba asiranderande asiwe malaya wa kisiasa.

The Executive: Katiba hii ya majimbo itakuwako na mambo yafuatao. Kuwe na Rais, na Vice wake lakini powers zao zipunguzwe. Zikipunguzwa powers zile zitakwenda wapi? Zipunguzwe maanake sasa Rais ndiye kila kitu, ana powers nyingi lakini zipunguzwe ili powers za kuendesha mambo ya bunge zipewe Prime Minister na Vice Prime Minister maanake utazipunguza utazipeleka wapi? Ukizipunguza lazima umpe mtu mwingine. Hivi sasa Rais yuko bungeni, Rais yuko executive, Rais yuko kila mahala hata Judiciary pia yuko Rais. Hiyo tunaona kuna hitilafu fulani. Zikipunguzwa zile za ubunge, leader of government business awe ni Prime Minister akisaidiwa na deputy wake. Na bungeni pia vile vile kuwe na leader wa official

opposition huko bungeni na hawa wote wawe Kenyan citizens by birth- kwa kuzaliwa. Constitution pia ikubali iandike yafuatayo:-

- Maximum age ya Rais iwe sabini na tano,
- Na Raisi awe na Bachelors Degree,
- awe endorsed na 50 registered voters in each constituency.
- President na Prime Minister wanaweza kuwa na tenure of office ya miaka kumi mfululizo ikiwezekana lakini isizidi miaka kumi ya terms za miaka mitano, mitano.

Kwa mfano, katika upande wa Rais kazi zake kubwa zitakuwa ni kazi za security, Head of State, yeye ni mkubwa katika ile sarafu ya Kenya maanake yeye ni kiunganisho wa nchi. Na Rais apate asilimia hamsini na moja (51%) za vote zote zimekuwa passed. Na isitoshe, awe na asilimia ishirini na tano za votes katika 5 provinces. Pale mbeleni tumesema kuidhinishwa lazima awe na hamsini, hamsini signatures katika kutoka kila constituency lakini kuwa Rais apate asilimia ishirini na tano kutoka kwa majimbo matano na tuko na majimbo manane. Ikiwa kiti cha Rais kita 'fall vacant' basi atakayeingia pale ni vice wake. Lakini, kuwe na uchaguzi ndani ya siku tisaini. Tunaingia Judiciary.

Tunasema Presidential Structure sisi inatutozelesha lakini kesi zinarundikana miaka tano, miaka kumi. Hio urundikano wa kesi huo katiba hii iseme ya kwamba kila kesi izungumzwe ikizindi sana ndani ya mwaka mmoja. Na judiciary ifanye vyovyote ifanya vyo lakini judiciary ihakikishe ya kwamba kila kesi imezungumzwa ndani ya mwaka mmoja. Sio watu wasafarike, wasusurike kwa muda wa miaka tano, kumi na kesi haizungumzwi.

Constitution itambue ya kwamba local communities sio kila kesi inaweza kwenda hizo korti kubwa, kubwa. Local communities na elders watumike na akina mama waweko ndani ya hayo. Judicial Service Commission lazima ikiwe vetted by Parliament. Judicial powers of state na court elders tushazungumza mambo yake. Constitution/Katiba pia ihakikishe ya kwamba civic education inaendelea kila wakati sio tungojee tu wakati wa uchaguzi au wakati wa kutengeneza katiba ndiyo kuwe na civic education. Katiba ihakikishe, hii ya sasa, elimu ya raia imeendelezwa na hasa iwe syllabus kutoka primary school.

Local Government. Sisi tunatambua ya kwamba kuna serikali ya uraia. Hizo zitaendelea. Mayors na Council Chairmen wachaguliwe na wananchi wenyewe na mishahara yao Macouncillors pia ilipwe kutoka kwa consolidated fund au na serikali ili wasije wakalia lia kila wakati hawajapata allowances zao. Tumesema Heads of Departments, Chairmen, DDCs, wote wawe wenyenji pale. Councillors term yao iwe ya miaka mitano sio kubadilishwa badilishwa kila baada ya miaka miwili. Wawe na umri wa miaka ishirini na moja, elimu ya Form 4 au equivalent lakini wengine walipinga wakasema hata Std. 8 aweza kuwa lakini watatoa yale maoni tofauti na haya. Ilikuwa ni wengi wape!

Waziri wa local government asiwe na idhini ya kuvunja baraza hilo na Councils should be answerable to Regional Assemblies. Kama waziri hatakuwa na nguvu hizo basi nguvu hizo zipewe Regional Assembly

University Education: Wananchi wa Kaloleni wanasema kila jimbo liwe na University moja angalau. Hiyo iwe katika katiba.

Electoral system: hali ya uchaguzi. Kenya baado iyendelee na representative wa electoral commission ambayo kila mtu awe na haki, kura moja kwa kila mtu, na watu wachague waakilishi wao wenyewe. Party iliyo na majority wa watu wengi ndiyo party ambayo itaunda serikali lakini katiba itoe idhini ya kufanya serikali ya mseto. Waweze kuwa na uhuru wa kuenda katika vyama vingine, waweze kuchukua Mawaziri kutoka vyama vingine. Candidate ambaye ameshindwa kupata nomination katika chama chake basi kuwe na sheria katika chama chake itakayomwambia wewe chagua mwenyewe. Utaingia katika chama hiki ni wewe mwenyewe. Basi ukishindwa ndani ya uchaguzi huo huo asiruhusiwe kurukaruka; angojee mpka uchaguzi mwingine aruke katika huo uchaguzi mwingine, aingie katika chama kingine. Lakini sio le akatazwe na DP kesho aendi kwa KANU. Kesho kutwa huko akose nomination aende kwa Ford Asili, akose nomination kule katika uchaguzi huo mmoja hiyo si utovu wa kidemocrasia ama wakinidhamu. Hiyo ieleweke.

Present geographical constitutional boundaries zitazamwe. Kaloleni Constituency ni kubwa mno na ipewe angalao mbili, Mariakani na Kaloleni, ziwe angalau mbili. Tunataka tatu lakini minimum ziwe mbili. Hata nyinyi wenyewe mliamua muende Mariakani ama mje hapa Kaloleni (**clapping**). Kwa hivyo muliungana na sisi jambo hilo Macommissioners. Pia review ya constituencies zitazamwe upya kila baada ya miaka kumi kulingana na census results. Uchaguzi wa Rais ni by the people direct, wao wenyewe sio kwamba sio wachaguliwe na kamati, wananchi wachague. Na baada ya uchaguzi miezi tatu kila chama kieleze walitumia pesa ngapi sio kwamba wapewe kiwango lakini iwe public information- accountable waeleze walitumia millioni ngapi. Waeleze na heshabu ile itakuwa inachunguzwa na uma.

Uchaguzi wa mwaka 2002 uwe kivipi? Kwanza bunge lisiongezwe maisha yake. Uchaguzi huu uwe vile ulivyopangwa. Na wananchi wa Kaloleni wanauliza mfanye bidii mtoe Katiba mpya maanake wangependa kuona uchaguzi ndani ya katiba mpya. Na jiapo kunazungumzwa mngependa nyongeza ya wakati nyinyi Commissioners lakini wananchi wanasema ya kwamba hawapendelei nyongeza ile. Mmalize kazi yenu kabla ya wakati huu wa uchaguzi, na uchaguzi usije ukaongezwe mda. Ile haitakikani na wananchi.

Basic Rights. Katiba ihakikishe ya kwamba kila mwananchi amepewa haki zake, civil and political rights, rights to worship, freedom of association, rights za kuweza 'ku-associate' social, economic, cultural, zote zile na hata ethnic rights pia ziweze kuhesimika katika katiba hii na haswa Regional Assemblies zihakikishe ya kwamba haki za wananchi ambao wanaongaliwa kwa sababu wako karibu zaidi zihifadhiwe. Haki pia ziwe katika Katiba kuhakisha kila mwananchi ana haki ya kupata usalama, matibabu, maji, elimu, chakula na kuandikwa kwa kazi, kwa hivyo wahakikishe uchumi umezaa kazi za kutosha.

Elimu: Free primary education tena iwe compulsory mpaka kwa darasa la nane kwa kila Mkenya. Baada ya hapo ile elimu ya secondary na university kuwe na cost sharing baina ya wazazi na serikali. Upande wa university kuwe na bursary na loans.

Tumesema wa mama na disabled wawe na viti bungeni lakini tunataka kusema hata husbands and wives waheshimiwe ndani ya Katiba. Kwa mfano sheria iliyopitishwa juzi, inayojadiliwa bungeni sheria ile hawaitaki waume. Sheria kama ile ni mbovu inyoingia kwenye vitanda vya watu. Watu wa Kaloleni wamesema mambo ya bwana na bibi waachiwe ethnic ya kimila sio kwamba bwana akichapa bibi kofi au bibi achape bwana yule bwana au bibi akafungwe ah ah…. Mila ifuatilizwe kwa sababu mkigeuza zile mila, mkileta sheria ambazo haziambatani na mila tutakuwa na divorces mingi na mambo ambayo yatavuja haki na nchi vile inavyo endelea.

Land and Property Rights. Neno squatter hakuna tena Kenya hii kulingana na katiba hii, kwa hivyo katiba hii iuwe neno ' squatter'. Na ardhi iwe ni ya wananchi wale indigenous pale na Regional Assemblies zitazame mambo ya ardhi sio Commissioner wa land kule apeane certificate ya land na hajui ile ardhi iko mahala gani kumbe kule kuna watu wameishi hapo. Pia wamesema ya kwamba Kiingereza na Kiswahili ziwe lugha za biashara lakini tuongeze pia lugha ya mama siku hizi kulingana na global village ya ulimwengu, lugha kama ya kifaransa na kijerumani.

Natural Environment: Kila mtu amepewa rasilmali katika jimbo lake. Port of Mombasa ni ya Pwani - Coast Region. Port of Kisumu ni ya Nyanza. Parliament ihakikishe kwamba vitu hivi vimehifadhiwa. Appointment mumesema hizo zichunguzwe. At the Coast kuna mti huu unaitwa mnazi ambao una vitu mia moja na elfu mia moja na mia moja. Mti huu utazamwe kama mukahawa, mchai vile inatazama miti mingine. Yaani lasilimali za hapa ziweze kuheshimiwa. Na hasa tunaambia Commission mazao ya mti huo munazi sio mengine ya kubaliwe na mengine yawe subject to police harassment. Hiyo hawataki hawa ( **clapping**). Kwa hivyo mazao yote ya miti yetu hapa yatawalwe na Regional Assemblies na kama Regional Assemblies hazijaja, Administration Police waache kunyanyasa wananchi kabisa.

International Relations, NGOs, CBOs, Civil Society, Religious …. Hawa wote wanasaidia serikali kieconomic na mambo yale mengine. Lakini wasiwe kama vyama vya kisiasa, katiba ikatae hivyo. International relations, hiyo ni kazi ya serikali kubwa lakini waulize majimbo. Constitutional Commissions ziwe vetted na Parliament. Succession na transfer of power. Rais ni Rais; mpaka Rais mwingine achaguliwe na yule Chairman wa Electoral Commission ndiye atakayesema kama kumechaguliwa Rais mpya, halafu Chief Justice ndani ya wiki moja aweze kumapishaa yule Rais mpya.

Conclusion: Watu wa Kaloleni Constituency wamefurahia kazi ya Commission isipokuwa tu kazi moja, ile ya civic education ( **clapping**) Hatukupata sisi ile elimu ya uraia kwa hivyo tunalalamikia Commission lakini tunaelewa hamkuwa na pesa na pia sababu mumeambiwa mharakishe kazi yenu. Hata hapa mmekuja kutuburukisha. Mmekuja sio kwa mpango wa ki-sawa, (you have ambushed us) na kwa sababu vile mumetuambush maandishi mengine tume 'type' mengine yako kwa mkono mtupe msamaha kwa jambo hilo. Otherwise tunawashukuru kwa kazi yenu mzuri. Tunawaombea dua la Mwenyezi Mungu kazi yenu ibarikiwe na sisi watu wa Kaloleni tunasema Commission hii ibarikiwe na wakenya wote wabarikiwe na tunamalizia na kusema sisi ni serikali ya majimbo. Mungu awabariki. **(clapping) (and applause)**

**Com. Lethome:** Asante Mheshimiwa. Umezungumzia habari ya Parliament to vet all constitutional appointments, lakini kuna kifungu katika Katiba yetu ambayo inasema all Constitutional office-bearers do so at the pleasure of the President. Una nini ya kusema?

**Hon. Keah.** OK. Hivi sasa, Katiba ya sasa, zile Constitutional offices zote, Mawaziri Macommmissioners wote, wanachaguliwa na Rais pekee yake, na hizi ndizo nguvu za Rais tunataka tuziondoe agawanye na Parliament. Ufafanusi ni kwamba Rais awe hata Prime Minister akiwa ni uchaguzi wa mawaziri watateuwa wale watu (nominate) halafu Parliament wata-vet waone ya kwamba huyu ana kisomo kinachofaa, ana experience inayofaa waidhinishe, kisha yeye ataenda kuweka mkono. Kwa hivyo ni kazi ambayo Rais anaanza au Prime Minister anaanza, Parliament inachunguza kwa sababu Parliament ni Committee iliyochaguliwa na wananchi wote.

**Com. Lethome**: Swali, Mheshimiwa ni hivi (inaudible) at the pleasure of the president, that is what the current Constitution says .

**Hon. Keah**: Sasa hiyo ndiyo tunataka ibadilishwe at the pleasure of the citizens as represented by their members of the Parliament.

**Com. Lethome:** Parliament inasema Fedha za Kenya signature iwe ni ya Rais na ile picha ya Rais ibaki vile vile.

**Hon. Keah**: Ndio, kwa sababu inaunganisha nchi.

**Com. Lethome**: Kwa hivyo akija Rais mwingine tubadilishe ile picha.

**Hon. Keah**: Akija Rais mwingine apewe heshima yake.

**Com. Asiyo**: Hili jambo la domestic violence, unasema haija-faa kupitishwa pale lakini hujatupatia jibu la hii shida kwa vile kuna shida sana nyumbani kwa vile watu wameacha muongozo wa zamani za Mwafrica. Je pengine ungetuelezea vile tutakuwa na kamati au kiti kama ya Ombudsman ambayo mtu akiwa na shinda za kinyumbani au za kiclan anaweza kwenda pale akawalilia wakamsaidia au waje kwa mila?

**Hon. Keah:** Kwa vile mliniharakisha, Ombudsman iko katika memorundum hii lakini sisi tumesema Ombudsman aweko yaani Ombudsman ni mtu ambaye Polisi akikunyanyasa unaenda kwake sio kwenda kwa polisi mwingine. Kule nyumbani bibi amekuchapa kofi unaenda kwa Ombudsman, bwana amekuchapa kofi unaenda kwa Ombudsman na huyo Ombudsman atakuwako pengine atakuwa na kamati ndogo katika kila wilaya na hata inaweza kwenda mpka kijiji. Thank you.

**Com. Lethome**: Asante sana Mheshimiwa. Matangazo kwanza. Huyu mama aliyetoa maoni kwa niaba ya wa-mama wa kilifi hakuweka sahihi katika daftari yetu tafadhali aende aweke. Kisha tu na Bi. Beatrice Mwaka Mwaringa tafadhali uende uka-sign. Sasa nitamwita Councillor Priscilla Charo.

**Priscilla:** Kwa majina yangu sahihi ni Bi Priscilla Dhahabu Charo. Mabibi na mabwana, hamjambo? Mimi nataka katiba hii iwe na utangulizi ama dibaji ya umoja, amani na upendo, lakini majimbo. Na-ungana na wenzangu waliounga mkono majimbo. Rais akiwa mwanamume vice awe mwanamke. Rais akiwa mwanamke Vice awe mwanamume, ndiyo tunajenga.

Ardhi kuwe na kiwango kusiwe na masquatter mtu asiwe na hekari milioni tano. Ziwe na kiwango. Kama ni hekari mia mbili ama elfu mbili ziwe hivyo lakini si mtu awe na mtaa ama division moja ni ya mtu mmoja hali mwenye hapa yeye hana kabisa ( **clapping**). Mtu asiwe yuko ulaya na ana mijihekari yake hapa na asema mimi namiliki Kenya. Hiyo mimi naona si vizuri; kuweko kiwango kama ni hekari mia mbili ziwe hekari mia mbili kwa mkaaji wa Kenya. Asiwe kwao kusema ana chake hapa na mimi niitwe squatter na mimi ni wa hapa yeye yuko kwa na ardhi hapa hataki ikanyagwe kwao style yake. Madiwani waanze darasa la saba na kuendelea awe university - au nini, lakini awe darasa la nane huku chini na kuendelea.

Matibabu: Hasa maradhi ya cancer, ikiwa mimi ni cancer survivor na matibabu ya pelekwe kila district unakuta watu wana-kufa wengi kwa vile matibabu yako mbali na ni ghali ya legezwe. Wanawake ikiwa kuna nominated Councillors, nominated Wabunge 35% ipewe wa-mama. Mimi ningependa hata Madiwani baraza mzima iwe wanawake lakini hata wanaume tuliwazaa tushirikiane huko lakini iwe 35%. Ikiwa kuna nominated kule kwa bungeni wawe nusu kwa nusu, wanawake na wanaume. Ndipo pamoja tunajenga. Thank you. (**clapping**).

**Com. Asiyo**: Umesema maneno ya matibabu kwamba ni ghali mno lakini ungependekeza tufanye namna gani?

**Priscilla:** Mimi ningependekeza hivi. Haswaa maradhi ya cancer ni ya ghali sana iletwe kwa kila wiraya kama ni machine ya radiotherapy na chemotherapy hizo zote ziletwe huku. Watu wawe na ujuzi kwa maana tumeona watu wanavungwavungwa na hii ni cancer lakini yapitiwa na mbali ili ufe pole pole kwa maana unaonekana huwezi. Wale hawawezi waambiwe ukweli wao hapa kwa wilaya/district kuwe na machine hapa sio kusafiri kuenda mbali kupata matibabu.

**Com. Asiyo**: Lakini mama ufahamu kwa wakati huu hakuna radiotherapy au chemotherapy machine kwa hospitali zote Kenya zile za serikali isipokuwa za watu binafsi. Ungeweza kutoa pendekezo gani juu ya jambo hili lako la maana sana.

**Priscilla**: Radiotherapy iko Kenyatta lakini mara imeharibika, na-jua hivyo, lakini ingetiwa maanani, ni kwa maana hawaoni maana ya wamama kisha kufa. Serikali ihakikishe kila wilaya hii machine iko. (**clapping).**

**Com. Lethome:** Daniel Mzungu. Karibu.

**Mzungu:** Wananchi hamjambo. Mbele yenu ni Daniel Mzungu kutoka Ribe location. Mimi nataka majimbo. Kitu kingine ni haki ya kibinadamu idumishwe. Elimu kwanza, maana bila elimu duniani huwezi kuishi vizuri. Kiafya hivi kama mambo ya udaktari hiyo nayo ndiyo maisha yetu. Tatu, mambo ya kimila idumishwe haswa mambo ya kaye itiliwe maanani sana kwa sababu kuna mila zetu za kivamani hata sasa wengine wameziacha lakini sasa kwa vile inatajwa tajwa watu wameingilia kufanya na ni kitu muhimu sana kwa hivyo hiyo mambo ya makaya idumishwe.

Ingine ni kwamba ardhi ndiyo uhai wetu. Kila mmoja ni lazima azaliwe na nchi yake hata akiwa na mwenzio njiani anasema mimi natoka mahali Fulani. Kwa hivyo ni kitu muhimu ambacho ndiyo uhai wetu. Mtu akifa azikwe mahali pake lakini hii mambo ya wageni kuja kwa kuwa watu wako na pesa zao waje wanunue, na kwa vile ambavyo watu wanasema mwenye pesa ndiye mwenye nguvu, ikiwa huna pesa lako hakuna. Mwananchi ni lazima ahakikishiwe kwamba mahali anapoishi ndio pake.

Kitu ingine ni kwamba katiba hii ambayo inatengenezwa - nasema habari ya wafugaji wa ngombe. Katiba itengenezwe kwa wenye ng'ombe na shamba. Ningependekeza wapelekwe kortini kwa sababu hakuna mtu angependa upande mimiea yake halafu iharibiwe na ng'ombe. Sisi ambao tunalima geografia inasema watu wasilime karibu na mito, kukata miti karibu na mito, maji hukauka. Watakaokata miti karibu na mito kwa mashamba yao naomba wachukuliwe hatua na kushtakiwa.

Hali ya ugemaji wa tembo watu wa Pwani ndiyo sisi tunapanda minasi. Nataka utuliwe maanani kabisa kwa sababu sisi tumefundishwa ugemaji wa nazi. Sio kwamba mtu akishkwa na tembo asichukuliwe hatua kama aliuwa mtu. Ningependa watu wanaogema tembo wageme bure, wanaouza wauze bure, wapandaji wagema bure, kwa sababu ndio hali ya kudumisha sisi wengine ambao hatuna hata wengine hawana mashamba ili wapate kuelimishwa na shinda zao zote.

Hali ya kuonani, ma-arusi, vigelegele utamaduni. Bibi na Bwana wameoana wapelekwe mbele ya wazee watemewe mate ili utamaduni uwe utandumishwa sana zaidi ya ndoa maanake ile inahakikisha kwamba mzee wa kike na mzee mume atapatiwa mtoto wake usalama bila tatizo.

**Com. Lethome**: Asante sana Bw. Mzungu. Juma Thoya.

**Thoya:** Wananchi hamjambo. Kwa majina ni Juma Thoya. Mimi nitaanza na jambo la umasikini. Na sema Kenya kuna umasikini lakini tatizo tunaleta sisi ambao kuna miradi ingine ambayo sio muhimu (gradion project). Miradi yote itakayoanzishwa iwe inaweza kufaindisha wananchi wa kawaida katika sehemu za vijijini. Sio miradi ya kufaindisha mtu mmoja kwa mfano, miradi wa kununua ndege ya Rais hiyo ni pesa nyingi sana na huku watu wanaangamia, miradi kama wa kujenga airport na mtambo wa risasi, bunduki. Hiyo milandi yote ifutiliwe bali, miradi itakayoanzizwa iwe ya kusaidia mwananchi wa kawaida. Zingine na unga serikali ya majimbo mkono ambapo nasema 75% za utajiri wa jimbo zibaki jimbo hilo na 25% iende kwa serikali kuu.

Ingine naongea kuhusu uraia. Raia yeyote atakayependa kuisi Kenya na ni mgeni uraia wake apokonywe mara moja. Hii itasaidia kuangamiza mambo ya ugaidhi kama wewe mzungu au muhindi na unataka kuishi hapa, basi ule uraia wa nchi ingine upokonywe sio kuanza tatizo hapa halafu unaruka. Mahitaji ya ki-msingi kama elimu, matibabu, chakula na makao yaweze kupatikana kwa urahisi. Masikini na wasiojiweza wapate kupata vitu kwa urahisi. Vyama via kisiasa vijitegemee vyenyewe. Chama kile kiko mamlakani kisitumie fedha za uma zile za consolidated account. Asanteni.

**Com. Lethome**: Asante sana Bw. Juma. Kasema Changawe.

**Changawe**: Habari zenu. Kwanza na-wasukuru. Pendekezao langu la kwanza ni serikali ya majimbo kama ule mfano wa America, Uingereza na hata Ujerumani utatuletea manufaa sisi watu wa Pwani. Urais napendekeza ikiwa rais anapendwa na watu na ameenda miongo miwili, ikiwa watu watampenda na chama chake kuwe na uwezekano wa kuendelea hata kama ni term tatu au nne kama vile wanafanya Uingereza, unaweza kufanyika kama vile Margaret Thatcher alienda.

Kwa upande wa walemavu, watu wengi wameongea juu ya walemavu wapewe nafasi za kikazi na kimasomo lakini hayo yoteya-naongewa kwa mdomo. Hakuna mkazo unatiliwa kuhakikisha walemavu wote wameenda shule hata kama wazazi wao wamewaficha wasakwe. Unapata askari kutoka kwa Chief na Sub-Chief wako radhi kuzunguka kutafuta wale wanaswe lakini hawawezi katafuta ule mtoto mlemavu ambaye ana tatizo la kupelekwa shule.

Kuna hii hali ya mila kuna mila nyingine za Kenya ambazo watu wengi wanazipinga lakini hawaziangalii kwa urefu kama lile neno la urithi. Wanawake wengi na wanaume wengi wanasema urithi unaleta ukimwi. Tusiangalie habari ya mtu mmoja. Ikiwa mtu amefiwa na bwana akirithiwa anaweza kuambukiza yule anayemrithi na wanaweza kuishi hapo kama miaka tano wakiwa mke na mume. Kwa hiyo miaka mitano wakiwa waaminifu ule mmoja ndiye ataambukizwa. Lakini akikataa kurithiwa ama aachiliwe huru, ataenda kwa trading centre atakuwa ana ambukiza mtu mmoja kila siku. Hasara kwa taifa (laughter) afadhali arithiwe ambukize watu wawili kwa mia kumi. Maanake miaka tano atakufa lakini kuondoa hiyo mila sipendelei.

Halafu kuna maombi mengine tunaomba lakini inatakikana tutafute merit. Ikiwa tuta tafuta engineer tusimuajiri kwa sababu ni kabila fulani maanake tunarudi ile miaka ya '63 ambapo Kenyatta alikuwa anasema tupozese ukabila. Ikiwa Kilindini port ipo Mombasa na tunatafuta engineer, pajitokeze Mjaluo na Mgiriama, wengi watasema Mgiriama apewe kwa vile anatoka pwani lakini ikiwa we Mjaluo amemshinda huyu Mgiriama kwa pengine stage mbili si inatakikana tumweke yule Mjaluo maanake tunataka production.

Ikiwa tunatafuta mtu wa kuondoka mbio awakilishe Kenya unataka kuniambia tutashinda wa-Nandi kwa mbio ndefu? Sasa ikiwa ni Mnandi na ana kipawa fulani tukitumie bila kufikiria mahali anatoka. Hapo tutapata manufaa. Tusiseme tuchukue Mgiriama. Kuna Mgiriama unaweza kuwa unampenda lakini akawa hawezi kutoa mazao. Nchi nyingi zina ungana, East

Germany -West Germany, sisi tunafikiria kujigawa tena tuwe ukabila. Hapana. Majimbo, lakini kusiwe na neno ukabila. Maasai akiwa hapa awe anaweza kuitwa Mcoast kama vile Mrabai anaitwa Mcoast.

Lakini tatizo la mwisho na la muhimu, sisi wa pwani tumelaliwa juu ya tembo la mnazi. Na mara nyingi hizo sheria zinaletwa saa hizi tuko karibu na kura, tutaruhusiwa kunywa kwa sababu tunachezewa. Ikiwa serikali inasema ulevi unarudisha maendeleo nyuma kwani unataka kuniambia mlevi anayekunywa Tusker hakosi adabu? Kwanza anatumia pesa nyingi zaidi (clapping). Sasa unasikia mtu anahubiri sitaki ulevi kesho anaongea na Kiere-ini, Managing Director wa Kenya Breweries, kesho anaruhusu Castle Brewing, kama ulevi ni mbaya hata Kenya Breweries zifungiwe zote! (clapping).

Tembo la mnazi - najua hapa tuna madaktari poleni, ama twawashukuru vile muko - kuna ile tembo ilikuwa inatumiwa Nairobi ya kumi kumi. Ilikuwa na madhara ya afya mpaka ikaua watu lakini na wahakikishia tembo la mnazi haliwekwi hata sukari na binadamu. Liko naturally brewed na Mungu (clapping). Halina viongezo mbaya ama madhara yoyote. Napendekeza mnasi uruhusiwe usindane na Kenya Breweries (clapping) kuliko nitoke hapa niende Nyali Beach na-nunua ile chupa imewekwa round Jamaican Wine na ni mnazi wa Jamaica huwa hapa Rabai hautakikani. Mnazi uruhusiwe na kama utapigwa marufuku Kenya Breweries na Castle zipigwe marufuku pia (**clapping**).

**Com. Lethome**: Bw. Rashid Karissa

**Karissa**: Asante sana. Kwa majina naitwa Rashid Karissa. Mimi ningependeza serikali ya majimbo na kuna baathi ya mambo ambayo huwa si mazuri kwa serikali iliyopita ambayo tunayo kama machief na pia ningependekeza machief wa chaguliwe na raia kama wanavyochaguliwa Madiwani. Na pia sehemu kama za urithi pia ningependekeza kwa hawa ndugu zetu wanawake, wasibaguliwe kwa sababu ni wenzetu na waangaliwe pia upande wa urithi.

Nikisema wasibaguliwe ni kuwa mimi mwanaume nikipewa ka acre moja, dada yangu apewe ka acre moja (clapping). Na kuhusiana na mambo ya elimu ningependekeza Madiwani elimu yao isiwe chini ya darasa la nane kwa sababu wengi wana ujuzi wako na vipawa vya uongozi lakini ile elimu ya kuenda shule hana. Sasa hao nao wapewe hiyo nafasi. Wajaribu kushidana na wale wenywe elimu. Asanteni.

**Com. Lethome**: Samuel Victor Mbugo.

**Mbugo:** Kwa majina naitwa Samuel Vitor Mbugo, Chairman wa Kaloleni Constitutional Constituency Committee na mimi mwenyewe natoka Ribe. Maoni yangu ni kama yafuatavyo:- Serikali ya Kenya iwe na serikali kuu moja halafu kuwe na serikali za majimbo. Serikali kuu iwe itahusika na mambo yanayo ifanya Kenya ijulikane nje. Kwa mfano serikali hiyo kuu ya Kenya itakuwa ikihusika na security kama mambo ya majeshi, hewa, nchi na bahari iwe itajihusisha na mambo ya elimu kuu katika nchi, na mambo ya health ya wananchi. Katika security serikali kuu inatengeneza army. Huko kwenye army ni lazima

kuwe na quota system ambayo wale watu army ya Kenya iwe imendondoa ndondoa katika jimbo la Pwani, Magharibi, kila mahali. Na wale wa Pwani wawe ni wa pwani haswa si watu wamekuja pale waka kaa. Mtu wa Pwani anaonekana ni mtu wa Pwani. Kuna majina kama Kadenge na Karissa. Tukimchukua ndugu wetu ambaye anatoka huko na tuseme huyu ni mtu wa Pwani nafikiri tunajindanganya wenyewe. Kwa hivyo wale watu wa Pwani wawe ni wa Pwani halisi

Education: Ninataka elimu ya bure tokea Nursery school mpaka Std. 8. Hiyo ina maana kwamba hakutakuwa na mtu yetoye asiyejua kusoma na kuandika. Na hiyo elimu bure iwe ni bure halisi. Mtoto awe anazingatiwa vitabu, mshahara wa waalimu na kila kitu kule shule, pengine tu nguo za mtoto. Tena iwe ya lazima, yaani free and compulsory education.

Tatu, elimu ya juu, Serikali kuu ya Kenya iwe inazingatia kusaidia chuo kikuu ambacho ni cha government. Kila mkoa uwe na chuo kikuu ambacho kinaangaliwa na central government. Elimu hizo za bure za msingi tunataka serikali kuu iwe inachunguza quality education. Munaweza kuambiwa munapewa elimu ya bure lakini quality sio ya- kutosheleza. Kwa hivyo education iwe free, compulsory , na elimu ambayo ina quality. Pia free education kwa dispensary na hizi community centres Serikali kuu iwe na serikali moja katika kila jimbo ambayo ina zingatiwa na serikali kuu. Hiyo ndiyo ambayo, kama yule mama alisema, kuna mitambo ya kuangalia cancer na nini, sasa katika region itakuwa na serikali kubwa ambayo itakuwa imeweka hivyo vitu na hiyo pia waangalie quality ya mambo kama hayo. Hiyo region iko katika Province yaani, ni jimbo, na jimbo letu tunataka litoke hapa mpka sehemu ya Kibwezi na serikali ya jimbo iwe na mamlaka. Tuwe na mtu kama Regional Governor atakayekuwa na Bunge lake nawatakuwa na mamlaka ya ardhi na usalama, kutakuwa na mapolisi ya region. Wale wachukuliwe kutoka pale pale. Mtu mwingine amesema tuchuwe ya merit, ikiwa kuna mtu mwingine hatoki katika jimbo hili naye ni mzuri sana kwa upande wa Polisi na kazi nyingine ataandikwa hapo kwa mkoa lakini wale watu wanaotoka pale pale zaidi waandikwe upolisi.

Usalama: Mali ya asili ya lile jimbo ifaidi wale watu, na mimi nataka 'ku-endorse' kwamba kitu kama 75% ya mali ya asili ya jimbo ibaki pale na ile quota imebaki ipelekewe Serikali kuu iweze kusaidia yale mambo ambayo serikali kuu inafanya.

Uzalendo ni jambo litambalozingatiwa na serikali kuu. Napendekeza kuwe na school of excellency ambayo itawekwa na hiyo serikali kuu. Hiyo school of excellency iwe inatabua watu katika upande wa science, sanaa, sports wame 'ji-distinguish' katika mambo kama hayo. Tunataka hizo international stadiums ziwe katika kile region, kuwe na moja, ili michezo ikija isambazwe na sisi tujivunie tu Wakenya. Lakini ikiwa michezo yote ni Nairobi sasa sisi tutajua-je tu Wakenya?

Serikali iwe itazingatia professionalism. Mimi nimechukua degree ya Agriculture, Nimeingia siasa nimepitia sasa nitakuwa mtu ambaye anaangalia mambo siyaelewi. Kwa nini kama mtu ni daktari asipewe hiyo Ministry of Health ambayo ni relevant na hiyo kazi yake (**clapping**). Sasa huyo President atachagua watu na achague na akili ya kwamba huyu ni mtu wa elimu naye atakuwa na Ministry ya elimu, lakini asichukuwe mtu wa elimu apeleke agriculture na ni mgeni kama mimi. Kenya ina wasomi wengi, economist, educationists, scientists, medics, financiers etc. Kwa nini hatuwezi kupata watu kama hawa kukaa pamoja ku advise mtu kama Rais? Educationists, engineers wao watakuwa waki advise serikali kwa njia moja au nyingine. Lakini wao

wametoka wamekwenda nchi zingine kwa kuwa hapa hakuna kitu kama hicho. Mapendekezo yangu ni kwamba tuwe na 'think pot' ya watu kama hawa. Serikali iwe itatumia watu kama hawa kuwauliza watafanya nini. Universities ziwe zitafanya research kwa faida ya Kenya yote. Kwa hivyo pesa za Central Government ziwe zita shugulikia research ambayo itaweza kusaidi watu wa Kenya.

Retirees: Kuna wengine wame retire kwa umri mdogo, pengine wamechagua lakini wako still 'functionable'. Watu kama wao kuwatupa nje tu hivyo, serikali imekosea. Wale watu wanaweza kuchaguliwa na wa kasaidia in their relevant areas. Asante.

## Tape 3

**Mama:** I am the first active youth from Kalololeni. Madhumuni yangu ya kufika hapa mimi nataka serikali ya majimbo (clapping). Hata tumerudishwa nyuma kwa sababu ya tembo pekee yake. Ninao wengi niliowafunza na wengi waliokufa na niliwafudisha na hiyo tembo. Sasa nitaacha tembo vipi? Wale waliosema kuwa mgema asishikwe lakini muuza tembo ashikwe iko aje na yeye pesa zake kule zaendakununua tembo lake? Na yeye pia anataka kupeleka watoto wake shule na pesa ni hizo hizo. Kwa hivyo ningependa hii serikali ya majimbo iwasamehe iwaachilie (clapping). Hakuna mtu aliyeshikwa na (not clear) ni vigumu. Mimi husikiza vile ma DO, PC, Councillors vile wote wahama hapa Kalololeni na hii minazi yao ili tuweze kula na sisi, tufundishe watoto wetu. Hakuna shule ya bure. Mtu akienda shule akirudi asema ametumwa mia mbili na hilo ni tembo washikwa na polisi. Sina zaidi ya hapo (clapping)

**Com. Lethome:** Asante. Naona huyo ni mama ana heshimu mambo ya masomo, anaitilia mkazo. Je, angependa katiba mpya iwe na elimu ya bule?

**Mama**: Sitaki elimu iwe bure lakini iwe inalipwa na malipo ya ile tembo anayouza. Serikali yenyewe ichague vile itafanya.

**Com. Lethome**: Wewe mwenyewe wataka nini?

**Mama**: Kama hawana pesa wasome bure.

**Com. Lethome**: Haya asante mama. Hon. Morris Dzoro.

**Hon. Dzoro**: Asante sana. Jambo la kwanza ningetaka kuchukua nafasi hii kushukuru na kusema kwamba pomoja na yale maono tumetoa ambayo yameongozwa hap na mheshimiwa ambaye ndiye Mbunge wetu wa Kaloleni, Hon. Matheas Keah, mimi natoa nyongeza pamoja na yale ambayo sisi kama wakaazi wa Kaloleni tulitoa naye akatuakilisha aelemishwe kati ya ili civic education kuhuzu haki yake. Hivi ni kusema kwamba haki inaweza kuwa ipo katika vitabu ama katika Katiba lakini

mwananchi awe hajaweza kuelewa haki yake kwa hivyo civic education ile ambayo tumesema iyendelezwe mimi ningeongeza ya kwamba mwananchi wa kawaida aelemishwe. Tena rasilmali yake ilindwe iwezekanavyo. Kwa mfano ardhi mali la shambani, mambo kama uhuru wa kuongea bila uoga, haya mambo yote nafikiri mwananchi wa kawaida aweze kuelimishwa na kuonyeshwa kwamba ni haki yake.

Desturi na mila za Kimijikenda zipewe heshima tena Katiba iwe na uwezo wa kulinda mila zetu. Nikiongea hivyo ni kusema ya kwamba kwa mfano hili tembo la pombe ambalo tumekuwa tukizungumza ni kitu cha maana sana kwa Miji Kenda kwa sababu wakati wa Maharusi, Bwana na Bibi arusi wanapobarikiwa mpka hili pombe liwe pale. Wakati wa mtoto kuzaliwa anapoitwa jina lazima pombe pia liwe pale.

Wakati wa maafa ama msiba mara nyingi sana pombe huwa latumiwa. Kwa hivyo Katiba liwe wazi wazi na watu waelimishwe hasa wale wanaofanya kazi ya security yaani polisi ili kwamba ikiwa wanaweza kushika mtu mmoja akiwa na chupa moja kwa sababu ya mira za kidesturi ya Miji Kenda pia ya ma-jerican yanabebwa na lorri kwenda Mombasa yaweze kushikwa na waweze kushtakiwa bila wasi wasi wowote isiwe ni tu wale ambao wanafanya mambo kulingana na desturi za Kimijikenda.

Ningependa pia kupendekeza kwamba Katiba iweze kuruhusu kubuniwa kwa kamati itakayo angalia nidhamu na kesi za wafanyi kazi wa Kijeshi na Polisi. Wabunge maalum na Madiwani maalum wachaguliwe na kamati kulingana na ujuzi wao na elimu yao. Pia umezungumzwa tayari na imeonekana kwamba ni maoni ya wengi, mti wa mnazi uhaliliswe ili kila faida ya mnazi iende kwa mwenye mti huo. Kwa mfano makuti, kwita, pombe ambayo tumezungumza, mafuta vyote hivi vikaweze kufaidi yule mwenye mti huo. Ili kuwezesha kutia mutisha watoto wetu waliosoma kazi za utawala zipewe, ama kazi zozote zile zinatokea watoto waliosoma wapate kazi kama hizo angalau kufikia kidato cha nne wasiachwe. Ikiwa watachukua wale wa darasa la nane pia wale wamefika kidato cha nne waweze kuchukuliwa bila kizuizi ili tuwaweze kuwapa mutisha wale vijana wetu ambao wanasoma.

Ningependekeza kwamba kuwe na kamati ya kushughulika na kuhusu madiwani kupatiwa mishahara mizuri kwani hawa wako karibu sana na wananchi na mara nyingi ndio wanashughulikia mambo ya vijijini. Wakati mishahara ya Bunge inayoshughulikiwa na ile kamati tulioitaja pia ningeomba kuwe na kamati ambayo itaweza angalia mishahara hiyo ya Madiwani. Na pendekezo ni kuwa mishahara hiyo iwe inalipwa na serikali.

Pia ningependekeza kwamba mda wa Mbunge uwe vipindi viwili yaani miaka kumi. Ningependa kusizitisa habari za mashamba. Wenye mashamba wawe na vyeti vya kumiliki mashamba yao na wawekewe hali ya kulindwa kwani mara nyingi inaweza kuwa kwenye shamba kuna rasilmali either mawe, ama madini na kwa sababu hakujakuwa na pengine na civic education ya kwamba kuna haki mtu huyu akaja hadaiwa na shamba lake likanunuliwa kwa bei rahisi hali kuna rasilmali yule mnunusi atafaidika kwa miaka mingi Mimi pamoja na yale yalikuwa yamezungumzwa nimeonelea niongeze hayo machache na nina sema asanteni sana.

**Com. Lethome**: Lydia Baya

**Lydia**: Mimi kwa jina ninaitwa Lydia Baya kutoka Mwanamunga Location. Mimi nami naunga mkono mambo ya serikali ya majimbo kama wenzangu walivyosema. Mimi nikuzungumza kama mzazi na nina watoto wavulana kwa wasichana. Lakini nasikitika sana na kitu kimoja ambacho wasichana wetu sisi wazazi tunasomesha halafu wavulana wanawapatisha mimba na kuwatoroka. Ni jambo ambalo ninasitikika sana. Mtoto wako tumemfundisha mpaka form 4 amemaliza halafu anaharibiwa na mvulana wa darasa la nane. Vile akiona amempatisha ile mimba yuakimbia. Mvulana yeyote atakayepatikana na hatia hii kwa msichana wa form 4 amempatia mimba, au Std. 8 au msichana yeyote mvulana yule apatiwe yule mtoto amefundishe, amuelimishe, amulishe mpaka maisha yake. (**clapping**) Ni maoni yangu. Na kabla kufanya hivyo uule kijana ni naomba ashitakiwe na afanywe vyo vyote sahihi.

**Com. Lethome**: Pendekeza.

**Lydia**: Afungwe kabisa (laughter).

**Com. Lethome:** Unazungumzia juu ya mwanaume wowote.

**Lydia**: Mwanamume yeyote. Jambo lingine ni kuhusu afya. Maoni yangu ningependekeza kila location iwe na dispensary. Yangu ni hayo mawili. Mungu awabariki.

**Com Lethome**: Asante sana.

**Com. Asiyo**: Huyu kijana aliyepatia msichana mimba unasema afungwe. Mapato gani atapata ya kumsaidia mtoto huyu?

**Lydia**: Sasa hiyo nilikuwa amekataa mtoto wangu amekimbia. Sasa nitafanya nini? Afadhali atafutwe afungwe kabisa. Mimi sipate …………… (clapping)

**Lemo Tere**: Asante sana Macommissioners kwa kunipatia nafasi hii ili niwapatie memorandum kuhusu katiba kwa niaba ya wajimbana wote. Jina langu naitwa Lemo Victor Tele. Katiba tuliyonayo nasema iwe na utangulizi. Na utangulizi ule uwe based kwa jitihada ya wananchi. Gera waliyonayo katika utengenezaji wa serikali. Preamble hii ijihusishe bila kuchoka itafute kuhakikisha kuwa nchi hii inatawalwa kwa misingi ya kidemocrasia, uhuru, uendeleaji, nyaja za uchumi, usawa, haki za kibinadamu na social justice. Katiba kupitia vipengele vyake lazima ihakikishe kuwa kuna haki na uhuru kama vile ilivyo pangwa katika mikataba ya dunia kama vile Umoja wa Mataifa ulivyo panga juu ya declaration of human rights ikishikana na declaration of human rights kupitia kwa African charter.

Aina ya serikali. Nina shukuru sana wakati nikiwaambia wenzangu kuwe na serikali ya majimbo nilikuwa ni kipingwa. Kufikia sasa Macommissioners mumeona wazi wazi ni sawa ha ni haki nchi hii itawalwe na mtindo wa serikali za kimajimbo. Katika serikali tutakuwa nazo tunataka tuwe na Rais ambaye mamlaka yake itakwa madogo lakini achaguze waziri mkuu ambaye atakuwa kiongozi wa serikali.

Nikizungumzia juu ya Bunge ya Serikali ile ya Federal. Nataka bunge hilo liwe na uwezo wa kumpeleka kortini Rais akichezea serikali yetu (**clapping**) Bunge hilo tunataka liwe na uwezo wa kuunda wizara na kuzivunja ikiwa inahitajika kufanya hivyo. Bunge hilo tunataka liwe na uwezo kuwaita mawafisa wa Serikali wa ngazi za juu na kuwauliza maswali ikiwa wamedharau mamlaka yao.

Nataka serikali ya Federal Government iwe na uwezo wa kupitisha jinsi gani pesa za uma zitatumika na twataka bunge hilo liwe na uwezo wa kupanga vipindi vile wa bunge watazitumia kujadili misulada ya nchi hii sio Rais kusema - January tutakuwa na kikoa cha bunge halafu aende akalale kule Toiyo kisha arudi aseme tuta vunja bunge leo njooni jumapili. Twataka Parliament yenyewe ipange 'calender of events'. Tunataka bunge la Federal Republic liwe na uwezo wa kuunda tume ambazo zinaweza kuzungumzia maneno muhimu ya kitaifa kama vile Macommissioners mumechaguliwa mzunguke kutafuta maoni kuhusu mambo ya katiba.

The Judiciary: Majudge wote wa kila aina na ngazi zao tunataka wachaguliwe na bunge - commission ya bunge. Commission ile ndiyo itapanga jinsi gani majudge watalipwa ama kutunzwa katika kazi zao. Majudge hao lazima walindwe vilivyo katika afisi zao. They should enjoy security of tenure in their offices. Na kuwe na tume ingine ambayo iko huru - it's not interferred with by the Presidency, ili iweze kuteva, magistrates. Chief Kadhi achaguliwe kwanza kwa mpitio wa kura na waislam wenyewe halafu aidhinishwe na Commission inayohusika. Chief Justice wa Kenya lazima awe na qualifications zile ambazo zahitajika katika kuketia kiti kile ikiwemo, lazima kwanza, awe Judge wa High Court. Yeye lazima awe na Ph.D katika upande wa sheria na lazima awe zaidi ya miaka hamsini asiwe chini ya hivyo.

Powers of executive: Lazima zijulikane ni zipi (it must be defined).

**Com. Lenaola**: Naona wachukua kila point ………. (inaudible)

**Tere:** Natural resources na other issues. Katiba lazima itoe mamlaka kuwa rasilmali yote ya uma iwe mkononi za Serikali mwa majimbo. Na kila serikali yoyote ya majimbo lazima isimamie rasilmali ya uma vilivyo. Serikali za mkoa ziwe ndizo serikali za husika tu ambazo zinaweza kutengeneza sheria za mkoa ule sio central government.

Other issues - ningetaja hapa katiba iseme kile kiwango cha chini sana cha msichana kuolewa awe amefikisha miaka kumi na

nane. Na ikiwezekana kila ndoa mwandikishwe kwa uandikishaji wa ndoa. Na katika uma ikiwa demakrasia itapatikana lazima kuwe na free adult education kila mzazi aweze kuelemisha bila malipo.

Uandikishaji wa Majeshi - kila mkoa upewe quota yake ikiwa nafasi arobaine zimetokea zigawanywe mala nane. Na kila mkoa iwe na university moja ambayo itasimamiwa na central government. Mwisho kabisa ningependekeza kuwa katiba iruhusu kuwe na uhuru wa kuabudu hata ikiwa mtu atakwenda aabudu katika shina la mti kwa sababu makanisa hayatutoshi hivi sasa. They are more distant from God than the people who pray under the tree, the tree is natural and closer to God than the concrete wall. Thank you. (**clapping**)

**Com. Lenaola**: Free education mpaka kiwango gani?

**Tere**: Free education inawezekana mpaka Form 4. Kwa mfano if all the available minerals, precious minerals that are in Coast Province were extracted for the benefit of Coast people every child from nursery school up to Form 4 is capable of getting free education (**clapping**).

**Com. Asiyo**: Health?

**Tere**: Kila sublocation iwe na dispensary. Every division should have a main hospital for referral purpose. Professor umetosheka? (**clapping**)

**Com. Lenaola**: Asante Bw. Tere. Mzee Pekeshe.

**Pekeshe**: Mimi jina langu naitwa Baba Pekeshe Denje. Watoto wangu, ndugu zangu baba zangu wako hapa nimeletwa na jambo moja nililopenda leo. Nimesikia nilipokuwa nimeingia hapa nikaambiwa leo kuna marekebisho ya katiba. Jambo la kwanza nilipoanzisha na akina wazee Ngala sisi tulikuwa ni majimbo tayari. Lakini tukafanywa na makabila mengine maanake Kenya ina kabila arobaine na mbili kabila zote zikahamisha watu wenzake wote ikabakia ni moja tu. Kwa hivyo ikasahau kwamba pia ina na mikoa nane ikafanya mkoa mmoja. Niambieni jameni kabila arubaini na mbili na kila kabila ina mila yake mtu mmoja atiaendesha vipi?

Ikiwa Kenya hii haitapatiwa majimbo yake basi sijui mwataka vipi nyinyi wa-Kenya. Lakini mimi nasema lazima Kenya hii ikubali kumpa haki kila mwanajimbo apate jimbo lake (clapping) Kwa sababu hatuwezi kuenda kuchukuwa mkahawa kama agriculture inakuja hapa, tukaambiwa tukate minazi yetu tupande kahawa. Na hakuna mkahawa mmoja uliyoishi hapa unaiyoishi hapa ni mnazi. Na ikiwa baba yangu ameshindwa kunielimisha kwa sababu Mkenya asije akasoma kesho akaja akachukua nchi yake. Lakini sisi tukachukua watoto wetu tukawaelimisha. Mimi naweza kusema sasa kwangu bado sijapata ni DO na sikusoma. Kwa hivyo sasa, ningetaka ikoa hii minane ipatiwe uhuru wa majimbo sehemu yake. Ikiwa sasa vile tunaona

hapa viwili wili vya miti yetu huu mnazi ni mti ambao sisi umetulea kutoka mababu na mababu mpaka baba ni mkubwa, mnazi, tunategemea, tunauza hatushikwi leo mahamri mama anauza lazima akaambiwa kama huna licence utasitakiwa. Hilo jambo la mahamri na mnazi ambayo ni uchumi tumepata, hakuna haja ya license. Huu ni mti ambao unalea binadamu**. (clapping)**

Kitu cha pili, serikali ya majimbo ambayo tunaisema ishike usukani ukweli - mimi niwa na watoto kumi na wote ni kiwa ni nao hapa nitawaambia tule chakula pamoja? Sitakuwa hiyo ni kupata ugonjwa? Lakini kila mtoto uwekwe mahali kwake ndiyo Serikali ya majimbo tunataka ifanye namna hiyo. Hlafu serikali hiyo yetu isiwe kama iliyoko sasa kutoka machief wachaguliwe na wananchi wenyewe (**clapping**) Masub-chief sio wa karatasi nataka achaguliwe na mwananchi mwenyewe. Tena such-chief tu pekee yake abaki katika location nba sub-location yake. Lakini Chief azunguke vile waalimu wanazunguka. Ikiwa amemaliza miaka saba hapa aondoke Kaloleni aende Mariakani (**clapping**), kutoka Mariakani aende Rabai, kama kwao ameharibu aende akaharibu kwingine tena ili tumuone uongozi wake usiwe ni wa si pale pale. Hili ni jambo mimi naliambia Bunge lile linalokuja la majimbo. Ikiwa wewe ulikuwa ambaye unatekeleza ya kweli kwa nini usipatie wenzako fursa kama hiyo? Hilo mimi ndilo maoni ya majimbo yanoyokuja. Majimbo yale tunaetaka mwananchi aachiwe uhuru afanye kile anataka haswa kwa jambo la mnazi. Tembo la munasi ni tembo halali hata mimi mwenyewe nilikuwa nikigema. Kwa sabau linandondoka lenyewe na habari ya Mungu mwenyewe. Tembo tuachie wenyewe. (**clapping**)

Tukitaka kuondoa umasikini kabisa ni lazima turundi kwa kilimo na watu wa kilimo tuwaambie serikali ya majimbo itafute pesa iwapatie watu mikopo ya kulimia. Matinga wawe rahisi kwa sababu imepitia na serikali ya majimbo. Kuliko sasa hekari moja ni shilingi elfu moja na mia tano. Mimi nina familia ya watu ishirini na tano acre yangu ni moja tutaondoa aje umasikini? Lakini tinga likiwa rahizi likilima ulikima acre kama zamani, likilima acre moja shilingi arobaini je elfu moja atalima acre ngapi? ( **laughter**) Kwa hivyo ndipo na taka serikali hiyo tuondoe umasikini si kwamba tuwatafutie chakula bure lakini wa patiwe pesa za kuweza kuondoa umasikini na ukulima.

Pendekezo lingine ni kwamba serikali hiyo ya majimbo hayo yalikuwa yakifanywa na serikali hii siyataki. Tunataka Serikali ya majimbo. Fursa letu hiyo bahari ya Kilindini pesa hiyo zikiingia mikononi mwetu. Jambo la kupatia polisi pesa sisi hatulitaki.

**Salim Albert Ngala**: Mimi naitwa Salim Albert Ngala, kutoka Migirinana sub-location, Kaloleni Location. Napendekeza serikali ya majimbo. Katika Katiba hii, tume hii ya katiba kuna makabila arubaini na mbili, kuna majimbo manane tunakata kila jimbo lijitawale lenyewe kwa sababu kila kabila imepigania uhuru hapa mimi nikiwa mmoja wao. Kwa hivyo napendekeza katika tume hii ya Katiba iekwe kila jimbo lijitawale lenyewe na kwa sasa kuna majimbo mawili ambayo yasha-jitawala bado majimbo sita. Majimbo haya sita ikiwapo moja ni la Pwani hiyo Rais wa hapa anayepigania uraisi tumechagua kutoka jimbo la Pwani. Nikisema hivyo ni kwamba ni kutoka hili jimbo hili kutakuwa kumebaki majimbo matano. Jimbo lingine lishike vile vile utawala mpaka yamalizike, yakisha malizika itakuwa kila mtu ameonja asali. Hivyo ndivyo napendekeza.
Mengi ya-mezungumzwa na hayo yote anayefanya kazi akipata mshahara akifika nyumbani ndipo atapanga. Kwa hivyo hayo yote yaliyozungumzwa siwezi kuendelea nataka hayo hayo.

**Com. Lenaola**: Francis Kazungu:

**Kazungu:** Mimi kwa majina naitwa Francis Kazungu. Mengi yamezungumzwa hasa kuhusu Katiba hata mimi ninaunga mkono majimbo kabisa. Lakini kuna moja ambalo linanikera sana na nimeweka memorandum yangu pale na nitaeleza kwa ufupi. Hii ni kuhusu mahakama. Mahakama kuna mambo mengi ambayo ya-nafanyika ambayo sio sawa sawa. Hii si Majudge pekee yao. Tunafahamu wananchi nyote mnafahamu, mawakili, poleni, hao ni wanasheria hata kama wako hapa mutanisamehe kidogo. Mawakili wanaruhusiwa kuingia korti yoyote katika Kenya hapa na hii ni Katiba ya Kenya vile inawaruhusu, lakini kuna wakati mmoja kuna wakati fulani President mwenyewe alikuja akaona mambo haya hawafanyi sawa sawa. Akaja akafanya ile tunaita "Presidential Decree" kwamba wasihusike na kesi za mashamba.

Sasa mimi ninataka hivi, nataka hii sheria isongezwe kidogo mbele hao mawakili waondolewe kabisa katika kesi za maajali. Zile kesi ambazo gari huwa zinaumiza watu zimeuwa watu, mawakili sawa wanakuwa na matumbo makubwa kwa sababu ya hizi kesi. Kwa hivyo hii sheria, hii Katiba, isongeze mbele, iondoe kabis, ule uhusiano wao katika hizi kesi. Na mimi napendekeza hivi ikiwa inawezekana kesi hizi zisikizwe na Town Clerk. Town Clerk ni mtu ambaye ni lawyer pia au Judicial Commission of Kenya wachague special committee ya mwakili ambao wao watakuwa wakisikiza kesi kama hizo. Ili kwamba insurance wakiandika cheque kule iweze kumfuata yule mwananchi ambaye anakosa haki yake.

Poleni, hata juzi kuna mmoja kule Nairobi anatafutwa. Ana cheque ya elfu mia nane anakimbia nayo huku na huku alitangazwa juzi anatafutwa ashikwe. Kwa hivyo hii tunaita professional misconduct ambayo mawakili wanafanya na katika mahakama hawajaguzwa kabisa. Kwa hivyo mimi nataka waondolewe kabisa katika hali za hii. Hasa kabisa hiyo mambo ya ma-ajali.

**Com. Lenaola**: Asante sana. Bwana Mwalili Tumbo.

**Malili**: Mimi naonelea, naunga mkono katika hii mambo ya majimbo. Majimbo hii tukikubali na tumekumbali hii pendekezo langu ni kwamba tunataka majimbo ili uchumi wetu katika Kenya na katika Katiba hii ya mgao uchumi wetu umezoroteka. Uchumi ni mnazi katika sisi Pwani mnazi na hii pombe ya mnazi ambayo inasomesha watoto wetu katika Pwani. Pendekezo langu ni kwamba tembo la mnazi liwe huru. Lingine, kuhusu elimu ninaona ni bora sana katika Kenya hii kurudia hapo tena pendekezo kwamba hii katiba na tembo ya mnazi iendelee.

Ingine ni kwamba la mwisho, plot zetu hatuzipati namba hata moja, kwa hivyo pendekezo tunataka plot kila mmoja tukipata majimbo plot na sisi tutapata. Kwa hivyo sitaweza kuendela na mengi sana, hayo machache, mengi yamezungumzwa. Jina langu naitwa Mwalili Tumbo.

**Com. Lenaola**: McDonald Chiranzi na afuatwe na Japheth Kariga, yuko?

**Kirathi**: Jina langu naitwa Macdonald Chiranzi, natoka Jibana location. Asanteni sana Macommissioners kwa kunipatia nafasi hii nitoe maoni yangu. Kwanza napendekeza serikali ya majimbo. Na, ninapendekeza hivyo kwa kuwa nataka kuwe na nafasi wa kusimamia uchumi wa jimbo lile ambalo watu wale watakuwa kwa jimbo hilo lao. Kitu kinginge ambacho napendeleza ni kwamba katika dunia hii kitu cha kwanza kabisa ambacho ni first right of a human being haki ya binadamu katika hapa duniani ni hii ardhi. Kwa hivyo napendekeza hivi mzalendo anayetoka jimbo lile awe anaweza kuruhusiwa kama ni kuuza na kunua lakini mgeni, foreigner awe anaweza kupata haki hapo ya shamba kwa njia ya lease yaani tujue anaweza kukaa hapo kama ni miaka ishirini baadaye akimaliza ile contract kama vile walivyo-kubaliana na yule mwenye ardhi awe ana weza kutoka. Pesa zake zitakuwa zimeisha kulingana na mapatano. Hii, kwa sababu tunataka baadaye, hata vizazi vyetu vinje vione nchi yetu bado ni yao. Hilo ndilo pendekezo langu. Pendekezo lingine ni kwamba mwananchi wa Kenya hii kwa sababu kitambulisho kinamuita mtu kuwa mwana Kenya kuwe basi mtu anaweza kuandikwa kazi pahali popote, isipokuwa aweke sheria za pale jimbo alipo.

Kitu kingine, ukija wakati wa kuchagua kama ni wabunge, nini, kwa sababu mzaliwa na mzalendo ni watu wawili. Mzaliwa anaweza kuwa ni mtu tu amekuja kwa muda akisharudi pahali pake, lakini mzalendo ni mtu ambaye hana kwingine kwa kwenda kwa hivyo ukija wakati wa kuchagua wajumbe achaguliwe mzalendo ndiye aliye na asili ya kazi. Asanteni sana.

**Com. Lenaola**: Jina tena?

**Kirathi**: Naitwa Macdonald Chiranzi.

**Samson Chombo:** Nashukuru sana kwa siku ya leo kwa kuwa na mkutano huu wa maoni kama haya nawashukuru sana hasa…………..

**Com. Lenaola**: Sema jina.

**Chombo**: Mimi naitwa Samson Chombo. Mimi ni fundi wa kushona nguo. Na hasa mimi nazungumza katika upande wa kibiashara. Kwanza, kibiashara ni kama hivi, mtu anaweza kuwa, kwa mfano, mtu yuko na bibi yake na mvulana huyo huyo hana kazi yoyote. Sasa yule mvulana na babake hana, alifariki, mamake hana, alifariki, sasa huyo mvulana hana funzo yoyote, hakusoma, sasa yule mvulana akiondoka pengine yuko na mia tano anataka kuanza biashara kama kuuza tomato, viazi, ili kupata chakula yeye na bibi yake. Sasa hana zaidi ya hizo pesa mbali yeye alikuwa yuko na mia tano na wakati anaanza biashara katika meza hiyo ndogo wanakuja watu wanamwambia atoe leseni yeye anasema leseni sina, katika wakati huwo. Sasa ile toa leseni, yeye anahtakiwa na sasa atakikana aende kotini.

Mimi nilikuwa napendekeza hivi, kwa upande ya biashara upande wa leseni, wawe wapewe leseni katika makampuni

makumbwa ya kushona na katika ma wholesale wawe wanapewa leseni, lakini katika mafundi ya wale wanaoshona katika baraza mafundi wote upande wa vioseki, biashara za mboga hakuna leseni kabisa, leseni ziondolewe kabisa. Ni hayo tu.

**Com. Lenaola**: Jonathan Mbaya uko tayari?

**Antony K.** Kwa majina mimi naitwa Antony Kenga Mpe natoka Rabai. Mengi yamezungumuziwa na sababu kila mmoja anataka kutoa maoni nitazungumuzia kuhusu pendekezo moja la uchumi.

**Com. Leonala**: Asante sana.

Ninapendekeza, miti ile yote ya kutoka jani, miti kama miembe, mikanzu na minazi iweze, serikali yetu ambayo itakuwa ni ya majimbo, iweze kuhifaidh miti kama hiyo ili wananchi waweze kupata manufaa kutoka kwa hiyo miti. Na, ninapendekeza mti kama wa mnazi uhifadhiwe zaidi na nikitoa mfano unakuta nchi kama ya Sri Lanka, mti huu umeweza kusaidia sana nchi hiyo na kwa sababu umekuwa na factory nyingi kutokana na miti kama hiyo. Kwa mfano kuna factory ya bottiling. Cooperation: Unakuta ikiwa kama mti wa mnazi utafunguliwa factory ambayo itakuwa inahusiana na bottling na bottiling nayoi itakuja kwa kupitia tembo la mnazi likiwa litaruhusiwa kuwa bure na tuweze kupata kiwanda kama hicho cha factory ya bottling na watu kama wale wagema. Wagema waweza kuandikwa katika viwanda kama hivyo wawe wanaweza kufanya application kama vile waalimu wanafanya application na kuandikwa katika viwanda au kamati kama hizo.

Na kitu kingine ni upande wa oil corporation na fibre corporation. Mwananchi aweze kupata faida nyingi kutokana na huo mti wa mnazi.

Na jambo lingine ni kuhusu upande wa ardhi. Unakuta mwananchi amekuwa akionyanyaswa sana na hii serikali yetu ya umoja. Ninapendekeza ardhi, mwananchi akiwa amepata kibali cha kumiliki shamba lake na labda katika hilo shamba kuna madini asilimia sabini na tano iwe inaweza kumsaidia mwananchi. Na asilimia ishirini na tano ziwe zitaweza kwenda katika Central Government.

Na jambo la mwisho, ni kama lile limezungumziwa kuhusu upande wa uchaguzi wa machifu. Mimi natilia mkazo kuwa machifu wawe wataweza kuchaguliwa na wananchi na kwa hayo machache Mungu awabariki.

**Com. Asiyo**: Ulipoanza kuongea ulisema juu ya miti. Halafu baadaye ukasema kwa ile Serikali ambayo unajua ya kimajimbo. Lakini pengine usichukuwe tu kwamba ukiongea juu ya miti tutachukuwa kwa roho yako kwamba unaongelea mambo ya serikali ya majimbo kwa hivyo useme kabisa vile unavyotaka serikali ikujayo iwe.

**Antony Kengo**: Haya. Asante sana. Mimi ninatilia mkazo serikali ya majimbo. Tuwe na serikali ya majimbo. Na serikali

hiyo ya majimbo kiongozi uule ambaye atachaguliwa kama Rais aweze kutambua Serikali ya majimbo imekuwapo kutoka zamani lakini viongozi ambayo walikuwa wako hapo hawaku-ha-mini majimbo. Na ndio unakuta mpaka leo watu kama wa pwani tumekuwa tunanyanyaswa sana. Kwa hiyo mimi ninasisitiza serikali ya majimbo. Asanteni.

**Jonathan Mbaya**: Kwa majina naitwa Jonathan Baya. Mapendekezo yangu kwa leo kuhusu msimamo wa serikali mimi ningependelea serikali ya majimbo. Na majimbo haya tuwe na Rais mmoja. Rais yule asiwe ni rais mwenye uwezo mwingi ni lazima ule uwezo upunguzwe. Na ule uwezo ukipunguzwa chini yake tuwe tuna Prime Minister. Prime Minister yule ataweza ku - form government. Yeye ndiye atakayekuwa na uwezo wa ku-form ile government. Tukirudi kwa Rais tutaweza kumpa ile mamlaka ya Commander-in-Chief. Na katika Prime Minister ataweza ku-form government, ataweza ku-appoint ministers na shughuli zote za bunge atakuwa anashughulika nayo.

Tukipitia upande wa uchumi kwa vile itakuwa ni Serikali ya majimbo, uchumi wote utakaopatikana kwa jimbo, 90% ubaki kwa region 10% iwe itakwenda kwa serikali kuu. Na kuhusu umri wa Wabunge, mtu yeyote yule ambaye ana zaidi ya miaka ishirini na tano yaani kuanzia miaka ishirini na tano anaweza kusimama ubunge. Na mtu yule yule asipungue kiwango cha Form 4. Si uchukue Std. 8 usema huyu anatosha, haitoshi. Na pia vile vile ukichuka yule wa Std. 8 kule tunataka mtu atakaye ongea kizungu. Sio Kiswahili, Kizungu ndio wageni wale wanakuja kutoka ng'ambo watazungumza na yeye kitu gani? Hata kama wewe mwananchi lakini mwananchi gani yeye anajua Kiswahili Kizungu huwezi kujua?

Na katika President tunataka mtu wa kutoka miaka arubaini. At least awe university level. Na Councillors at least kutoka miaka ishirini na moja. Na huyu councillor awe kutoka Form 4 sio Std. 8. Kwa machifu pia usichukuwe mtu ambaye yuko illiterate ama hana kipazi cha kusoma. Education iko tofauti na kipazi kwa hivyo ni lazima tuhakikishe kuwa hata kama ni chief awe ni Form 4 level. Kwa nini uwe wewe utakuwa being led na kipofu na wewe umesoma zaidi ya yeye? Yeye ni kipofu lakini atakuongoza itowezekana aje? Hiyo ni vigumu. Katika security kama ilivyozungumzwa kwanza lazima tuwe na quota system. Hatuoni sababu niende kwa OCS hatuelewani lugha hajui shida za hapa lakini yule ambaye atakuwa ni mwenyeji ndiye anajua shinda za hapa. Maanake ukienda kwa yule anayetoka bara anakutolea ukali kama wewe ni mtoto na anajifanya hajui lakini kama ni mtu mwenyenji wa hapa anaweza kuelewa.

Education: Free education from std.1 to 8. Na wakati wa serikali ya majimbo madini yetu yakiwa yamekuwa exploited vizuri nafikiri hata university level jimbo letu linaweza ku-cater for the whole Kenya. Sio Pwani pekee yake kama hii ambayo iko hapa Kwale, Malindi ikiwa exploited sawa sawa serikali itaweza kupeleka mtu kwa free education in university level.

Health: Nafikiri kwa health ni lazima health iwe ina vutwa kwa mwananchi vijijini. Kwa mfano Mwanamwenga hakuna dispensary. Ile distance ya kutoka kule kuja hospitali hapa ikiwa ni emergency sidhani yule mtu anaweza pona. Kwa hivyo ikiwa tutakuwa na health system ambayo iko kwa village zetu nafikiri itasaidia sana. Kwa hivyo ni lazima tuwe na health centres katika village level. Ikiwa ni hospitali ya mkoa ama hospitali ya district level ama divisional kama vile Kaloleni lazima

tuhakikishe tuna madawa, sio ni hospital tu jina, ukienda unaambiwa daktari hayuko. Ama unatimbiwa unaambiwa madawa hakuna mpaka ukanunue dukani. Kwa hivyo nikimaliza ningependa health iangaliwe zaidi maanake health inakuja number one mambo mengine baadaye.

**Com. Asiyo**: Na iangaliwe vipi? Kwa kupeana free health services au …?

**Mbaya:** Tunataka free health services . La mwisho: problem ya squatter. Kwa nini tuwe squatter katika jimbo letu? Mtu anakuwa na 25,000 acres mwingine anakuwa na 100,000 acres na si mwenyenji. Ikiwa itakuwa system ya majimbo ambayo tunaitaka tuhakikishe, hata yule mwananchi wa kawaida akikosa ardhi awe na at least acre moja. Iwe ni policy yeyote yule mwananchi awe na acre mjoja. Hatutaki kuyanyaswa maanake huwezi kuwa wewe umezaliwa hapa ama katika Kenya hii halafu una-ambiwa wewe ni squatter. Ulitoka wapi? Unaweza kuwa squatter kwa nchi yako? Inakuwa ni vingumu. Asante

**Com. Lenaola**: Douglas Mkanji. Joseph Maitha uko tayari? Daniel Mwachinga uko tayari?

**Mkanji**: Kwa jina naitwa Douglas Mkanji. Mimi natoka Jibana location. Nilikuwa na maoni mawili tu ama matatu hivi ambayo nataka ni peane kwa Commission. Kwanza ni naunga mkono kabisa serikali ya majimbo. Maanake nafikiri system ya majimbo ilikuwa imeandikwa mbeleni na tuliona vile pengine ingefanya lakini ikaja ikaharibiwa mpaka ikawa hii tulionayo. Kwa hivyo kama itarudi vizuri kabisa itakuwa serikali nzuri hapa Kenya.

Pili, ni starehe na uchumi. Kila Mkenya anatakiwa kustarehe na kila Mkenya anatakiwa kutajirika lakini kumekuwa na system kwanza sasa tuko na uhuru miaka therathini na tisa kila mmoja anazidi kwa maskini. Kuwa masikini ni kwamba mtu anajifikiria hana kazi ya kufanya, lakini aone afadhali nitafute unga angalau nitengeneze mahamri nikae pale nje ni uze nitapata posho. Lakini, baada ya dakika kidogo haitakuwa atafuatwa na either watu wa municipality au polisi apewe license. License ile ni kama 1,200/= ambayo utoa wa mahamri hauwezi kununua license. Pendekezo langu ni kwamba hii license iondolewe kwanzia mtu wa biashara ya kwanzia 1,000 mpka 50,000, iondolewe kabisa. Mtu mwenye biashara ya 50,000 kuendelea mbele alipe license.

Kitu kingine ni kama uhuru wa kuabudu. Ningetaka serikali iangalie sana hizi dini ambazo haziabudu hata national anthem, haziabudu kama kuna President zina mambo mengi mengi ukiwa mgonjwa huwekwi damu ufe. Dini kama zile sioni kama kwamba ni ndini za maana sana kupewa authority kuweza kusambazwa maanake hazina hata heshima. Kwa hivyo ndini kama zile serikali ichunguze sana zifungwe ama zifunikwe zisiendelee. Asante.

**Com. Lenaola**: Stephen Ngela George?

**Daniel Mwachinga**: Jina langu mimi ni Daniel Mwachinga, Councillor wa Libe location. Yangu yale nataka kuzungumza ni

yale yamezungumzwa nitakaongeza zile sehemu ambazo hazikuguzwa. Naunga mkono serikali ya majimbo. Na amini kwamba uhuru tulipopata serikali ya majimbo kama ingekuwa introduced tungekuwa tuko mbali. Serikali ya majimbo hii tunaitaka isimamie elimu kutoka primary education to secondary education iwe chini ya majimbo.

Polisi iwe mikononi mwa majimbo isiwe katika central government. Uraia wa jimbo kwa mfano jimbo Rift Valley raia ni yupi? Raia wa jimbo ni yule amekata shauri kuishi katika jimbo lile, kwa mfano hapa Pwani, hata kama wako bara lakini amekata shauri kuwa anaishi hapa, anafanya biashara hapa, yule anachukuliwa kama ni mwenyeji wa jimbo la pwani na apewe haki zote kuondoa ukabila. Tukija hapa katika elimu ya councillors tumesikia wengine wakisema councillor awe Form 4 na MP awe Form 4 kwa nini? Education si proof ya leadership. Napendekeza kuwa elimu ya Councillor at least awe Std 7 or 8. Na hawa present sitting Councillors hata kama ni Std 4 yeye aruhusiwe uchaguzi huu asimame, aendelee kusimama, kwa sababu si yeye alishinda wale ma form 4 na Std. 7? Kwa nini leo aondolewe aambiwe asisimame, itakuwa unfair. Tunajua kuwa katika Parliament kuna MP kule hata Form 4 hawajafika basi kuwa hao waondolewe hata wale waondelewe wale qualifications zao ni less than Form 4 watolewe. Pendekezo langu nasema sitting Councillors hata kama ni Std 4 waruhusiwe kuminyana na wale wenye elimu. Asante.

**Stephen Ngela George**: Kwa majina maitwa Stephen Ngela George. Na mapendezo mawili tatu hivi ya kupendekeza. La kwanza ni kuhusu mimea yetu. Nikisema mimea kuna baathi ya mimea ingine ambayo kwa dakika hii sisi wenyewe tunaaza kusahau kama mkorosho. Tungependa serikali ya majimbo kama itafuaulu iweze kututafutia market ama soko la mazao hayo. Jambo lingine, ni kuhuzu mnazi. Mnazi tungependa kwamba pia uweze kutafutiwa soko ama utafiti tuweze kujua kama inaweza ikatoa dawa, sukari ama nini ili kusudi wenyeji wakaweze kufurahia mazao yao. Lingine ni kuhuzu barabara. Ningependekeza kwamba barabara yetu iweze kuangaliwa vizuri sio wakati wa mvua tu barabara iweze kuangaliwa. Lakini wakati wa mvua na wakati wa jua ili barabara ziweze kupitika na usafiri upatikane kwa uangalifu mzuri. Ni hayo tu.

**Com. Lethome**: Asante sana

**Konde Dzui:** Kwa majina naitwa Konde Dzui. Natoka Maweza Location. Maoni ya watu wa Maweza walikuwa wanaomba hivi kuwe na serikali ya majimbo. Wanaonelea jimbo la Pwani limekosa kuhudumiwa vizuri makusudi watakuwa wa jihudumia wenywe na hii serikali ya jimbo iwe na uwezo wa kujipangia mambo yake. Pato ambalo latoka jimbo hilo itumie yenyewe juu serikali imekuwa kama mbili central na hiyo ya local government 10% iende kwa central government, 90% itumike kwa jimbo hilo. Pili, wanasema kwamba Wabunge wasichaguliwe zaidi ya vipindi viwili hata kama mtu anauzuri wa aina gani baada ya kipindi cha pili asiendelee tena.

Tatu, mahakama nayo iwe na uhuru wa kufanya kazi zake, isiingiliwe na afisi yoyote ama upande wowote. Upande wa utawala kuingilia mahakama hiyo imefanya kesi nyingi kukosa kufanyiwa wakati unaofaa.

Nne usambazaji wa elimu. Elimu isambazwe kisawa sawa. Kila jimbo liwe na university hata kama ni moja, na colleges. Hiyo itafanya elimu iwe kila mahali kuna wasomi wakutosha pengine kama waandishi wanaweza wakapatikana na kuangalia matatizo gani yako katika jimbo lile.

Tano, wanasema wenye viti wa mabaraza na ma mayor wachaguliwe ni watu wenywe directly kuwe na public election ya hao watu wenye viti na Madiwani.

Sita, Wabunge wapunguziwe zile sehemu zao wanaakilisha. Maana tunaona pengine Mbunge sehemu zingine hafiki na kuna kuwa na matatizo chungu nzima katika humo ndani ndani, lakini yeye hafiki kwa kuwa hiyo sehemu ni kubwa sana. Kwa hivyo zipunguzwe ndio ziweze kuwakilishwa sawa sawa. Madiwani nao wardi zao zichanganywe zikawa mbili mbili. Maana sasa itamfanya diwani awe na kazi ngumu kwa mfano wakati huu tunasikia Maweza na Luluma zimechanganywa hiyo ni kama division mzima. Diwani yule kufanya maendeleo inaweza kuwa kazi ngumu sana.

Saba, kuwe na sheria kali ya kufanya polisi wasitake hongo au kusumbua raia pasipo na sababu za kueleweka. Na sheria hiyo ichukuliwe polisi akifanya makosa hayo hatua kali mara moja.

Nane, Rais awe kati wa umri miaka hamsini na sabini na awe amekomaa ki akili na awe anaendesha maendeleo kwa taifa.

Tisa, kesi za mashamba ama mipaka iachiwe wazee wa kijiji; wala sio mawakili kwa sababu wakiri atakuwa hakuna kitu anaelewa pale atakuja pale kwa sababu ya tamaa zake, anaanza kuregesha mpaka pale ama kurudisha huku. Kwa hivo ikawa kuteuliwe kamati ambayo itatikana na kijiji kile ili wawe wanaelewa ni akina nani walikuwa pale na mpaka ulikuwa ukipita vipi.

Kuwe na sheria kali kwa mtu wakutumia vibaya mali ya uma.

Kumi, kura zihesabiwe vituoni ili kupunguza gharama au wizi, na saa zingine watu wanasema kura zimeimbiwa zikiwa safarini kwa hivyo zihesabiwe mahali hapo zitakuwa zimepigiwa (**clapping**) Asanteni.

**David Fondo**: Jina langu naitwa David Fondo. Nazungumzia kuhusu elimu. Elimu waalimu watunzwe sana kuliko mtu yeyote kwa mishahara. Pili, madaktari vile vile waangaliwe sana pamoja na wauguzi kwa sababu hawa waalimu ndio chanzo chetu sisi na nyinyi. Madaktari baada ya Mwenyezi Mungu kuleta hapa wao nao hufuatia vidokezo maksudi tukaendelea kuwa hai bila wao mambo ingekuwa misonga mingi kwa hivyo wakaangaliwe si wajumbe wakajiongeza mishahara huko watu wa maana wakaachwe hapa. Mbunge ajiongeza mshahara sehemu ambazo zinataka kufikiwa, barabara mbovu - yeye hafiki kule.

Upande wa mashamba: Ningependa mzalendo yule wa chini kabisa kama hana shamba awe na acre nne. Na yule ambaye ana kubwa sana acre kumi na mbili kwa sababu watu wamevamia mashamba yote hata sehemu za barabara kwa sababu wana

pesa. Sasa mashamba hayapatikani. Sasa mtu moja ana karibu acre elfu kumi na wao wengine si wananchi? Wakiwa si wananchi basi wawaondoe wabaki wao wenywe lakini wakitaka usalama yale mashamba walio nayo waitumie kwa kazi ili mzalendo apate kazi na kama hawezi agawiye raia mara moja. Hayo ndiyo nilikuwa nayo.

**Ali Juma:** Asante sana Commissioners na kamati ya waakilishi wa Constituency na pamoja na Coordinator wa Kilifi District. Mimi ninakubaliana na memorandum ile iliyopeanwa na Kaloleni Constituency. Yangu ni kuongezea tu mawili au matatu. Nakubali ya kwamba katiba ifanyiwe marekebisho. na hiyo 'exercise', kama haitamalizika kwa ule muda ambao unahitajika, kuwe na 'mini-reforms' na mini reform zile zisiweze kumpatatia mamlaka Rais kuendelea na kipindi kidogo au chochote ambacho kinatarajiwa kwa kuongezwa.

Pili, Bunge lisiongezwe muda kama hamtakuwa mumemaliza kazi yenu. Ingine kiini kikubwa sana ni kwamba should the parliament's power to amend the constitution be limited? Mimi nakataa hicho kifungo kwamba wakati wa 1963, wakati legislative council imeenda kuleta Katiba hapa Kenya, Katiba iliyoweza kuchorwa katika Serikali ya kwanza ilikuwa Federal System. Na leo sisi tuna shangaa ya kwamba nyinyi Macommissioners munazunguka ati kwamba turekebishe katiba. Watu ambao wamepoteza katiba hiyo in Wabunge kwa hivyo ile minimum 65% ya Wabunge kubadilisha katiba ndiyo inazidi kuleta matitizo.

Leo tutatoa maoni lakini kule wakienda Wabunge nyinyi hata maoni mnayoyatoa saa hii either mtaipeleka Kasarani wale wamechaguliwa waende kule kujadili, na baadaye muna handover ile kazi kwa wale Wabunge. Kwa hivyo wale Wabunge wakipewa 65% minimum ya kura ya kubadilisha katiba, kuna-kuwa na hasara hii ya kwamba katiba ile ya Federal iliingia wakati ule wa serikali ya kwanza, wana jukumu tena ya kurekebisha kwa hivyo badala ya 65% kupitishwa ya kwamba wabunge wabadilishwe, hiyo kazi ipewe wananchi waulizwe maoni kama hivi wanaulizwa, itakuwa ni vigumu sana ile katiba ambayo imeadikwa kubadilishwa. Sina mengi sana bali naunga mkono ile memorandum iliyopewawa na constituency.

**Com. Lethome**: Asante sana Bwana Ali Juma. Sasa twa muita Rev. Samuel Ngala.

**Rev. Ngala**: Kwa jina naitwa Rev. Samuel Ngala. Ni mmoja kati ya wale wana Committee members wa mambo ya Katiba. Kwa kuwa mengi yamekwisha kuzungumzwa, nitasema machache sana. Ya kwamba, maoni yangu mimi nami naunga mkono kwamba nchi yetu ya Kenya iwe na Serikali ya majimbo. Nataka kuleta kitu tofauti kidogo. Kitu chenyewe ni kwamba, hapa tunataka kugeuza Katiba. Lakini nataka niseme, Katiba ambayo haijapata msomi wa kuiandika na ndiyo ya asili ambayo tunaifuata. Na katiba hii, ambayo tunaifuata ni Katiba ya mume na mke na wanawe ndani ya nyumba. Wanaishi kwa sheria zao. Hakuna mtu aliyewaandikia sheria ya jinsi ya kuishi watu hao. Na wanao wanaishi sawa sawa.

Serikali yetu ya Kenya vile inavyotutawala, inatutawala kama mtu aliye mbali, lakini, mimi naazimia ya kwamba serikali yetu ya majimbo ianze chini ipate kwenda juu. Sio ya kutoka juu kuja chini. Kwa sababu ikianza chini itaanza na mume, mke na

watoto kwa sababu hao ndio wanajuana, wanafahamiana katika shida zao. Ikiwa ni elimu, ikiwa in afya au ikiwa ni umaskini walio nao. Kutoka hapo waende katika Kijiji. Wakienda katika kijiji, maoni ni kwamba katika kijiji ni watu wachache ambao wako chini ya sub-chief. Na hapo wana-juana shida zao. Wakijuana shida zao hapo basi wanaweza kutengeneza shinda zao maana ni wachache, na watajua ni nyumba ipi ambayo watu wanashida hii na hii wataweza kurekebishana hapo. Wakitoka kijiji ambacho ni sub-location wanakwenda kwa location. Kwa hivyo ni kutoka chini kwenda juu. Wa-location watakuwa chini ya Chief ambaye chief huyo ataweza kujua kwa upana zaidi vile ambavyo watu wake wanahitaji.

Ikiwa ni afya wanaweza kuja pamoja ili waweze kupata dispensary. Ikiwa ni elimu wataweza kufanya mashauri jinsi watakavyo-elimisha watu na ikiwa ni umasikini ni hapo wanajuana wote, wanaweza kutafuta njia za kuondoa umasikini. Wakitoka kwenye location ikiwa wamekwisha kujua mambo hayo yote wanaweza kwenda mpaka wafike kwa D.O. yaani (District Officer). Kwa kuanzia chini kwenda juu ndio yale matakwa, mahitaji ya maisha ya mwanadamu katika jimbo itaweza kujulikana kutoka ndani ya nyumba mpaka kufikiliana na yule ambaye atakuwa ni Governor wa jimbo nzima kwa kuwa wamejuana kutoka chini.

Nikitaka kuingia upande wa urafi kwa sababu huko juu kuna mengi ambayo yamekwisha kusemwa. Kuhusu mambo ya urafi. Urafi ambao unatisha watu hasa akina mama ni mke kuchukuliwa na mume mdogo au mume mkubwa wa yule aliyekufa. Kwa ajili ya kuogopa hivyo mimi ninaazimia ya kwamba kwa sababu ya mila yetu na tunaona ya kwamba mila haifai kuachwa na hiyo tukiona kwamba pengine ingeweza kufaa basi kabla ya watu hawa kuchukuana ufa kwa kuondoa ule woga wakapimwe kwanza kwa daktari. Wakipimwa na daktari wataweza kuonekana mke ana ukimwi, au mume ana ukimwi, hapo wataweza kupata advice ya kwamba hamuwezi. Ijapo mila inawalazimu hivyo hamuwezi kwa sababu yule ni mgonjwa na huyu ni hivi. Kwa hivyo itakuwa hakuna tisho tena la kuogopa kwamba mmoja atamtia mwingine ukimwi. Maoni yangu.

Katika urithi pale pale watoto wote waliozaliwa na baba na mama wa kike na wakiume wanayo haki ya kupewa urithi wa nyumba. Lakini (na hiyo katiba iandike neno hilo "lakini") - ikiwa msichana ameolewa na huko aliko olewa amepata bwana na ana mali ya kutosha na raha mstarehe na watoto wake, huyu aliyeolewa kutoka nyumba hii asipate urithi kwa sababu atakuwa anachukuwa sehemu ya wale ndugu zake aliowaacha pale na hali yeye tayari ana mali kule. Ni maoni yangu.

Wakimbizi: Hao wakimbizi ambao wanatoka nchi nyingine kuja katika nchi yetu ya Kenya ijapo watakimbia waingie katika jimbo. Lakini wakimbizi wajulikana katika serikali kuu, ili iwe ni gharama ya serikali kuu badala ya majimbo kuweza kuwekaribisha na kuweza kuwashughulikia wakimbizi wanaotako nchi zingine. Wakimbizi wagharamiwe na serikali kuu. Wakimbizi hawa watakapofika kabisa wasipewe vyeti vya kuwa raia wa nchi yetu ya Kenya. Kwa sababu hao wakati mwingine ndio wanaotuharibia nchi yetu. Na-azimia kwamba hawa wasipewe kabisa kabisa uananchi - kuwa citizen - wa hapa Kenya. Uwananchi wawe watakuwa hivyo siku zao zikimalizika warudishwe kwao.

Jeshi. Jeshi imebidi liwe moja ili tuweze kupata mamlaka ya kulinda nchi yetu kutoka mchali pamoja. Isipokuwa na kubali ya

kwamba polisi wa majimbo wawe wanatoka katika jimbo hilo hilo ili waweze kuelewa shida za jimbo hilo na hata lugha na mahitaji ya watu vile walivyo. Ninataka nikome hapo. Ikiwa kuna maswali niko tayari kujibu.

**Com. Lenaola**: Asante sana.

**Com. Lethome**: Antony Njao? Job Mwarumba?

**Mworuba:** Majina yangu naitwa John Mwarumba. Mimi nataka kutilia mkazo na kuunga mkono serikali ya majimbo. Lakini nataka kwenda hatua moja zaidi ya kukubali serikali ya majimbo. Ukweli ni kwamba iwapo serikali ya majimbo, majimbo mengine watakuwa wamepinga kuwaandika kwa serikali ya majimbo, lile jimbo ambalo lina asilimia themanini na tano ya raia wake ambao wanaunga mkono serikali ya majimbo. Napendiekeza kwamba wapatiwe haki ya kujitenga ili waweze kujitawala wenyewe (**clapping**)

Pili, napendekeza ya kwamba wale ambao wamekuwa viongozi wa serikali hii na pengine wametoka katika uongozi, Katiba ipewe mamlaka kwa serikali zinazokuja ziweze kuwashtaki kujibu mashtaka fulani wa katika uovu wao wa uongozi. Kwa hivyo napendekeza kuwa katiba mpya iwe na kifungu cha kuwa ita viongozi waliopita miaka ya nyuma wajibu mashtaka fulani.

Tatu, upande wa elimu, naunga mkono kwamba kuwe na elimu ya bure kuanzia nursery school hadi darasa la nane, iwapo system itakuwa ni ya 8-4-4. Lakini nataka kusisitiza hapa ya kwamba iwapo jimbo lina uwezo wa kirasili-mali katika upande wa elimu iweze ku-sponsor baadhi wa wanafunzi kutoka kila district kwa elimu ya secondary na ya university ili kuwa na usawa katika usambazaji wa elimu ya juu. Kwa hivyo serikali ya jimbo ama serikali kuu iweze ku-sponsor mbali na kutoa loan, iweze kuchagua wanafunzi fulani katika district kusudi wapate elimu ya juu kuanzia secondary hardi university level.

Rais napendekeza ya kwamba asiwe mwanasiasa, achaguliwe kutoka upande wowote mwingine lakini asiwe mwana siasa kwa sababu atakuwa ceremonial President hatuna haja ya mwana siasa. Lakini kuwe na Prime Minister ambaye ndiye atakaekuwa kiongozi wa serikali mwenye uwezo wa kuchagua baraza la mawaziri.

Upande wa afya ningependekeza ya kwamba watoto wenye chini ya miaka mitano na watu wazima wenye zaidi ya miaka sitini na tano wapatiwe huduma za afya bure.

Upande wa uchukuzi (transport): Napendekeza ya kwamba kila location iwe angalao na kilometer kumi na tano (15 km) za barabara ya lami. Halafu barabara za kijijini zinazo- unganishwa na barabara kuu zote kama hazina lami ziwe na murram. Tuweze kurahishisha uchukuzi.

Kilimo: Mti wa mnazi napendekeza ya kwamba katiba isisitize ya kwamba ufanyiwe reseach ama utafiti wa hali ya juu kusudi

product zake ama mazao yake yaweze kujulikana, nimazao gani yanaweza tumikia katika kuendeleza uchumi. Na mitambo ya butter iweze kutolewa kutoka ma-town na kuletwa katika vijijini ambapo mnazi unakuzwa. Kwa hivyo iwe ni sheria kwamba viwanda zote za butter na mafuta ya nazi zichukuliwe kutoka town na kuletwa vijijini ili kusudi kuwe na urahisi na kuweza kurahisisha usafiri na pia bei iweze kuwa juu kwa sababu watondoa ile element ya transport.

Local Government. Napendekeza ya kwamba Councillors wachaguliwe na raia na kiwango chao cha chini cha elimu kiwe Form 4. Kwa sababu miaka 38 ya uhuru hatuwezi kuendelea na ma-officers au ma councillors ambao wana chini ya kiwango cha elimu cha Form 4. Kwa vile technology imezidi na hali ya uchumi na mayandilano katika mabaraza yamepanda sio majadiliano na lugha ya kiswahili ama lugha za kinyumbani. Hivyo basi liwe jambo la lazima kwamba anayepigania u-councillor awe na elimu ya chini ya Form 4. Mbunge elimu yake ya chini iwe diploma level. Na Rais na Prime Minister wawe na degree level.

Security: Hali ya security isimamiwe na serikali ya jimbo kiasi ya kwamba polisi wachaguliwe ama wawe wakikuwa recruited na jimbo lenyewe na kuwa trained na jimbo lenyewe. Upande wa jeshi recruitment tuwe na quota system. Hali ya kwamba kila jimbo litakuwa na kiwango fulani, number fulani, ya wanajeshi. Isiwe hali ya kwamba viongozi wote wa majeshi wanatoka katika kabila moja kuleta sura ya kwamba hawezi "ku-traini-iwa" na wakawa effective katika upande wa security. Kuwe na usawa.

Upande wa employment: Napendekeza ya kwamba mashirika makumbwa ambayo yanapatikana katika jimbo yachukuwe wafanyi kazi wake asilimi sabnini na tano (75%) kutoka jimbo hilo asilimia ishirini na tano (25%) wawe wanaweza kutoka majimbo mengine ya nchi.

Corruption: Napendekeza ya kwamba katiba isisitize ya kwamba isiwe na hali ya kubembleza corruption. Afisa yeyote ambaye atapatikana katika hali ya corruption aweze kutolewa, aweze kupelekwa kotini na kushitakiwa na kupigwa marufuku ya kufanya hata biashara kama ametolewa kazini. Ama kurudi tena kuandikwa kazi mahali popote pale. Na pia asiweze kupigania kiti chochote cha kuchaguliwa.

Civic education pamoja na Katib: Napendekeza ya kwamba civic education iwe ikiendelezwa kila siku isingonje tu wakati wa kupiga kura. Na Katiba iweze kuandikwa katika lugha ya kabila zote za Kenya. Na copy yake iwe katika kila afisi ya chifu. Iwe inapatikana copy ya Katiba.

Tembo ya mnazi: Nataka kupendekeza kwamba katiba mpya ipatie huru pombe ya mnazi ili iweze kuuzwa katika sehemu zingine za Kenya bila vikwazo ama vizuizi vyoyote. Ili iweze kushindana sawasawa na beer zingine ama pombe zingine ambazo ziko sokoni.

Miraa: Napendekeza ya kwamba ipigwe marufuku Kenya nzima ama kama Kenya nzima haiwezi kupigwa marufuku kila jimbo liweze kujiamulia kama linataka miraa iuzwe katika sehemu hiyo au la. Na kama jimbo limekataa miraa kuuzwa katika sehemu hiyo basi isuruhusiwe hata kidogo kuuzwa.

**Com: Lethome**: Maoni yake hayo.

Rasili-mali: Ningependekeza kwamba rasilmali ambazo zinapatikana katika kila jimbo zisiweze kutumika bila idhini ya asilimia themanini na tano ya raia wa jimbo lile ili kusudi waweze kufaidika. Na kama ni kampuni kubwa ambayo inataka kuchimbua madini fulani katika jimbo fulani basi ipatiwe jukumu la kuendeleza barabara sehemu hiyo ama infrastructure ama upande wa afya, mashule na mahitaji mengine katika sehemu ile ambayo madini hayo yanapatikana.

Napendekeza kwa vile hapa pwani kumepatikana titanium kule Kwale na sehemu zingine za kule Coast kwamba madini ile isiweze kuchimbuliwa bila ya raia wenyewe wa jimbo la pwani kutoa idhini ya jinsi ambayo yatachimbuliwa ili kusudi waweze kufaidika wasiweze kunyanyaswa na serikali zile ambazo zimekuwa corrupt. Na Directors wa kampuni ambayo zinahusika na kuchimbua madini waweze kujulikana wazi wazi wachapishwe magazetini wajulikane na kuongea na historia ambako wametoka na historia ya kampuni ile katika ujuzi wa kuchimbua madini pia iweze kujulikana.

Voters registration na hali ya kutoa vitambulisho pia iwe inaendelezwa kila siku isingoje wakati wa kura. Na vitambulisho ziweze kutolewa kwa Chifu kwa sababu naamini ya kwamba ofisi ya Chief ikipatiwa wafanyi kazi wanaohitajika wana uwezo wa kutoa vitambulisho kwa urahisi. Raia wa kigeni wasiruhusiwe kupatiwa vitambulisho kama refugee wasiweze kupatiwa vitambulisho lakini watengenezewe vitambulisho vyao vya kuwa ni wageni ama refugees.

Food security (chakula): Napendekeza ya kwamba kila jimbo liwe na silos ama maghala ya kustore mahindi ama chakula, mchele, maharagwe, ngano n.k. ili kusudi iwe rahisi kupambana na njaa kama imehusika katika jimbo lolote.

Maji: Maji iwe ni lazima katika Katiba kwamba kuwe na maji kwa raia wote wa Kenya. Ikiwa haiwezekani basi napendekeza kwamba visima viweze kuchimbwa na kusiwe na umbali wa 200 metres kutoka kwa kila nyumba pamoja na ma-boreholes pia yaweze kuchimbwa, pamoja na dams.

**Mulewa**: Jina langu naitwa Esther Kanze Mulewa na mimi ni mkaazi wa hapa Kaloleni. Yangu ni machache sana kwa sababu kwanza nitaguzia katika Katiba. Katika Katiba yetu tuliyo nayo sasa Rais amepewa uwezo mkubwa kwa hivyo ningependekeza upunguzwe. Haijalishi ni aina gani ya serikali tutakuwa nayo, iwe ya majimbo ama serikali ya umoja lakini kama Rais atakuwa na uwezo kama alivyo nayo sasa kutakuwa hakuna tofauti. Kwa maana mwisho atakuwa dictator na hiyo ndio shida kubwa tuliyo nayo.

Tukiendelea upande wa Katiba amendments kurekebisha Katiba bungeni. Katiba tuliyo nayo kutoka wakati wa uhuru ilikuwa katiba nzuri sana na mimi nimeipitia, nimeiona lakini kwa sababu kurekebisha Katiba bungeni imekuwa ni mchezo ikiwa nintaka fulani aingie bunge nitarekebisha hivi ili aweze kuingia, nikitaka fulani atoke nitarekebisha hivi atoke. Ifanywe vingumu zaidi ya Katiba kurekebishwa bungeni, kuwe na sheria ngumu ambayo itaifanya katiba isichezewe na Serikali kama vile wanavyotaka kama wanavyofanya sasa.

Jambo lingine ni corruption ama ufisadi. Mambo yote haya tunasema hapa tunataka kufanywe hivi yote yako katika Katiba. Lakini kwa sababu ya corruption/ufisadi watu wanaweza kuhonga wakafanya makosa bila kuchuliwa hatua yoyote. Kwa hivyo wakati tunapopigania Katiba irekebishwe jambo la kwanza la kuondoa katika Katiba mpya ni corruption. Tuweke sheria ambayo itasimamia corruption na mtu yeyote atakaye fanya ufisadi kuanzia mwanzo (grassroots) awe ni Sub-Chief, ni chief, ni Councillor ni nani … achukuliwe hatua kali kwa maana wale wanaolalamikia mambo ya mashamba wananyanyashwa kwa sababu ya corruption. Yule ana pesa atasikizwa na yule hana atatupiliwa mbali. Corruption tunakikishe imechukuliwa hatua ya kutosha.

Tukiangalia upande wa uchumi wetu, wengi wanalalamikia mnazi. Mnazi ni mti wa maana. Tusilalamike kwamba turuhusiwe kugema, tunywe, tuuze. La. Serikali iweke sheria ambazo zitaufanya mazao yote ya mnazi yawe na soko. Ukigema tembo lako unapeleka sokoni kama vile mwenye maziwa anakamua anapeleka Dairy. Linanunuliwa, linafanyiwa kiwanda lichujwe litiwe kwenye chupa, lifunikwe vizuri lipelekwe ngambo tupate pesa za kigeni. Hatutakuwa walevi wa kunywa tukilala mabarabarani lakini mnazi wetu utakuwa unatupatia pesa. Kama ni fagio, kama ni makuti, ya-patiwe soko. Kwa hivyo kile tunachotaka ni soko la bidhaa zetu za kutoka kwa mnazi. Hatutaki kunywa mnazi tulewe tuanze kupitwa na watu wanaotoka nchi zile zingine halafu tuje tulalamike ati watu wa pwani tunanyanyaswa. Ikiwa tutakunywa mnazi tujisahau tukakosaje kunyanyaswa? Lazima tunyanyaswe na watu ambao wametoka nchi zingine! Ama sehemu zingine za Kenya. Kwa hivyo langu ni kuwa mnazi utafutiwe soko la bidhaa zake zote tuweze kuziuza bila matatizo.

Tukirundia upande wa elimu mimi ninaonelea kwamba tuondoe 8-4-4. Mimi ni mwalimu wa miaka mingi na wale wanani-jua wanatambua hivyo. Lakini 8-4-4 si nzuri, kwa mtu yeyote. Kwa hivyo serikali iondoe 8-4-4 kwanza. Pili, ikiwa elimu itakuwa ya bure kuanzia darasa la kwanza mpaka la nane tukiingia upande wa secondary hata kama serikali itakuwa haina uwezo wa kutoa elimu ya bure kwa wanafunzi wote lakini ijenge shule. Madarasa yajengwe na serikali, kama ni physical facilities zingine kama lab equipment, na nini, serikali itoe. Pamoja na hivyo ilipe waalimu. Kama wazazi watatoa karo watoe karo, kindogo ya kugharamia mahitaji yale mengine madogo madogo kama ya kununua vitabu, chalk n.k. Kwa hivyo ile cost sharing serikali ichukuwe sehemu ile kubwa na hasa ya kujenga mijengo katika shule. Wakati huu majengo wa shule nyingi utaona ni mabovu kwa maana wazazi ndio wanatakiwa wajenge na ni maskini.

Tukija upande wa adminstration, provincial administration, ni upande wa Machifu, Sub-Chief n.k. Wanatakiwa wachaguliwe kuanzia PC, DC, DO wale serikali inachagua lakini ikifika chief kurudi chini wananchi tupewe uwezo wa kuchagua. Tukija

upande wa Macouncillor, elimu ni muhimu kwa maana mtu mwenye elimu ndiye anajua maana ya elimu kwa hivyo tunahitaji watu wasome na tunahitaji kuwapa wale vijana wetu wenye elimu ya juu hizi kazi zetu tulizonazo kwa maana sisi tumechoka. Kwa hivyo councillor wapewe vijana walio na elimu ya kutosha ambao wataweza kuendeleza elimu katika nchi yetu kuanzia Form 4 na kuendelea (**clapping**).

Civic Education: Hayo yote tunayo-zungumza hapa wakati watu wakizungumza wengine wanavuna ni kwa sababu ni mambo ambayo labda hayahusianina katiba. Nimalalamiko yetu ya kibinafsi sababu hakuna civic education, lakini hii kwa sababu ni kitu cha muhimu inatakiwa ihusishwe katika masomo ili kama Tanzania. Tanzania kuanzia shule za msingi watoto wana-funzwa mambo ya Katiba na ya sheria katika nchi yao. Kwa hivyo inastahili. Ukiangalia mambo ya urithi yako katika Katiba yetu ya sasa ni kwa vile tu hakuna mtu wa kutuelimisha. Kama ni yale mambo mama amezeungumzia kijana amtie msichana mimba hiyo iko katika Katiba kwamba ukiwa umzazi unastahili kulea mtoto wako. Lakini, kwa vile hatujui tunaona haiko kwenye sheria. Mama ana-achiwa, msichana anaachiwa ulezi pekee yake hata yule Chief, Sub-Chief, hakuna kule chini wa kueleza watu vile wanastahili kufanya. Tukiingilia upande wa wanawake tumedai vitu vingi sana lakini mimi langu liko tofauti kidogo. Mimi ninasema wanawake wapewe ile nafasi lakini wapiganie kama mtu mwingine yewote. Tusipewe sahanini, tupiganie. Kama ni kuchaguliwa tupigane sawa sawa na wanaume kwa nguvu zetu wenyewe. Yule atakayefaulu atakuwa amedhibitisha kwamba yeye anaweza (clapping).

Mswada kuhusu wanawake, lile limezungumziwa na mheshimiwa hapa, mimi nasisitiza kwamba huo mswada upite kwa sababu hakuna mtu mwenye haki ya kupiga mwenzake hapa Kenya. Ukipiga mkeo ni kosa, ukipiga mumeo ni kosa kwa hivyo musaada huyo upitishwe ili ule atakayemkosea mwenzake akiona anastahili kumshtaki aende akamshtaki. Sheria ilinde kila mtu, kusiwe na mwingine hata-lindwa na sheria.

Mwisho tumezungumzia umasikini. Hatutaisha umasikini Kenya kwa sababu hakuna food policy. Hakuna sheria inasimamia uzalishaji wa chakula. Mimi hivi mvua inanyesha sijalima na hakuna mtu ataniuliza kwa maana nategemea nisipopata chakula si musaada utakuja? Lakini kuwe na sheria kwamba kila mtu mwenye ardhi aitumie, naasipoitumia apatwe aulize mbona hujalima wategemea chakula utapata wapi? Kwa hivyo food policy inahitajika, ili chakula kiweze kuzalishwa kwa wingi. Nilikuwa nayo mengi lakini nafikiri kwa hayo machache Mungu atawabariki (**clapping**).

**Com. Lethome**: John K Mwaduna.

**Mwadula**: Hamjambo wananchi? Mimi jina langu naitwa John Kenga Mwaduna. Mimi ni mzaliwa wa hapa Kaloleni, naishi hapa Vishakani. Yangu ni machacheu mengi yamesemwa. Mimi kilio changu kikubwa ni kwamba watu waliokuja hapa wengi wao wanasema majimbo na tunasikitika kwamba tumeharakishwa. Na-jua-aje tumeharakishwa? Kuna vipengele ningetaka watu wafikirie. Katiba iliyoko hapa Kenya kwa wakati huu tulionao ilikuwa tangu hapo ni ya majimbo na ikiwa Commission ina-jua hivyo, na inajua muda ni mchache kwa nini wasichukue tu ile ya zamani mara moja wakaileta mbele hapa? (**clapping**)

badala ya kusema kwa hatuwezi kwenda uchaguzi kwa katiba hii mpya na hali hiyo Katiba kutoka Lancaster House iko wazi na ilikuwa nzuri sana?

Lakini hakuna neno vile mnavyochukua. Pendekezo langu ni kwamba hata haya majimbo tunayosema, kila jimbo lina mpaka wake, lakini hatujataja mipaka hapa. Tunasema majimbo, majimbo ni kutoka wapi mpaka wapi? Jimbo letu la Pwani tangu zamani ilikuwa ni kutoka bahari mpaka Mtito Andei na iko katika Katiba (**clapping**) pale Bondeni - pale Mtito Andei kuna bonde hapo. Hapo ndipo ilikuwa mpaka wa Pwani, yaani kutoka hapo kuja huku ndilo jimbo na tunataka kusema ipewe uwezo.

Uwezo gani tunataka? Kwanza, tunahitaji polisi iwe mikononi mwa jimbo. Wafanyi kazi waandikwe kutokana na majimbo wa wale jimbo lile wanatoka waandikwe pale. Kuna sehemu zingine ambako ni ngumu. Jimbo lile laweza kukosa provision, kama hakuna engineer mahali pale anaweza kuchukuliwa kutoka jimbo lingine lakini jimbo lenyewe liwe na uwezo wa kuandika. Wanao omba jimbo lingine, kama tunavyona tunao Majudge hapa, wengine wameletwa kutoka nchi zingine kuja katika Kenya ili kuitekeleza. Ni sikitiko kuona kwa wakati huu tulionao muda sio murefu pesa nyingi za serikali zinakwenda na hali jambo lenyewe ukiangalia ni jambo hasimu kwa sababu hii Katiba haikufanyiwa utaratibu wowote - hikufanyiwa rehearsal tukajuwe hii Katiba ni mzuri ama ni mbaya Katiba hiyo ilifunikwa, ikaletwa ingine kutokana na mchezo ulifanywa ndani ya Parliament pamoja na President aliyekuwako ikawa ni kwamba ni kama imetupwa. Watu wa-kasahau kuna majimbo, lakini katiba iliyokuja tanu mwanzo ilikuwa ni ya majimbo.

Tungependa pia Polisi na revenue iwe chini ya majimbo. Katika hii revenue ndiyo tunasema 10% inakwenda Central Government lakini 90% inabaki hapa hapa katika jimbo. Sisemi kuwa ni jimbo hili pekee yake, ni majimbo manane yote inafanyika hivyo. Tukingia kipande kingine cha Serikali, ikiwa jimbo tume-chagua haijalishi ni President au ni Governor wa jimbo, yule atakayekuwa kiongozi wa jimbo ndiye mwakilishi wa central government anachua madai kutoka kwa jimbo anaenda kwa Central Government na kueleza vile mambo yalivyo. Hakuna haja ya kuwa na Vice-President na Prime Minster. Ikiwa President ako huyo ana cover e.g. katika America tunaye President, hana Prime Minister, lakini kwa sababu yeye ni overall wale Magovernor walioko pale wanapeleka report zao kwa Central Government. Ni maoni yangu ya kwamba huyu ambaye ni President au Governor wa jimbo yeye ndiye atakuwa akiwakilisha Central Government.

Nikirudi nyuma, Katiba hii iliyoachwa anafahamu wazi kwamba tulikuwa na senate - Wabunge walichaguliwa kutoka ……… Lakini tukiangalia upande wa ki-financial inachukua pesa nyingi kwa sababu kutakuwa na ma-bunge wawili upper house na lower house. Lakini tulichukuwa hapa kwamba hii region itakuwepo, region ichukue percentage zote za watu wa nchi ile wawe kwa jimbo lile. Halafu kuwe na mwakilishi anayekwenda katika senate ku-represent mambo ya jimbo lake. Kwa hivyo kutoka wakati huo, ingawa nina mengi, nimekuja upande wa utawala pekee yake ambapo tuna bahati mzuri tuna port, tuna revenue mzuri na iwe ni mali ya jimbo si ya kuachiwa hapa msaada, mnada kwenda kutafutiwa tajiri aje anunue. Ikiwa hivi sasa bado court ni yetu na wanajiliwa hapo sisi ambao ni wajimbo hili hatufaidiki, je, ikiwa ni mtu binafsi ametoka huko amekuja amenunua

tutapata kitu gani? Kwa hivyo mimi nimesoma upande huo tuachie hapo. Nafikiri mengi yamesemwa.

Tukija upande wa mnazi ni mambo yanasemwa yaku tosha. Nikiunga mkono huyo mama aliyekuwapo sasa hivi ni kwamba mnazi utafutiwe soko. Wakati tunasema mnazi haufai wale security wanaendelea kuwashika kwa sababu sisi wenyewe tunasema watu wanashikwa kwa sababu sisi wenyewe tunasema watu wanashikwa lakini hao ni viongozi tulio nao. Mimi nasema tu juu ya viongozi. Napendekeza kwamba viongozi walioko wasiwe watu wa kujitafutia matumbo. Ninahitaji ya kwamba viongozi wawe ni watu wanapigania haki zao na za raia alikochaguliwa. Awe atapigania. Lakini sasa ukiwa bubu; yule kiongozi akiwa ni maziwa lala nasema ni kwamba yeye aitwe na chama kilichomchagua aje apewe discipline. Ikiwezekana aweze kuondolewa tupate kongozi mwingine. Asante.

**Amani:** Kwa majina naitwa Alfred Amani. Kwanza napendekeza serikali ya majimbo. Pili umri wa kuchuka ID card upunguzwe mpaka ……………..

Katika upigaji kura na kuchukua vitabulisho age ipunguzwe mpaka 16 years. Kwa sababu …………… Kazi achukuwe 90% from coast halafu 10% achukuwe kutoka kwingine, ili pia wale watu wa Pwani wapate kazi. Lazima haki za binadamu zidumishwe kila mtu apatiwe ile haki yake. Hii ni kwa sababu kama juzi baada ya watu wa Kenya Airways walipogoma tunaona wengine walifungwa wengine wakashtakiwa, ile si vizuri. Wale wanagoma wanataka haki yao kwa hivyo serikali iangalie haki yao, iwapatie haki yao.

Kama waalimu wamegoma kwa sababu ya mishahara, mishahara iongezwe lakini si kuwa ati kama mwalimu amegoma anafutwa. Hiyo si haki ya binadamu. Katika kila jimbo kuwe kutakuwa na university na national schools. Halafu katika uchaguzi wa Wabunge, mbunge ni lazima awe na elimu ya Form Four ndio achaguliwe ili kupunguza kule kusinzia kule bunge (**laughter**). Machifu lazima wachaguliwe lakini kuchaguliwa kwa Machifu wawe amefika Form 4 pia ndio achaguliwe. Asanteni (**clapping**)

**Com. Lethome**: Erastus Mwambire.

**Mwambire**: Commissioners na wakaazi wa Kaloleni wote waliofika langu tu naanzia na aina ya serikali ambayo tunahitaji katika mkoa wa Pwani maana wale wameingia hapa wamesema kuna kabila arubaini na mbili katika nchi hii nzima ambao kwa kila kabila hatuwezi kwenenda kwa mwenendo mmoja kuwa sote ni watu tofauti na mahali tunaishi kila mtu ana vitu tofatuti ambavyo anategemea; vitu muhimu kwake, kila kitu kichukuliwe kinachotoka na umuhimu wake pale kiko. Kwa mfano mnazi na kahawa. Mzee mwingine alipotoka hapa alisema kwamba tukate mnazi tupande kahawa pale nyumbani, nina mfano mzuri, tulipanda kahawa mti mia moja hamsini sasa bado tisa na imefika miaka kumi na mbili hakuna hata mmoja ulio zaa hata sasa ile hali na mchanga pale hauwendi na ile hali ya pale. Kwa hivyo kila hali hii serikali ya majimbo itakuwa mzuri maanake ile tegemeno ya kule naishi ndiyo ile itanisaidia penye napoishi kulingana na pesa ya jimbo itakavyotumika na hii serikali ipeleke

15% kwa serikali kuu.

Hiyo serikali kuu itakuwa na uwezo mdogo na ni kazi dogo itakuwa ikitelekezwa na Serikali kuu kushinda ile kazi ambayo majimbo yatakuwa yanateleza maana kila jimbo litakuwa na waziri kuu na bunge katika lile jimbo na mahitaji ya wale mawaziri katika ile jimbo watatakiwa walipwe na fedha za kila jimbo. Vitu vinavyoingia kutokana na kila jimbo vinahitajika vigawanywe kama ni kupelekwa kwa jimbo ingine 75% imbaki kwa lile jimbo kwa manufaa ya lile jimbo, halafu 25% iende kule jimbo lingine kama kuna uhitaji.

Kwa mahospitali ni pendekezo langu kwamba kila location iwe na dispensay ambayo inaweza kuweka wagonjwa wasiopungua 150 walale pale. Tukitoka kwa location kuwe na National hospital kila division ama hospitali kuu kwa kila division ambayo itachukua wagonjwa kwa kila division pale. Halafu kuwe na vifaa vile vinatibu kia magonjwa pale si kwamba lazima upelekwe kwa hospitali ya mtu binafsi ama serikali ziwe hazina nini hiyo tunakataa. Ule Prime Minister atokane na lile jimbo lenyewe. Kusikuwe na nomination ya Councillors na MPs. Mbunge yeyote ambaye hatakuwa kwa kikao cha bunge zile allowances ambazo anapatiwa asipatiwe.

Kuwe na university kwa kila jimbo, waingeleza wa-kasema (necessity is the mother of invention) mahitaji ndiyo mama wa uanzilishi wa kila jambo. Tukangalia serikali ya sasa zile training colleges zote ziko Nairobi. Ile training iende kulingana na vile vitu vinavyofanywa pale, kama ni hotels, na wale wengine ambao wanakuja hapa nao wapelekewe zile colleges ambazo ule ujuzi unapatika hapa ufanywe vile vile.

Pendekezo lingine, Wabunge wasifanye mareekebisho yoyote kwa Katiba maanaa wao ndiyo wana tatiza hiyo hali ya sasa. Maana walifanya marekebisho ukifuata vizuri sana sasa ile katiba ambayo wanafuata unaona zile allowances za wabunge vile ziko nyingi na kuna wizara nyingine ambazo wanalalamika hawana pesa. Ikiwa sasa Mbunge amekaribia ule mshahara wake ni 700,000/= it's a lot of money na hao ndiyo wamejibandikisha wanafanya wale wengine wanakosa umuhimu wa mahitaji yao. Napendekeza mshahara wao uwe unakaliwa na huyo Prime Minister ndiyo ambaye anatoa salaries za Wabunge ambao watakapopatikana wakichaguliwa, kuwe na kamati ambayo itashughulikia ile mishahara yao. Na kuwe na kiwango cha miaka ambacho kila Mbunge anashtahili kuwa na cho kipindi cha sehemu mbili ambacho ni kipindi cha miaka tano kwa kila kipindi moja; awe ni mzuri awe ni mbaya, sharti aondoke pale kuingie mwingine.

Kumalizia kuwe na rotational Chiefs awe na kiwango cha elimu cha chief maana elimu sio sana uongozi - zinaingia tofauti. Chief awe ameowa, ama ameolewa kutoka pale eneyo anapotoka achaguliwe na wa kaaji wanaojua tabia zake na vile anapoishi katika lile eneo anatawala. (**clapping**). Sub-chiefs wachaguliwe na wale watu wanaokaa pale anapotawala na awe permanent na pia awe na muda wa kutawala. Asiwe mpaka aende mpaka retire, azeeka pale anaharibu haribu la, tuwe na wakati mzuri wa Sub-chief kutawala. Napendekeza awe na miaka nne ya kutawala. Madiwani wawe na elimu ya chini kidato cha nne na kuendelea. Kwa hayo machache Asanteni. (clapping)

**Com. Lethome**: Denah Mwabai.

**Mwabai:** Asante sana kwa hii tume kuja hapa. Jina naitwa Denah Mwabai. Maoni yangu ni majimbo. Tena elimu iwe ya bure kwanzia nursery mpaka darasa la nane. Na mengine yamesemwa tayari na mimi sina la kusema kwa hivyo yote yamesemwa. Asante .

**Idi A Katana**: Asante sana Ma-commissioners. Mimi niko hapa kujaribu kutoa maoni yangu juu ya kubalisha katiba. Lakini kitu napenda sana kusisitisa na kujaribu kutoa mawazo yangu ni juu ya chapter 6 ya katiba ambayo tuo nayo sasa ambayo ya hisika na matumizi ya pesa ya uma.

Pesa zote zinazokusanywa za ushuru, (tax na revenue) na kama Port Authority na Authority nyingine, KRA, na nyingine mchanganyiko, pesa zote huwa zinapelekwa treasury ambako zinasimamiwa na Controller and Auditor-General. Na hapo wanasaidiwa na Paymaster-General na wengine. Baadaye pesa zile zinapelekwa kwa bunge, National Assembly. Wanazungumza halafu katika kila mahitaji ambayo inatoka kwa District au kwa Province wanatoa mahitaji yao halafu baadaye ndiyo zinagawanywa kupelekwa huko. Lakini matatizo ambayo iko ni kwamba wananchi wanalia wanasema pesa zikigawanywa haziwafiki kama Kilifi, Mombasa sasa hapo katika shuguli zangu za kwanba ningeweza kutoa mawazo yangu juu ya mabadiliko ya chapter 6 ya hayo matumizi ya pesa za uma ni hivi.

Tungependa collection yote inayofanywa, iwe Revenue, tax ,authoriy zote katika kila jimbo pesa zikikusanywa ziwe zitabaki pale pale katika jimbo. Ni katika kila jimbo wachague kamati yao ama authority yao wafanye budget yao wajue watatengeneza bara bara, mashule, mahospitali au kama ni university. Budget yao ikikamilika sawa sawa, ikiwa katika jimbo lile wamekusanya million mia nane na pengine katika matumizi yao kama ni estimate zao za budget yao ni million mia sita, pesa zile ambazo zitashughulika na matumizi ya budget yao ziwe zitambaki pale pale katika lile jimbo kutokana na vile watakusanya sio lazima pesa zote zipelekwe kwa treasury halafu ndiyo baadaye watu wapige magoti waende kuomba pesa zipelekwe kwao.

**Com. Lethome**: Zipelekwe asilimia ngapi pale?

**Katana**: Kama 80% ibaki na pia itategemea pale vile kamati ya jimbo imeamua matumizi yetu ni shilling fulani. Zitakozobaki kama ni 20% ziende kule kwa treasury ambako kule Controller na Auditor General atajua pesa zile zitatumika kwa shughuli za Central Government. Hiyo itakuwa juu yake mwenyewe. Kitu nimeona muhimu katika collection ya tax au revenue ni kuwa ikiwa kutakuwa na kamati kwa kila province au region, ikiwa itakusanya pesa nyingi hapo ndipo ufisadi utapunga maanake itakuwa competition ya kila jimbo na vile utakavyofanya pesa ziwe nyingi zaidi ndiyo percentage yenu itakuwa kubwa na ambayo mtapeleka kwa treasury itakuwa ndogo.

Kwa chapt.7 kwa katiba tuliyonayo sasa Chairman wa Public Service Commission ni mmoja tu ambaye yuko kule Nairobi. Sasa wakati wowote inabidi kuwa watu wote kila mara wakienda kwa interview inabidi wanatravel Nairobi kwa Public Commission wanafanya interview kule. Sasa hapo kuna uwezekanao kwamba hata kama watu ni wazuri wa kutoka jimbo fulani lakini wakitoka kule Nairobi wanaweza kufanyiwa njama yoyote hawawezi kupita. Lakini kama zile nguvu za Chairman Public Commission zimegawanywa kwa kila jimbo, sasa itabidi kila jimbo linajua ni kijana yupi mzuri na wale wenye jimbo pale wawe wamechagua committee yao ambao ni wale wale na majina ambayo watakuwa awamefanyia interview ni yale yale.

Napendekeza kuwa wale ambao watakuwa wafanyiwe interview na kwa vile Public Commission itakuwa imegawanya kila jimbo ni watu wa pale pale kwa hilo jimbo ndio watajua watu wale wako pale. Sio kwamba interview inafanywa halafu mtu anatoka Nairobi anaitwa pengine Kariuki Mwangi aje afanyiwe interview Kilifi huku halafu watu wa Kilifi waambiwe tumechukua watu hamsini kumbe mmoja sio ka kilifi. Akichukua hiyo anarudi zake kule. Asante sana

**Charo Kidzao**: Asanteni sana. Mengi yamezungumzwa lakini pia mimi ningependa kuongezea katika aina ya serikali ya majimbo. Napendekeza kuwe na majimbo na katika mapendekezo yangu na sema kuwe na Rais anayepata advice kutoka kwa National Advisory Council, ambayo itakuwa ikimpatia mwongozo na pia itakuwa ikiangalia mwelekeo wa nchi, zile policies za nchi maanake kulingana na siasa za siku hizi unapata kuna chama fulani, wakati wote kikishindwa chama kingine kinaweza kuingia. Kwa hivyo kuwe na muelekeo fulani ambao council ndiyo itakuwa inaangalia; ndiyo hata serikali ingine iikingia ule mwelekeo usiwe unabaidirika baada ya miaka tano, serikali ingine ikiingia inafuata mwelekeo usiwe nabadilika baanda ya miaka.Huu muelekeo naongea uwe unaongozwa na hii council, iwe imetengenezwa na watu professionals, si politicians. Kwa mfano economists, bankers, mambo ya security ili waweze kumuongoza yule President atakaye-ingia pale vizuri.

Halafu hawa watu pia wawe wanachaguliwa kutoka yale majimbo manane ya Kenya. Hii National Advisory Council ina-advice ile government iko pale katika National and Foreign policy, iwe ina angalia mambo ya security, halafu iwe inafollow up matters ambazo parliament inaweza kuwa ina lalamika. Kwa mfano, jambo kama la 'Goldenberg' pengine kama serikali haifuatilii ile National Advisory Council iwe inafutilia kuangalia mambo yalienda vipi ili wahusika wawe wanaweza kushtakiwa.

Halafu wawe wanaangalia ile unity ya majimbo yaliyoko pale ili isigawanyike kabisa ili wakawa pengine wanataka uhuru iwe hawa ndio wanaangalia unity wa majimbo yale mengine. Pia hawa watu wawe wanaangalia zile complaints za watu kama jambo fulani halifanyiki kwa mfano, jimbo fulani ikiwa kuna shida fulani serikali yake haifuatilii sana kuwe kuna committee fulani ambayo imekuwa decentralized kutoka kwa hii National Advisory Councils kwa lile jimbo ambayo itasikiza zile kesi kuwa zitapelekwa kwa National Council ha hilo jambo liwe linafuatiliziwa ili ikusiwe na ile issue kwamba region fulani kuna shinda Fulani lakini regions zingine haziwezi kuingilia itakuwa si vizuri kwa hivyo hii National Advisory Council iwe decentralised na iwe inasikiza shinda za wale watu. Kukiwa na shida kama Serikali haifuatilii ule region iwe wanapata hii National Advisory Council ikiwa independent na composed of professionals, wawe wanafuata lile jambo vizuri.

Na katika Federal Government yule Rais awe na at least first degree pia hii government iwe concerned na polisi na Armed Forces, Foreign affairs na welfare ya majimbo kwa mfano kukiwa na njaa kwa jimbo fulani yale majimbo mengine yaweze kuhusishwa ili ile njaa iliyomo jimboni iweze kutatuliwa.

Katika hizi Regional Assemblies hawa wawe wanakuwa kwa region, kama ni barabara, elimu, agriculture wawe wanahusika na mambo kama haya na wawe katika lile jimbo, zile appointments zitakazofanywa kwa public offices ziwe veted na ile assembly ya ile jimbo zisifanywe tu hivi hivi.

Katika Regional Government iwe composed na representatives kutoka zile counties katika lile jimbo. Si Councillor achaguliwe direct aende katika regional assembly. Katika zile counties ambazo ziko wale Macouncillors wakienda kwa respective counties wawe na representatives ambao wanaweza kuenda kule Regional Assembly ili kusiwe na watu wengi sana. Halafu huyu Governor pia awe elected direct na hao wananchi wenyewe.

Katika hii constitution pia napendekeza hii lugha inatumiwa tukianza kutumia hii lugha ya malawyers nafikiri itakuwa inaccessible kwa watu wa kawaida ambao hawakuchukuwa masomo ya ulawyer. Kwa hivyo iwe simplified na kama itawezekana hizi lugha zetu pia ziandikwe. Kwa mfano ki Rabai, kichoni, Giriama ama Kiswahili. Vile vile katika hii majimbo, hii corruption iwe checked na hii National Advisory Committee kwamba mtu akipatikana na makosa kama hayo, hii National Committee ambayo itakuwa independent wawe wanashughulikia lile jambo. Hapa na jaribu ku-emphasize mambo ya politics na professionalism kwamba tukiingiza politics sana katika maendeleo ya nchi huwa inaharibika. Kwa hivyo tuweke professionalism kuliko policy ili kila jambo ambalo linafanywa liangaliwe linafanywa na nani na anaweza kufanya hilo jambo ama vipi. Hayo ndiyo machache ambayo nikuwa nataka kuongeza.

**Com. Lethome**: Juma Shimba, Hassan Mbao.

**Hassan**: Mimi naitwa Juma Shimba Hassan kutoka Rabai location, Kaliangombe sub-location. Mimi hivi sasa kule ni youth leader katika chama chetu kinachotawala. Katika pendekezo langu kuhusu serikali tunayoitazamia ya majimbo, ukweli ni kwamba sisi hapa Kenya wale wanyonge ndiyo wengi kushinda wale wanaojiomundu kimaisha. Na kwa hali hiyo hiyo ndiyo ya kwamba tunaonekana wadhaifu na sio ya kuwa sisi hatuna akili hata kama kuna wengine nimesikia wakizungumza kuhusu elimu. Elimu ni tochi na tochi unaweza kutumia kwa mfano usiku kwa sababu hakuna giza na kuna usiku mwingine ambao hauihitaji tochi kwa sababu kuna mwezi. Sioni kwa nini utimie tochi na kuna mwezi. Lakini tochi ni muhimu usiku wa giza. Nikisema hivyo ni kwamba mimi nikiwa ni mtoto kwa mfano, nimezaliwa na baba angu ameniacha, ameaga dunia na mama angu ameaga dunia, katika kizazi ninachotoka kwa mfano kuna wababa wadogo ama mababu wadogo kupitia kwa mwanzilish wa familia hiyo.

**Com. Lethome**: Bw. Juma, hebu pendekeza mambo ya katiba naona unachukua njia ndefu sana.

**Juma:** Asante, eh pendekezo langu kuhusu katiba mimi nilikuwa nachangia majimbo nikiona kuwa sisi tukiwa wa Pwani jimbo linaweza kutuletea mazao kwa sababu ya kupitia bahari yetu hiyo kupitia kwa uchumi kama kilimo tukiwa tuna mmea hapa ambao tunaita mnazi. Mnazi ule pale nyuma ulikuwa unasaidia wananchi ambao hawana uwezo wa kuajiriwa kazi kwa vilabu vilivyokuwa vikilipwa ushuru na watu wanaenda kufanyia biashara. Na kutoka hivi sasa ingawaje ule ugemaji unaendelea lakini hakuna uhuru wa wale wagema na wachuuzi. Kwa hivyo mimi nilikiwa na uchungu sana tukiangalia hapa idadi kubwa ni ile ambayo inategemea mnazi kwanzia ile tembo la mnazi lakini kwa sababu hakuna uhuru tunafanya tukiwa wenyewe lakini tunafanya kama wageni kwa sababu hatujapewa uhuru wa kufanya vile tanavyotaka.

Ninaomba inapopatikana hiyo serikali ya majimbo basi umuhimu uwangaliwe wale wako chini kabisa na tukiangalia wale ambao wako chini tunaye kiongozi wa utawala ambaye ni Sub-chief akiongezewa na wa kuchaguliwa ambaye hivi sasa tunamuita Councillor. Watu wale wawili wakiwa ndio wanao kiwango cha kuleta maendeleo katika kule mashinani, ningetaka wale watu wawili wawe wanafanya kuchaguliwa sub-chief achaguliwe na wananchi bila kujali kama yeye amesoma bali awe ana uwezo ama kipaji cha kuweza kuongoza wale ambao watamchagua.

Naye Councillor anaweza kuwa awe na kisomo kwa mfano awe amefika Form 4, Form 6 hata university mradi kwamba awe ana kipaji mbali na elimu cha uongozi kwa sababu kuongoza watu ni vimaendeleo mbali si mawazo. Kwa sababu saa hii nikisama nitapika pilau Kaliangombe sub-location ni-kichaguliwa Councillor basi wale wakisikia lile neno pilau pengine watakuwa na morale lakini watakapo nichagua ile pilau imekwisha.

Pendekezo lingine ni kwamba tukienda umilikaji wa shamba, ile kamati inayosimamia sasa kesi za shamba ambayo imechaguliwana ofisi ya DO mimi ile kamati ningependa ifutiliwe mbali, na badala yake kamati zile ziwe zinaudwa kule mashinani kwa sababu zile ndizo zinazonjua wazi kwamba nambari hii wanapakana kimashamba. Hivyo ningerundia ikiwa tutaweza kuuleta umilikanji wa shamba mipaka ama shamba plot kupita kwa kamati zile ambazo zimeundwa pale kijijini basi zile kesi zitaishia kule kule wala hazitafika kotini. Mimi nilikuwa nikiomba hivyo.

Pili, katika elimu, wale watoto werevu ni watoto ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwapeleka kule mbele. Hivyo basi katika serikali hiyo ya majimbo ningeomba kadili ya vile tunavyoendelea watoto wetu kusoma wale watoto welevu tayari kuwe kuna upelelezi kama wanatoka kwa vizazi vilivyo na uwezo gani kimaisha. Nikisema hivyo ni kwamba tungeweza tupekue pekue wale watoto wakija wakisema amebada la nane naye amepita tayari ile mipango ya kumpleka mbele tulio nayo imeshapatikana badala ya kuweza kupata skuli halafu anaambiwa ngoja bursary, ngoja bursay hapana.

Mimi nilikuwa napendelea vile vile wanavyoendelea kule halafu report za watoto wale waweze kuwekewa akiba. Ili ya kwamba akifika darasa la 8 ashapata skuli anaenda kabla ile elimu haijamtoka katika mawazo. Asante kwa hiyo na-shukuru

kwa kunipa nafasi. Asanteni.

**Com Lethome:** Hassan Ngumbao?

**Ngumbao:** Salaam alaikum……. Mimi ni Hassan Ngumbao na naishi hapa Kaloleni. Kitu muhimu ya kwamba naunga mkono majimbo. Mengi yamezungumzwa mazuri mazuri hakuna hata moja ambalo nimeona kasoro. Hata ikiwa nilikuwa niendelee zaidi ni vigumu. Kasoro kwa serikali yetu, ilibagua kumbagua kwake ni kumbagua muislamu, ambapo sote tu waislamu. Lakini ikawaje ikambuga serikali ilioko hivi sasa? Kulinganisha na nini? Na kisomo. Mwana ukimpeleka nursery, anaambiwa huyu hafai kwenda class hii. Muislamu huyu alisoma Koran - ah - ah. Koran si ya Mwenyezi Mungu? Kitu kile nilitaka haya majimbo yazingatie kama wananchi wetu ambao wanazingatiwa.

Ingine kutoka tupate uhuru huu wetu sisi, kutoka hayati mpaka kuingia nyayo, vitu vya kulimia hazipatikani. Ukiwa huna halafu la mia tano huwezi kupata shamba. Twaomba serikali hii ya majimbo ijaribu kusawazisha zile machini za kulima. Mtu mzima kama mimi nitazama vipi mpaka nipate angalao acre moja? Acre hizi ndogo ni shilingi mia tatu - mzee. Ni nini kufanya hivi ni ma-kampuni ama ni mimi nitayasema hayo ya serikali yetu?

Kupendekeza kwetu twataka vitu virudishwe nyuma. Yaani bei ya vitu iwe nyuma. Ndivyo asiye-jiweza apate kujiweza. Kuna sukari, kuna unga, kuna mahindi yenyewe, kuna huu ukulima zile zote serikali yetu ikiwa italegeza nyuma basi kila mmoja atafanikiwa. Kwa hivyo yangu ni kidogo sina mengi. Asalaam aleikum wahamatulahi wabaratu.

**Com. Lethome**: (Amidst noise) Haya asanteni. Kila mtu atazungumza. (clapping) Chibule wa Tsuma.

**Tsuma**: Waheshimiwa Macommissioner, mabibi na mabwana hamjambo? Basi ikiwa tunachora katiba lazima pia tufikirie mambo ya serikali. Dunia ina serikali nyingi, kila mahali, kila nchi, serikali.

Kazi ya serikali ni nini? Sio kukusanya kodi ama kutawala, bali ni kurahisisha maisha ya raia. Hiyo maanake ni nini? Maanake ni kuondoa umasikini, sio kupunguza umasikini kuondoa umasikini. Na kama unataka kujua kuondoa umaskini ni nini naweza kusomea hapa. Binadamu kile anachotoka ni chakula, nguo, malazi mema, elimu atiba, na kazi ya kufanya, ajione naye ni mtu. Hiyo ndiyo kazi ya serikali. Na kazi ya katiba ni nini? Ni kuweka msingi mzuri wa nchi ili serikali yoyote anayochaguliwa iweze kutimiza wajibu wake. Sasa kwa ufupi, mimi ninaunga mkono wale waliozungumza hapa, naunga mkono sera ya majimbo. Na sababu ni nini? Ni kwamba sela ya majimbo itagawanya ule uwezo wa serikali usiwe mahali pamoja. Kuna bwana mmoja mtaalamu aliyegundua ya kwamba uwezo wa serikali, ni kama ulevi wa pombe. Ukiupa mtu mmoja atalewa na akilewa ataharibu. Ukiuweka pia mahali pamoja kama vile central govt. pekee yake iwe na mambo yote ataharibu. Ile inayotakikana ni ule uwezo ugawanywe vipande viwili ama vitatu. Na sasa sera ya majimbo itagawanya uwezo serikali uwezo wa kuendesha nchi vipande vitatu: Central govt., regional government na local government, ili kama President pale akikuweka kidole namna

hii kuwe na kivuli hapa, ha pale kivuli angalau. Kama ilivyo sasa akikuweka kidole namna hii ana-hit! na hiyo ndio sababu tumehabikiwa na mengi. Kwa hivyo naunga majimbo.

Pili naunga referendum. Yaani bunge lisiruhusiwe hata kidogo kubadilisha katiba. Saa hii sisi tunaingia gharama ya pesa na time yetu kuchora katiba. Halafu eti bunge kwa 65% ibandilishe hiyo katiba? Hata kwa 100% bunge isiruhusiwe kabisa. Ona mara ngapi hii? Sisi ni mataifa mangapi? Taifa moja. Tumechora katiba tayari. Na matifa mengine duniani yanachora katiba mara moja tu. Kwa nini sisi tunachora katiba sasa mara ya pili? Ni kwa sababu ya hii mambo ya bunge hii. Walishikana pale wakabadilisha badirisha. Sasa we could have avoided wasting time. Kwa hivyo ni lazima iingie kwa katiba ya kwamba hakuna mtu anayeweza kubadilisha katiba ila wananchi through referendum (**clappin**g). Na si katiba pekee yake. Mishahara ya wabunge pia ipitishwe through referendum. Kama wanataka kuongezewa pesa inawekwa through referendum.
Sasa Court of Arms, yaani ile emblem ya nchi. Ukiangalia pale katikati kabisa utaona jogoo. Jogoo amewekwa hapo. Ile Court of Arms ni ya soteni hata wale ambao si wa KANU kama mimi. Pia ile ni yetu. Jogoo na shoka lakini ile jogoo, shoka ni sawa, lakini ile jogoo haituitaki pale (**clapping**). Na hata sasa wale simba pia, hizi parties wengine jogoo, wengine ni simba, wengine ni twiga, hatutaki pale. Tunataka ile Court of Arms iwe ya soteni na tujivunie na tuone ni yetu. Kwa hivyo Court of Arms lazima igeuzwe.

**Com. Lethome:** Unapendekeza iwe na nini?

**Tsuma**: Pale, iwe na vitu ambavyo vinaonyesha umoja kama map ya Kenya, Mt. Kenya, Lake Victoria, the sea, ama tutafute kitu ambacho hakina ubaguzi hata mnazi (clapping). Na sio Court of Arms pekee lakini hata pesa zetu picha ilioko kwa pesa isiwe sitting President. Lazima iwe ni kitu ambayo ni ya wote, ni ya kudumu. Kule America wanavyofanya ni kwamba sitting President ama President aliyetoka juzi haingii pale kwa picha wanachukua wa zamani tena ambao wana sifa nzuri.Hapa tunaweka sisi, Mt. Kenya, Lake Victoria, what, what, lakini sio picha ya President ambaye yuko pale. Kwa hivyo ni pesa na Court of Arms.

Hii mambo ya umoja munataka, kuna institutions fulani ambazo hizo lazima zifikirie wote. Kama vile army. The army of the country lazima iwe na waakilishi kutoka kila pembe. Sio ku-recruit watu kutoka one region.

Corruption: Sisi tunalia kwa sababu nchi ni masikini na tulikuwa matajiri lakini sasa tu maskini. Na sasa tunanyimwa pesa na World Bank na IMF kwa sababu hatuna mpango mzuri wa kupambana na corruption. Nataka iwe hivi. Sisi tuna pesa nyingi ambazo zimepotezwa. Goldenberg ilikula pesa lakini kuna report moja naitwa Controller and Auditor General kila mwaka ana-angalia pesa za serikali zilizopatikana vile ambavyo zimegawanywa na Parliament na nafuata zile pesa mpka kule akaone zimetumika namna gani. Halafu anasema hapa PC wa Mombasa, PC wa Pwani, alipewa million tano zitumike kwa mladi fulani kule "Magenyakuro" na hizo pesa zikapotea halafu hiyo inaachwa hivyo. Tayari ijapojulikana ni PC alipokea hizo pesa na akajua maana yake.

Sisi tunataka kwa Katiba hii tuandike ya kwamba tuta recover zile pesa zote tangu tupate uhuru mpaka sasa ziko records za pesa tilizopata **(clapping**). Vile ambavyo vimeporwa na watu na wale wamepora wako wanajulikana in records na walipitia kwa bunge ambako kule bunge kuna kamati moja, kule pale kuna Public Accounts Committee. Lichunguza lakini ikawaacha hawa watu ikawadadisi halafu ikaamua kwamba huyu ni mwizi. Hiyo haitoshi? Yatosha. Tunataka kwa katiba hiyo maanake mimi na simama kwa President na nikifaulu I will recover that money **(laughter**) .

Human Rights ni kwamba watu wamezungumza hapa juu ya mnazi, hapa mazungumo mengi lakini mawili yamesimama. Kwanza majimbo, pili mnazi. Sasa mimi sitaki kuzungumza sana kuhusu mnazi, kwa sababu soteni tanojua tumedhuiumiwa ambaye haelewi faida ya mnazi kwa sisi basi nafikiri na Moi na KANU na serikali, lakini sisi wengine wote tunaelewa (kweli). Basi na sema hivi lazima kwa Katiba kuwe na kitu ambacho kinazuia President ama kiongozi yeyote kufanya kitu against yaani to go against human rights of anybody of raia. This was unfair. Kwa miaka ishirini Moi ametugandamiza hapa kwa kitu ambayo ni wazi ya kwamba yeye ni muongo iwkokwa Itiwe kwa Katiba. Nataka hivyo.

Na sasa watu wanalaumu ukabila. Ukabila ni mbaya. Hatutaki ukabila mimi nasema ukabila si mbaya, mbaya ni wewe. Ukabila ni mpango wa Mungu. Sasa wewe, ukizaliwa na pua kubwa ambayo huitaki utafanya nini? Utaikata? Unaamua ku-deal nayo kama vile mvua ya el nino inakuja na nyumba yako mahali ambapo inaweza kufagiliwa na maji. Unafanya nini? Unatengeneza barabara yale maji. Maji yakija, yanapita pale yanaacha nyumba. Lakini usipochukua hatua za kufaa, the house will be swept. Ninavyosema ni kwamba lazima tu 'tame' ukabira tu 'tame' ethnicity. Na hii majimbo ndiyo njia mzuri ya pekee. Nimemaliza, lakini hapa nina memorandum lakini sio ile ya jana. Asante (clapping)

**Com.Lethome**: Francis Lugho Chai Kama kuna mtu ana mobile azime.

**Chai:** Asanteni Macommissioners. Mimi ni Francis Lugho Chai ni mkaazi wa Chilulu, Jibana. Maoni yangu inagusia kila kipengele katika ile katiba lakini nitagusia zile za maana halafu Macommissioner wakihitaji wanaweza kichukua. Kwanza kabisa ningependa kuunga mkono wasemaji wenzangu kuhusu ule muundo na mufumo wa serikali tunayoitaka, ni majimbo. Lakini haya majimbo wa-Kenya wenzangu naomba radhi nitoe pendekezo langu specifically kuhusu hiyo majimbo. Ningependa tusisahau ya kwamba hiyo majimbo tunayoitaka tusielewe ile majimbo ambayo tunaambiwa na mbaathi ya viongozi, kwa sababu sisi ni wa Kenya kuna majimbo sio majimbo ya wale wa bara kwao. Tafadhalini, tukumbuke kwamba hata tukipata serikali ya majimbo tutakuwa na serikali kuu ambapo Kenya bado itakuwa ni moja sisi tutahitaji kulelwa Pwani kama vile Kenya nzima inavyohitaji rasilmali kuletwa kutoka wafadhili wa ulimwenguni kote. Kwa hivyo hapa ninaomba tupendekeze haswa kwamba majimbo ile tunayotaka yawe hakikisho kwamba serikali kuu inalinda zile haki zakimsingi za raia, haswa umilikaji wa rasilmali ili tata ikiwa tuna majimbo daktari huyu ama mwalimu huyu anaweza kuwa anafanya kazi huko Kisumu, anaweza kujenga hospitali yake huko mwingine akija huku akiweka rasilmali yake hapa pwani itakuwa inaendeleza hapa Pwani. Kwa hivyo ndiyo nasema majimbo hayo ya sisitishe zile haki za kimsingi haswa kulinda kwa mfano umilikaji wa lasilimali.

Pili, nikigusia ile muhimu kabisa ya ile katiba ninakumbuka, naunga mkono msemaji mmoja akisema bunge lidumishe ile haki ya kurekebisha katiba ya 65%. Hapo sasa hivi daktari ni-tatofautiana naye nikizidi kuchangia nasema ile bunge ni waakilishi wetu pale, kwa hivyo tuache ile haki ya kuamend zile sheria sababu sisi zote waKenya hatuwezi kuenda kule lakini sisi pia wananchi tubakishiwe haki fulani. Bunge liwe na uwezo wa kurekebisha sheria lakini sisi raia tuhusishwe wakati kwa mfano ubadilishaji wa sheria hizo unagusia kwa mfano, wanataka kupitisha kura ya kutokuwa na imani na Rais, sisi tuhusishwe, kwa mfano, wanataka kuondoa katiba yote, sisi raia tuhusishwe, urekebishaji huo unataka kugusia zile haki zetu za kimsingi, sisi tuhusishwe. Nikisema hivyo mtakumbuka Wakenya wenzangu kwamba fursa hiyo hatupewi ndiposa mnasoma magazetini kuna public opinion poll zile watu wa magazeti wanakuja wanatuuliza maoni. Fursa hiyo tukipewa itakuwa Wabunge tumewapa ile haki yao ya kurekebisha katiba na sisi pia katika vipengele muhimu watuhusishe.

Tatu, nagusia kuhusu vyama vya kisiasa hapa Kenya. Hivi vyama katika Katiba, kuhusu ule uundaji ile management na jinsi vinavyoendesha shughuli zao haswa specifically sisi Kenya ina makabila mengi. Bila kuchunguza jambo hili kuna hatari ya kwamba tunaweza kuunda vyama vingi hata kiasi cha kwamba kila kabila liwe na chama chake. Hapo tunakuwa hatujengi Kenya moja. Ningeomba kamba Katiba iwe wazi kuhusu idadi ya vyama ili kwa mfano ikiwa Kenya yetu ina watu million thelathini au waKenya million ishirini na nane angalau idadi ya vyama iwe robo ya ile idadi ya Wakenya. Kwa mfano 25% ile idadi ya vyama vile viwe vitakuwa vinaunganisha wa-Kenya sio kila kabila chama chake.

**Com. Lethome:** Mapendekezo yako ni gani?

**Chai**: Napendekeza haswa ile idadi itategemea na idadi ya Wakenya kwa sababu ina badilika. Kwa mfano 25% ya ile

population ambapo ikiwa Kenya tuna million thelathini sasa labda vyama saba au nane vitahakikisha kila Mkenya amepata chama.

Tatu, ni kuhusu bunge. Wakenya wenzangu ninaomba tufahamu ya kwamba sisi raia uwezo wetu mkubwa ni bunge, tuna-tuma wakiilishi wanaenda kule kutuwakilisha. Kwa hivyo shida yetu ambao inaleta malalamishi tuna yaoitaoa hivi leo ni kwamba bunge letu halina uwezo ule ambayo unastahili. Hapa haswa napendekeza kwa hivyo katika ule muundo wa serikali uwe na ugawanaji wa mamlaka kati ya zile sehemu tatu za serikali. Usiwe uwezo una pande mmoja, kwa upande wa Rais, sababu hilo tatizo ndilo linaletga kwamba Rais ni dictator lakini nataka bunge liwe na uwezo zaidi ya vile vyombo vitatu vile viwili vimebaki kwa mfano urais na ile sehemu nyingine. Pia hapo ningependa, kuhusu ubunge, tunalalamika hapo tukichagua Mbunge mara tunalia; Mbunge hatumuoni ana kazi nyingi haya, sababu ni nini?

Ninapendekeza ya kwamba hiyo kazi ya Ubunge iwe full time. Iwe ndiyo kazi yake muhimu kule. Huku mashinani atuachie hayo mambo mengine. Isiwe kwamba Mbunge ni Chairman wa KANU Kilifi District, Mbunge ni Chairman wa KANU Kaloleni, Mbunge ni Chairman, treasurer mpaka katika sub-locational level. Kule pia ni Assistant Minister. Hiyo ndiyo inasababisha wakati tunahitaji Mbunge wetu tunamfukuza tunaambiwa amehudhuria mkutano wa KANU, anahudhuria hivi lakini iwe kazi ya ubunge ndiyo ya muhimu full time. Ikiweza tunalilia separation of power kugawanya mamlaka kwa mfano kule serikalini Bunge, urais na mahakama vigawanye serikali hata huku pia mamlaka haya tuyagawanye. Kwa nini mamlaka yote tunamwachia yule mbunge halafu leo tunakuja kulia Mbunge hapatikani? Ni kwa sababu ana kazi nyingi. Asante.

Pia hapo katika ubunge ningependa kugusia wale wabunge wanaoteuliwa Katiba iondoe hiyo kwa sababu limekuwa likitumiwa vibaya. Ikiwa kuna wabunge wowote wanaoweza kuteliwa wawe kwa mfano viti vya wale walemavu lakini wale wote wanaojiweza wapigiwe kura.

Mwisho, kuhusu urais masharti ya Rais awe specifically nimependekeza kwamba ule muda wa kipindi cha maisha ya bunge kiwe miaka sita badala ya tano. Miaka sita hiyo ni kwa sababu ninapendekeza kwamba yule Rais asiwe wa maisha awe na vipindi viwili tu vya miaka sita. Kwa hivyo akiwa amepunguziwa tumempa tu vipindi viwili asiendelee basi angalau tumeongeza mwaka mmoja to be fair. Miaka sita imutoshe halafu Council Chairman wa County Council pia tuwape miaka mitatu.

Kipengele kingine kinachotukera sisi wananchi ni ile Provincial Administration - utawala wa mkoa. Sisi tunalia kwa sababu ya kazi wanaotenda hawa ni kwa sababu kipengele hiki ni urithi tuliorithi kutoka serikali ya ukoloni. Lakini wengi wamependekeza uondolewe kabisa. Lakini mimi napendekeza kwamba kilicho kibaya baadala ya kutupwa kurekebishwa. Utawala huu wa mikoa nitafanana na maoni ya wenzangu kwamba badala ya kuondolewa kabisa kutoka PC, DC hardi DO wale ni watu ambao kazi hii mara nyingi huisomea kwa hivyo wateuliwe na serikali. Lakini hawa wetu huku mashinani, chief na naibu wake tupewe fursa sisi tuwapigie kura. The chief authority act, the preservation of public order act zile sheria zao ndizo zina wapahuu uwezo wa kutuumiza uondolewe katika Katiba. Kufunga, ninasema kwamba hawa watu je kazi yao itakuwa nini sasa? Ningependa

kusema kwamba hawa wawe ma-coordinator tu wa maendeleo katika sehemu zao lakini ku-coordinate maendeleo wakishirikiana na serikali na NGO lakini kazi ya mambo ya usalama ya achiwe vyombo vya usalama kama polisi. Asante.

**Com. Lethome:** Kuna mama anaitwa Fatma Abedi, Dr. Munga

**Fatma:** Basi kwa jina mimi ni Fatma Abedi, hamujambo? Mimi ni member wa Kaloleni Community Development Fund. Mada haki za makundi na usawawajinsia. Kuna muhimu mkubwa sana wa kufikiria masilahi na haki za akina mama kupitia njia sahihi yenye muelekeo bora. Mkutano wa Beijing ulipendekeza hatua kali ya kutaka haki sawa za kijinsia kwa akina mama katika jamii. Kwa bahati mbaya mapendekezo hayo haya kuadhiki vizuri, kinyume na matarajio katika jumuia ya kimataifa………. (not clear). Kwa upande wa akina baba utafiti unaonyesha wazi kwamba pendekezo la mkutano wa Beijing la kutaka haki sawa kwa akina mama na akina baba zimezuazogo kubwa na sana kuwa swala lisilo-kubalika hata kwa akina baba. Kutokana ha hali hii, sisi wanachama wa Kaloleni Community Development Fund tunaona mwelekeo bora ungewezakuleta uelewano ambao ungesababisha makubaliano kati ya akina baba na akina mama.

Pendekezo langu ningependa sisi akina mama tupewe haki sawa na akina baba. Kwa mfano kama sisi akina mama tukitaka passport tukifika immigration tunaulizwa una bwana? Unanyimwa passport juu huna bwana. Au ukitaka plot unaulizwa una bwana. Huwezi mama wewe kupata plot kwa sababu huna bwana. Basi ningependekeza katiba itilie maanane hili neno akina mama waweze kupewa plot bila kuhojiwa una bwana au upewe passport bila kuhojiwa una bwana. Pia watoto wetu wakitaka kitambulisho aende na kitambulisho cha mama aulizwa na ya baba? Utakuta sisi akina mama baba wanatukimbia kwa sababu ya hali ya uchumi wa Kenya yetu hii. Akilemewa zaidi anaphora. Unabaki na watoto unateseka. Sasa mtoto akifika wakati wa kuchukua kitambulisho utaona unapata shinda kwa kuhojiwa ile kitambulisho cha baba. Mama anatatizika kutafuta baba alipohumpati. Sina zaidi kwa wakati umekuwa mwingi, asanteni.

**Com. Lethome**: Je mama hao baba waliwatoroka ungependekeza wachukuliwe hatua gani na sheria?

**Fatma**: Mimi ningependa hao akina baba wanatoroka sisi wamama wachuliwa hatua ya kutafutwa na kuadhibiwa ki sheria asanteni.

**Com. Lethome**: Dr. Mwinga Chokwe.

**Dr. Mwinga**: Macommissioners pamoja na wananchi hamjambo. Haya basi na-shukuru kwa sababu ya kunipatia nafasi ya pili kuzungumza. Kweli jana nilizungumza Mariakani, lakini wale ni watu wengine na hapa ni pahali pengine na ni vizuri umetumia busara kubwa kuuliza wananchi kama wanataka nizungumea au namna gani. Kwa hivyo na washukuru sana wananchi. Pili, nimechelewa hapa si maksudi, nilikuwa natamani nije hapa mapema lakini leo nilikuwa kortini na nilikuwa either nije hapa au niende Shimo la Tewa. Kwa hivyo mkutano huu kwangu ulikuwa muhimu sana kwa sababu na zungumzia haki za kibanadam

ambazo zimetajwa hapa. Na kisa na sababu ya mimi kuwa kotini ni kwa sababu nilitetea kuvunjwa vibanda hapa na County Council ya Kilifi. Kutetea tu, sio kuvunja sio kupiga yaani ilikuwa haki yangu kutetea lakini hiyo kutetea kulingana na katiba ya sasa ina kuingiza ndani, ushikwe na DO hata si Polisi akupeleke ndani na utalala Shimo la Tewa. Kwa hivyo ndio sababu nimefanya bidii baada ya hiyo kesi kutupiliwa mbali nikasema lazima nije hapa niwajulishe hapa vizuri.

Basi mimi ningetaka kusema hivi. Katiba ambayo tuko nayo ina-tusumbua kwa sababu ni katiba ya kikoloni. Ilitengenezwa na mkoloni kulingana na desturi za kikoloni za uingereza akiwa amemueka Bwana PC, na Bwana DC na walikuwa wanaitwa BWANA PC, DO ambao wote walikuwa ni wazungu na hakuna Muafrika alikuwa akipata kile cheo. Mkoloni alipo ondoka Muafrika akaingia lakini ukoloni haukuondoka ikawa sasa mkoloni mweupe ameondoka ameingia mkoloni mweusi. Mimi na recommend tusifanye reconditioning ya katiba lakini tuunde katiba mpya katiba ya Kiafrika, katiba ambayo ina heshimu mila zetu vikiwa pamoja na yale mambo yametajwa hapa kama mnazi iko katika mila ya area hii. Mnazi haupikwi, it's not a brew it's a wine kutoka juu Mungu anapeana. Hiyo ni mila lakini mila ya kikoloni inasema mnazi is a brew. Si kumi kumi, nataka kukuambia mnazi ni fresh kabisa. Kwa hivyo Katiba hii yetu ikiwa ni Katiba inaangalia asili yetu itatuwezesha kuangalia kila jimbo maanake mimi na simamia ile majimbo ile tunaita economic majimbo. Itasimamia rasilmali ya pale mahali halafu ita heshimu desturi za wale watu pale na itakuwa yale mambo wanayofanya si kukosa sheria.

Pili, ili kuondoa kabisa ukoloni ambayo uko Kenya ikiwa bado tutakuwa na Bwana DC ambaye anavaa kofia nyeusi na nini, itakuwa akili yetu siku zote tutakuwa bado tuna- mwogopa, anatutisha, na Bw. Chifu ambaye aliwekwa na Bw. DC kusudi kushtaki watu wote ambao wana-kosea serikali. Kwa hivyo Katiba hii mpya lazima iondoe kabisa mambo ya DC, PC, DO, Chief kusiwe na chief kabisa. Kutakuwa na management authority na hata tutaondoa local authority maanake local authority ilivyo tengenezwa sasa. Kuna central government na kuna local government. Unakuta hii local government ndio inataka ishughulikie masilahi yetu kabisa. Hivi ilivyo sasa local authority nyingi sasa katika Kenya ni zile zinapora mali na kazi haionekani kazi gani inafanyika. Kwa hivyo kukiwa na management board, management authority kutakuwa na professionals ambao wanafanya kazi hapo na ndiyo watakuwa wakipangilia mipango yetu kama ya hapa Kaloleni kujua mipango yetu inaenda kivipi kusudi kumaliza umasikini.

Halafu, katika upande wa Polisi tungependekeza kwanza wapelekwe kwa elimu ya gumbaro kwa sababu wana kusumba ya Katiba ya kikoloni ya hiyo Katiba ya kikoloni ilisema kama wewe ni Muafrika wewe ni mshtakiwa unless proved otherwise. Na hata leo Polisi ana nguvu ya kukushika arbitrary arrest, upelekwe ndani na watu wengi wanashikwa wanafungwa kwa sababu hakutoa hongo. Polisi lazima wafundishwe kama wale wa Britain ambao wakikuona wewe ni mlevi kule Britain umeanguka njiani wao Polisi hukuinua wakakuweka kwa gari wakakupeleka kwa bibi yako. Lakini hapa ukishikwa mlevi unapelekwa cell na cell hutatoka huko mpka utoe pesa. Kwa hivyo tukibadilisha mambo ya polisi tutaona tume-inuke kabisa.

Human rights nyingine ni freedom of association. Katika katiba hii kukutana lazima upate cheti kutoka kwa DO, kwa chifu kutoka kwa nani na wao wanaweze kukushika mara moja kulingana na vile katiba iko. Na sisi tunajua Waafrika saa yote

wanapenda kukutana, saa yote wana sherehe zao saa yote kuna matanga, mazishi n.k. Basi Katiba hiyo ndio unaona wakati mwingi Macommissioners mukija hapa law courts utakuta watu wengi wameshikwa kwa sababu walikuwa drunk and disordely.

Halafu, kuna mambo ya President. President mpaka awekwe chini ya sheria kwa sababu president sasa yuko juu ya sheria na shida ambayo tuko nayo Kenya wakati huu ni shida ya kujitafutia wenyewe. Juzi tu katika parliament kulitangazwa kuwa wakubwa wetu wa serikali, politicians, wameiba zaidi ya shillingi billion mia tano. Hiyo ilitajwa na Bw. Nyachae katika parliament. Billion 500 inaweza kuendesha wizara ya afya kwa miaka hamsini. Na ni pesa ziko mifukoni mwa watu wa Kenya wameiba. Hata leo tukizungumza habari ya umasikini, IMF mimi naona tunajidanganya maanake hizo pesa tuko nazo, na tunajua wale wameiba na katiba mpya lazima ishurutize wale wameiba pesa za uma. Zirusishwe, na zikirudishwa tunahakika kuwa elimu itakuwa ya bure mpaka university sio mpaka Std. 8 maaanake mtoto wa Std. 8 atafanya kazi gani?

Matibabu yatakuwa ni ya bure kabisa, kazi zitapatikana, infrastructure, kama hapa kwetu Kaloleni hatujui lami, lami iko nusu kipande maanake ufisadi uliokuja ulikula hizi pesa za kuenda mpaka Mariakani na hata juzi tu ufisadi mwingine tumona million mia mbili zimetengeneza barabara na barabara haionekani iko wapi. Kwa hivyo hizi pesa tunazozitafuta tuko nazo mifukoni tayari. Katiba hii mpya ihakikishe imerundisha hii pesa na IMF na World Bank, sisi hatutawaona tena, tutakuwa tukikutanatu kwa mikutano lakini rasilmali iko Kenya inatosha sisi kutupatia mambo yetu yote. Na katika kumalizia tulisema mambo ya infrastructure na kuna mmoja ametaja hapa serikali lazima itengeneze mambo ya shule.

Shule zetu hapa especially Coast na Nyanza maanake Nyanza ndio wanaogoza kwa umasikini na sisi tunawafuatilizia hapo mbele kidogo katika 62% watu ambao tunapata chini ya dollar moja kwa siku. Hizi shule katika katiba mpya zipewe umuhimu zaidi zitengenezwe kulingana na hali ya kimataifa. Ukiangalia katika Rift Valley sasa ilivyo wana university karibu tatu nne, jimbo moja pekee yake na Pwani hatuna hata moja. Kwa hivyo mimi nasema katika katiba hii mpya hizi jimbo ziko nyuma kwa sasa na sisemi Coast pekee yake, nimetaja Coast, Nyanza, Eastern na North-Eastern zitengewe pesa ambazo kwangu mimi ziliibwa kutoka jimbo hili zirundishwe zitengenezewe infrastructure kusudi standard yetu iweze kufika kiwango ambacho hata tukipata kazi kubwa kama hizi za hawa Macommissioners - unaona hawa Macommissioners. si ni watu wakubwa? Si wamesoma sana? Kuna wanyika (not clear) wangapi hapa? Kwa sababu hamjasoma. Kwa hivyo lazima tujiulize kwa nini hizi kazi kubwa sisi hatuzipati. Kwa nini huyu DO hawezi kuwa ni 'Mnyika' wa hapa? Kwa nini DC hawezi kuwa? Kwa sababu masoma yetu pia hafifu. Asanteni sana. (**clapping)**

**Com. Lethome**: Ngumbao Kifungu/ Nadiso Charo B. Hayuko. Erastus Kubo. Pato Bakari kuja hapa.

**Bakari**: Kwa jina naitwa Pato Bakari. Kuongeza kwangu naunga mkono msemaji mmoja aliyengea kuhusu rathi wakiwa wasichana kwao walikozaliwa. Wanawake sisi age zile za wazee wetu wengi hatukusomeshwa na wazee. Ilikuwa ni kupatiwa tu mzee yeyote, baba anapata ngombe, anaozesha vijana; vijana hao hao sisi baba akiwa amekufa ukisema kule pengine

mambo yameharibika ukirudi pale, ndugu yako yule ana vijana wake anakwambia shangazi hapa si kwako usijenge ukakae hapa. Kwa hivyo hiyo naomba upande wa Katiba ya sasa watoto wote, wa kike na wa kiume, wawekwe hali ya sawa. Ndugu akipata plot kama acre sita mimi msichana hata kama ni acre moja au acre mbili pia nipate. Hiyo ndiyo ilikuwa ni kulia kwangu. Akina dada tunanyanyaswa kwa sababu ya unafiki wa wazee wetu.

**Com. Lethome:** Asante, na je wale ambao wamewekewa urithi na dini zao wamepangiwa katika dini zao na sheria hiyo imetambuliwa na Katiba.

**Pato:** Na wengi hawaifuati.

**Com. Lethome:** Sasa wataka tufanye nini?

**Pato**: Twataka ingizwe kwa Katiba hii ya sasa.

**Com. Lethome:** Iko katika Katiba.

**Pato:** Basi twataka tufafanuliwe vile tutafuata huo urathi wa madada kwa ndugu zetu.

**Com. Lethome**: Asante, Geoffrey Mukungi afuatwe na Gideon……

**Geoffrey Mukungi:** Waheshimiwa Macommissioners wetu, wananchi, anayezungumza ni Geoffrey Mukungi kwa niaba yangu na familia yangu na jamii yangu. Mimi nimetoka Rabai Location. Nitagusia Katiba haraka haraka maana wakati naona umeenda. Habari ya Preamble/Utangulizi katika Katiba. Ni kweli Katiba yetu ya sasa haijatambulisha ina- wakilisha akina nani na lazima kuwe na maandishi/kifungu ambacho Katiba yenyewe inajitambulisha ni yana ni kutoka wapi. Mwana-Kenya ana hisi ya kutosha kwanza kutoka ukoloni, sisi tuko majimbo mengi, sisi tuko makabila mengi, sisi tuko mila tofauti tofauti.

**Com. Lethome**: Pendekeza mzee.

**Mukungi**: Katiba ieleze ina-mwakilisha nani Kenya. Iwakilishe watu wa Kenya wote na ijitambulishe inasimamia watu wa Kenya ambao wametoka katika ukoloni wa Kiingereza na wakajitawala wenyewe kupitia hata vita vya Mau Mau.

Kitu ambacho tumekipata katika Kenya ni kwamba tumetoka katika ukoloni na tuna historia ambayo tumejiwekea wenyewe. Vitu hivi tunataka viongezwe katika Katiba hata katika mwendo wetu na kisiasa. Peace, love na unity iweko katika Katiba na hata ikiwezekana kile ambacho kimetufanya tufaulu katika mirandi mingi ambao ni motto wa harambee iwe katika Katiba.

Supremacy of the Constitution. Tunaomba Katiba ieleze wazi kwamba ndiyo chombo muhimu katika Kenya na hakuna sheria yoyote chini yake ambayo itapita Katiba. Wana chama kama ilivyo katika Katiba na zile za mbele ni kwamba watu wote waliokuwa hapa siku ya uhuru tarehe 31/12/1963 wote ni wananchi wa Kenya na wale wanaozaliwa hapa ambao wako katika birth registry ya Kenya hii wote wapate uwanachama. Uraia wa juu juu usikubaliwe katika Kenya. Itakuwa watu waliozaliwa. Mwana-Kenya ambaye ameoa au ameolewa pia ana haki ya kuchukua wanawe na hata mumewe au mkewe kuwa raia wa nchi hii.

Defense: Security. Kusimamia hali ya usalama katika nchi. Hii iko sawa na iendelezwe. Lakini sasa, kitu kimoja ni kwamba, kama ni army, tunajua army inatetea nchi nzima, pia iwe katika national government na vyeo fulani katika polisi, labda CID, Special Branch, iwe isimamiwe na serikali ya kuu. Lakini kila jimbo ambazo tunaenda katika serikali ya majimbo ziwe na nafasi, ziwe na ruhusa ya kufundisha askari wake na kuandika askari wake haswa kwa upande wa traffic, upande wa kusimamia mikutano, upande wa kutuma patrol hapa na pale, wawe ni watu wa hapa ambao wanajua pale mahali walipo na waandikwe kutoka hapa. Quota tunataka system katika national level kwa upande wa CID special branch zile kazi kubwa na national army.

Political Parties: Vyama vya kisiasa. Tukiingia katika Katiba yetu, tukiingia katika utawala wa kimajimbo, vyama vya kisiasa vingine vitakufa maanake havina maana na havitatoka kwenda mahali pengine. Ikiwa jimbo lile watavikubalia vitaendelea au vikifa ni national death. Lakini kile mwananchi ana haki ya kupleka makaratasi yake ya kikatimba kusajiliwa katika Serikali. Kwa political parties hakuna haja ya kufunga hiyo.

Structure and System of Government: Sisi tunakubali kwamba tuwe na Rais katika serikali kuu na serikali ya majimbo ambako tutakuwa na magovernor au watapewa jina lolote. Katika kila jimbo kutakuwa na governor, kutakuwa na magovernor wadogo, kutakuwa na system ya serikali ambayo itatuongoza katika kila jimbo kulingana na mahitaji ya nchi ile au hata kama ni ecological system, yes, tuwe sisi tunajitawala au tunatawaliwa kulingana na mwongozo wa ki-jimbo. Kwa sababu kama tulivyosema mila na desturi viko tofauti na ni mambo mengi, natural resources, vitu ambavyo vitatuletea pesa, revenue, hata ukulima ziko tofauti katika kila jimbo. Basi hivi vitakuja kupangiwa katika jimbo lile, njia ambazo tutaziendea mpaka tukafikie kutosheleka nazo. Kwa hivyo serikali iliyo bora ni ya majimbo.

Tunapokuja habari ya ma - MPs, habari ya local councillors, habari ya wazee wale wale, hii inakuja katika Katiba ile ilitoka sitini na tatu (1963) ya majimbo ilikuwa ina kila kitu ambacho kilikuwa kimewekwa. Hii ni kuonyesha kwamba Regional Assembly kazi zake ni zipi na chini ya Regional Assembly kuna nani. Hii yote tukileta majimbo hapa inabidi kuondoa kabisa administrative system kama tulivyonayo sasa. Hakuna PC, hakuna DC, hakuna Chief, hakuna Sub-chief, hakuna mtu yeyote. Hiyo inaondoka system kabisa kabisa. Badala yake tukiwa na Governor mahali ya PC tunateremka chini tutakuwa na bunge la kijimbo na mamlaka itagawanyika hivyo. Kutakuwa hakuna mtu wa kunung'unika ati Rais ana mamlaka kubwa, Rais ana power nyingi, Rais ana uwezo mwingi kupita kiasi. Maanake itavunjika na tutakuja kugawanya mamlaka yale sawa sawa.

Lakini tunajua tu wazi huwezi kuwa kiongozi, huwezi kupata mamlaka, bila uwezo. Uwezo ni lazima. Utagawanyika Central Government lakini hata sisi ni lazima tutakuwa na uwezo wa kumfanya mtawala,wa kumfanya mtu anayeendesha mambo awe na uwezo wa kuyaendesha kwa faida yetu sisi.

Judiciary: Habari ya mahakama tafadhali sana iwekwe katika Katiba kwamba kila watu ambao wanajitawala wenyewe watajihukumu wenyewe. Vile vikorti vidogo vivyokuwa hapo zamani vikiitwa African Court virudi maanake chief atakuwa hayuko kusikiliza kesi za watu waliogobana. Kwa hivyo lazima kuwe na ka-court ka aina fulani hapa ambako katakuwa formed na wenyewe na kataendesha hii. Electoral system sawa sawa, local government watu wamesema local Councillor lazima wasome hekima si elimu na elimu sio hekima. Tuna wazee ambao wana miji mikubwa mtu ana wake kumi na mji mkubwa, na ngombe; ana kila kitu na mji ule umenyamaza na kwa sasa mmoja aliyesoma sana nyumba yake imemshinda kutawala. (clapping). Kwa hivyo tukisema elimu na hekima tugawanye. Sisi tunataka ma-councillors wale ambao hawakusoma wanajua shida za wenyewe. Tunachukua mtoto wa university ambaye hata hajui alisomeshwa na nini anawekwa hapo eti ni Councillor na anajua atapita na wapi.

Basic Rights: Basic rights tafadhali iwe ni kitu ambacho nataka kuzungumza sasa. Mimi ni mzee hapa nilipo, hata kama si hivyo lakini ni mzee kidogo. Tulipata uhuru miaka thelathini na kitu iliyopita na ni sawa kama mimi haki zangu za kibinadamu serikali ina- ni-guarantee. Lakini ardhi ninayoikaa mimi ina milikiwa na County Council si mimi. Uhuru wangu uko wapi? (clapping)

Mimi nikifa nagawanyia wanangu ardhi ya County Council kesho asubuhi wanaambiwa ondokeni hapa hii si kwenu. Nyumba yenu mnalipwa, ni nyumba pekee yake, ardhi inaenda. Katiba i-guarantee wananchi shamba. Si kwamba kila mtu apate shamba la bure si kwamba kila mtu apate shamba ambalo hatukulimia jasho, lakini mwananchi awe na haki ya kupimiwa ardhi anayokaa ili apate cheti chake cha kuendelea mbele. Hakuna haja ya mimi kwenda kortini kurithisha wanangu kitu ambacho sina karatasi yake haiwezekani.

Settlement schemes: Naona settlement schemes kwetu Kilifi ambazo zimeletwa watu tu kila mahali na wale wenyeji wa pale wanabaki hawana ardhi. Uhuru walio nao ni upi na haki yao ya kibinafsi ni ipi? Wamesimamia nini? Mali ya uma na hata mali ya watu ihakikishiwe usimamizi mwema katika katiba. Katiba lazima itambue mahitaji wa mwananchi na kuyaondoa. Elimu ya bure lakini iweko. Hatusemi eti hospitali iwe ya bure; twasema iweko. Hatusemi maji yawe ya bure, ah ah yawepo. Hatusemi umeme uwe wa bure la. Uwepo. Hivi vitu kama vipo, tutatafuta njia ya kuvipitia. Lakini hata tukisema elimu ya bure na skuli zenywe hatuna, tunasema nini? Tukisema tupate maji ya bure na mifereji hakuna twasema nini? Tunaangukia milaa. Serikali, Katiba ituhakikishie kwamba kila mwananchi atakuwa na uwezo wa kupata hospitali, wa kupata elimu, wa kupata mambo kama hayo. Asanteni kwa kunisikiliza (clapping).

**Com. Lethome**: Tusikize mzee mwingine, Gideon Lwambi kwako jitamke vizuri wewe mwenyewe.

**Lwambi:** Basi ndugu niliyeko hapa kwa jina naitwa Gideon Lwambi, mimi ni Mrabai. Nafikiria ushanijua vizuri?

**Com. Lethome**: Tayari. Asante.

**Lwambi**: Sisi tuko hapa kwa kuchangia Katiba ya majimbo Katiba ya majimbo ni ya wananchi. Katiba iliyokuwako ilikuwa si yetu hautijui. Na kwa hakika tulikuwa hatuijui ilikuwa ikibuniwa na Wabunge. Hapo sawa. Hivi sasa tunavyokaa kutoka juzi tunazunguka na nyinyi kwa sababu ya katiba tupate kuielewa na sasa sehemu hii itakuwa ni ya mwisho lakini tumenjua kimoja chako. Majimbo tulikuwa tunayangojea ilikwenda ikachukuliwa Lancaster House na marehemu Bw. Ngala. Ilipofika hapa majimbo haya - kufanya kazi kabisa. Ikakatazwa. Makatazo hatu-kuelewa ni sababu ya nini? Lakini tulikuwa wachache, sasa tushakuwa wengi na majimbo yamefufuka.

Katiba ni kwamba isiwe ya zamani, aliye-kuweko hapa amesema habari ya mashamba. Ni kweli tumepimiwa mashamba kitambo na wengine hawajapimiwa mashamba lakini seikali iliyoko inaogopa mtu mweupe, mtu mweusi haigopi. Mtu mweupe yeyote alioko hapa ana title deed lakini mtu mweusi hana. Huko bara kuna title deed hata kama una maskani kidogo tu kama hapa atu upande za nyumba una title deed, lakini hapa kwetu hakuna mtu mweupe anayo.

Pendekezo langu ni kwamba sisi tunataka tupimiwe mashamba na tupewe vyeti vyetu vya kumiliki mashamba yetu. Huo ndio utaondoa umasikini kwa sababu kuna kitu ambacho kimeanza kuletwa cha mkopo na mimi nikienda nikakopa kwe kile cheti changu. Nikiwa sina cheti basi nitakuwa maskini wa maisha. Vitoto vingi sana tunashindwa kuvipeleka skuli, skuli zimetajwa hapa, kwa sababu hatuna pesa. Na pesa ziko. Zinakuja hapa na zinarudi na hazi-chukuliwi na mwananchi wa hapa. Anayekopa ni DC, anayekopa ni DO, anayekopa ni PC. Kawaida ya mwananchi hapewi hata peni na hiyo ni Katiba iliyotungwa bunge. Mbunge anaingia bunge leo kesho kutwa ni millionaire kwa sababu anakwenda kupora sisi raia tuliompeleka kule.

Ni kwa sababu kwamba, pendekezo ni kwamba, Mbunge asiwe na sauti, sauti iwe kwa raia (**clapping**). Na Rais anaambiwa ana sauti kubwa sana katika kule mamlaka yake ni makubwa. Lakini amefanya kupewa, hakujibandika. Na amepewa na hawa wabunge kwa kubembeleza hajui kwamba kura zatoka huku, yeye anabembeleza Rais ati asitolewe. Ikifika miaka mitano atolewa, wewe ushabembeleza kule.

Pendekezo juu ya Rais ni kwamba asiwe na mamlaka, mamlaka yatoke huku chini kwetu. Nimesikia kwa habari ya elimu. Elimu, Chief awe ni wa Form 4. Ataandika nini kule? Kitu ambacho atakwenda andika ni nini? (laughter) Tuna ma-Chief ambao hawakusoma hata "a" na wame-retire wakiwa ni hivi hivi na wame-retire bila kosa. Na wale machief ambao kwamba ni Form 4, wengine walikuwa ni Form 6 zamani sasa form 6 hakuna, wana makosa chungu nzima.

**Com. Lethome**: Sasa unapendekeza machief wawe na elimu gani?

**Lwambi:** Ningependekeza machief hata kama Std. 8 kwa sababu yeye haendi mbali yuko pale pale katika location yake.

**Com. Lethome**: Na Councillor awe na elimu gani?

**Lwambi:** Councillor vile vile hata kama ni Std 4 lakini ana-eleweka (laughter). Kwa sababu heshima haiendi kwa elimu. Heshima inaenda kwa wewe mwenyewe pale kwenu uko vipi. Katika location yako, sub-location yako, uko vipi. Lakini haiendi kwa elimu. Wale wanaotoka ma-university tunawaona vilabu hawafui, hawaogi, suruli ziko tele mikonjo. Na yule ambaye kwamba hakusoma ni safi ana ngombe, ana mbuzi, ana watu, kwake nyumbani ana mfereji wa maji na hakusoma. Wa university ana aibu huwezi kwenda naye. Lakini poleni nyinyi nyote mumesoma mumekwenda university. Hatuwatukani (**clapping**).

Pendekezo moja limezungumzwa lakini halikuguswa, mimi ninaligusa. Serikali iliyoko, serikali, Katiba iliyoko inaonea wazee walioandikwa kazi kitambo wanenda retire, pesa zake za retire mpaka zipite bunge zikakatwe. Ninapendekeza kuwe na tume ya kutembelea katika makampuni wale wanao-retire tume yao iweko na wawe wana pewa pesa zao kikamilifu kuliko kwenda bunge.

Kuna kitu kimoja sisi wazee tunaenda retire. Kuna mti wa mnazi ni wetu. Kuna mkahawa ni wetu kwa sababu mnazi waliwa na mkahawa waliwa. Majani ya chai yaliwa, lakini kuna mti uitwao bangi. Bangi tunataka hii serikali ya katiba mpya iwe na power ya kufunga hao watu, kwa sababu hatusemi ni watoto pekee yake. Hata sisi wazee, hata nyinyi akina mama, mtu hujificha akavuta bangi, ukija ukimuona ile hali sio tena. Kwa hivyo tunataka kuwe na mahakama ya bangi (**laughter**) makubwa sana zaidi, zaidi hiyo bangi pekee yake. Kwa sababu tuna hatari nikiwa na shillingi zangu elfu moja ndani ya nyumba na vitoto hivi basi mpaka nifunge kisha nichukuwe magongo niwekelee tena nilale nikojoe nyumbani mkebeni nikamwage kwa sababu nachunga elfu moja ninayo. Na hapo hatari kwa hivyo nataka hii katiba mpya ya majimbo iwe na security kubwa ya kutosha kulinda mti wa bangi. Nikishimba na bangi nije nikaadhibiwe hata kama ni miaka ishirini hata kama ni kunyogwa, ninyongwe. **(laughter**) Asanteni. Ni hiyo tu.

**Com. Lethome**: Asante sana. Sasa naita huyu Bwana James Ottondosson.

**Ottondosson**: Asante sana Hon. Commissioners na viongozi wenzangu. Mimi naona ajabu sana na singeenda nyumbani bila kusema. Jina ni James Ottondosson, ndio secretary wa Mariakani Business Enterprise small scale na pia Chamber of Commerce member Kilifi. Kitu ya kwanza ningependekeza niseme hapa ni ardhi. Mimi mwenyewe sio Miji Kenda lakini nimekuwa kama mtoto wenu. Nimechaguliwa sehemu nyingi sana.

Land and property rights, absentee landlords katiba mpya iangalie sana. Sio mtu anakaa urala na land anayo, a mass of land, karibu acre nyingi. Iangaliwe vizuri kwa katiba mpya ya majimbo mimi ninaunga majimbo mkono. Federal government sababu yake federal government potential resources zinapatikana within that jimbo. Nyingi zinabaki hapa. Na watoto wetu ambao wamesoma kwa agriculture ndio wanachangia mambo ya food policy ili umasikini upungue. Umasikini umezidi kwa watoto wetu sisi tumesomesha hapa. Serikali wachukue maanani waangalie watoto ikiwa ni mtu wa agriculture. Mtu anapanda mahindi ishirini kwa shimo moja anakwambia ni sawa. Kwa vile anapata pesa. Huyu anapata hasara. Hiyo wafundishe watu njia ya kupata elimu.

Mambo ya ardhi. Tangu lini tunakuwa kwa state land na trust land mpaka sasa mtu Mijikenda anaitwa anakaa kwa state land na trust land? Waangalie. All over Kenya waangalie hiyo walekebishe. Nimependekeza waangalie hiyo wale wenye land ambao wanakaa kwa land ambayo haina title deed wapewe.

Electoral system process. Votes. Unasikia mambo mengi yanatokea kwamba kura imeibiwa njiani. Tunataka, tunaomba ama tumependekeza wale presiding oficer wanakaa kwa kituo apewe mamlaka kura ihesabiwe hapo hapo na report ndio ikuje kwa returning officer kwa division. Ikiwa mbele ya agents wake. Haitakuwa mambo ya kura imeibiwa njiani. hiyo nafikiri itapoa sisi.

Ballot Boxes: Ballot Boxes iwe transparent ambapo unaona kitu iliyo ndani ya box. Hiyo ningependekeza Commissioners waangalie hii boxes iwe transparent ndio kila mtu aridhike. Na kura iwe secret ballot.

Political parties: Maoni yangu, pendekezo yangu nimesema political parties ziwe tatu au nne tu. Kwa maana ikiwa nyingi mtu anakuwa na watoto wake na bibi yake kwa political party haina maana inazidi kuleta ukabila.

Ya mwisho upande wa uchaguzi wa Councillors. Councillors mapendekezo yangu au ninapendekeza ma-Councillors ambao wako na sisi kwa grassroot hata akipata std. 7 na yuko na talent mzuri hata Std. 8, Form 4, pia waingie wapambane, mimi nimeunga mkono. Lakini MP ningependekeza awe graduate na president awe graduate na president awe graduate of between 40 to 60 years of sound mind. A graduate, a degree as well hana criminal record, also a Kenyan and a person of great integrity. A married person. Kama ni mama awe na bwana, na kama ni bwana awe na bibi. Nafikiri niki save time hizo ndizo nilikuwa nazo kwa maoni yangu lakini ningeongeza ingine lakini mnasema time is over. Thank you very much.

**Rebman Kazungu.** Nashukuru sana kwa kupata kipindi hiki kuelezea mambo ya majimbo. Jambo ambalo napenda ni kwamba majimbo yetu ifanywe na sisi wa pwani kama ni kuchukuliwa vizuri tungekuwa wa kwanza kwa utajiri. Lakini Katiba yetu tuliyo nayo ndio kuna msongamano ambao si mzuri. Kwa kusema machache, mimi sitaendelea zaidi lakini ni kukumbuka ufisadi unaofanywa katika Kenya. Baada ya kupata majimbo kama ninavyopendekeza ni kwamba tuwe wale viongozi watakaokuwa wanatuongoza wasimamie vizuri wale ambao ni wenye kula pesa za wengine. Wafisadi ndio wezi. Wafisadi

wapelekwe jela na wakapata taabu au kufutwa katika kazi zao(**clapping**).

Jambo lingine ni njaa katika jimbo letu la Pwani. Kuna njaa ambayo kila wakati inatusumbua kutafuta msaada za kutoka nje. Na tunaomba kwamba kama tukipata jimbo letu tupate msaada wa kufunga mito yetu kwa farms, irrigation, river dams. Hii ndo itakayotusaidia kupata maji yakunyunyiza mashamba zetu.

Jambo la mwisho ni kwamba sisi watu wa Pwani tupendane. Jimbo hilo laja lakini kusiwe na utengano. Tupendane watu wa Pwani. Sina zaidi, ni hayo tu.

**Tsangwa Ngala**. Mimi naitwa Tsangwa Ngala. Nakaa Kaloleni. Mimi naunga mkono wenzangu wanaopendekeza serikali ya majimbo. Mimi ninapenda hivyo kwa sababu umri wangu nimetawaliwa na serikali karibu tatu kwanza mkoloni, pili, hiyo ya majimbo, tatu hii iliyoko. Sasa vipimo vyote vile nimevipima, na nafikiri hata nyini Macommissioners mungeunga mkono majimbo kwa sababu leo uko juu ya nundu kesho utakuwa chini, na utaumia na hii Katiba tuliyonayo. Nikisema hiyo ni kwamba hii Katiba ilioko inakusanya pesa zote za uma kuziweka mahali pamoja. Na pesa zile kupewa mtu mmoja na kamati yake- watu sita, saba, nane. Sasa pesa zile mara nyingine hutumiwa kama kiboko cha wajumbe wenu muliowapeleka kule. Yeye hutupa macho pande hii. Je, yule anipenda? Ikiwa anampenda zaidi amwambia ampe shilling elfu nane hivi. Halafu anatupa macho pande ile. Yule namna gani? Ah… yule yuaja lakini sio sana. Mpe mia nne. Yule namna gani? Oh … yule hata hana haja na mimi ….. basi mpe shillingi hamsini.

Kwa hivyo hayo bado nazungumza tu kumwambia kwamba serikali iliyoko, ile katiba ilioko ni kwamba ilikuwa inaumiza watu kwa sababu ya zile pesa zinatumiwa vile anataka. Sasa tunapendekeza hivi. Ile serikali ya majimbo iwe na Governor. Serikali ile ya majimbo itakuwa na bunge. Serikali ile ya majimbo sasa ndio itakayokusanya zile pesa zote za jimbo hilo na kuziweka katika benki yake. Lakini kuna serikali kuu hapo. Sasa mimi ninapendekeza kwamba hiyo kodi yote robo tatu ibaki kwa majimbo, robo iende kwa serikali kuu. Majeshi yote itakuwa kwa serikali kuu. Wafanyi kazi wa majimbo yale napendekeza kwamba kutoka A mpaka Z wawe ni wazaliwa wa pale.

Hiyo itaondoa ufisadi kwa sababu wananchi watashindana kutembelea majimbo mengine na wataona wale wenzao wanaendelea vizuri nao watafanya bidii kushindana wale wengine. Kwa hivyo tutaondoa ufisadi. Na nikisema hivyo sio kwamba ni ubaguzi ah ah Wewe kama ni mtu wa bara uko hapa, unaishi hapa, mtoto wako ni sawa na wa jimbo hilo kwa hivyo ataajiriwa sawa sawa na mtoto hapo.

Upande wa biashara, Mkenya afanye biashara mahali popote ila tunataka kodi yake tujenge jimbo letu. Kwa hivyo kulingana na hiyo Katiba ikiwa namna hiyo nafikiri nchi itaweza kutajirika haraka na wananchi watakula matunda. Kila mtoto atajenga nyumba na kukunywa chai ya maziwa maana watakuwa waanajiliwa sawa sawa. Maana wacha sisi, kuna wengine, watoto wao wamesoma na hawana kazi na kazi ziko. Kwa hivyo tungependa serikali ya namna hiyo iwe ya majimbo na igawanywe

uchumi sawa sawa kulingana na kazi zote zimepewa vijana wa pale. Asanteni sana.

Nina mahali pengine ambapo kidogo pamenigusa. Hapo mahali ni katika karatasi hii. Nafikiri ni ukurasa wa nane. Unataja sehemu ya mwambao na mazrui. Hilo neno limezuka wapi? Hilo lilikufa mwaka wa sabini na mbili. Kwa nini likaingizwa hapo? Sasa mimi ninapendekeza hili liondolewe maana yake hili lilikwisha. Sultan alilipwa ridhaa huko ulaya Masettlers wake na wazungu wale wa highlands wakapewa. Na ile dani ile iliwekwa serikali ya Kenya, ikalipa mwingereza mpaka ikamaliza, kwa hivyo hakuna hili neno kabisa. Mazrui hakuna! Asanteni. (**clapping)**.

**Kisau.** Asanteni sana Ma-commissioners. Mimi kwa majina naitwa Alfred Kisau Ndunda. Nashukuru kupata nafasi hii nitoe maoni yangu kuhusu Katiba tuitakayo. Mimi mwenyewe ninaunga mkono serikali ya kimajimbo. Kwa hivyo basi ikiwa serikali ni ya majimbo kuna mambo kadhaa ambayo nimependekeza kulingana na mfumo huo wa serikali ya majimbo.

Katika serkali hii nimependekeza ya kwamba kutakuwa na mabunge mawili. Kwanza kutakuwa na bunge la kitaifa ambalo ni National Assembly. Katika bunge hili kutakuwa na Executive na Prime Minister na legislators. Yaaani kutakuwa na Rais ambaye hana uwezo wa kitawala halafu kutakuwa na waziri mkuu. Huyu atakuwa na ule uwezo yaani ana executive powers, kisha kutakuwa na wale wabunge wengine pale. Tuiangalia pale tutaona yule Rais ambaye hana power kazi yake itakuwa ni nini? Sana huyu kazi yake ni kukaa katika vikao ambavyo vinahusu mambo ya kitaifa kazi za kitaifa - national functions. Atakuwa aki preside. Na atakuwa afisini ama kwenye mamlaka kwa munda wa vipindi viwili vya miaka mitano. Na huyu Prime Minister atakuwa hivi, nilivyopendekeza: yeye ndiye atakuwa ana uwezo na atakuwa ni kiongozi wa Serikali. Yeye pia vile vile atakuwa mamlakani kwa muda wa miaka mitano lakini inapomalizika atakuwa tena anaweza kuchaguliwa mpaka pale atakapokosa kura kabisa. Je hawa viongozi au wajumbe wa bunge hili la kitaifa wanachaguliwa namna gani? Mimi ningependekeza hivi; Wabunge hawa ambao watakuwa wakiketi katika bunge la kitaifa watakuwa wakitoka pande zote za nchi yaani katika yale majimbo yoyote atakayetaka ubunge katika lile bunge la kitaifa yeye anaweza.

Na kuchaguliwa atapigiwa kura na wananchi wa nchi nzima katika majimbo yote wale voters. Na katika hayo mabunge mawili vile vile kutakuwa na serikali mbili; kutakuwa na ile Central Government, yaani serikali kubwa, na Regional Government. Katika serikali hizi mbili tuangalie kazi zao ni nini? Katika Central Govt. yaani serikali kuu, itakuwa na jukumu ya ulinzi (yaani defence), foreign affairs, (mambo ya nje), kutoa sarafu ya nchi (yaani national currency). Sasa serikali hii itakuwa mikononi mwa Central Govt ndiyo itakuwa ikitoa hiyo pesa na kuzi-control. Hapo nimemalizana na national assembly.

Tukiingia katika hizi serikali za kimajimbo sasa, kila jimbo litakuwa na Executive mtawala ambaye atakuwa na mamlaka Fulani. Hao watakuwa wakiitwa Governors. Kila jimbo litakuwa na Governor wake au pia wakitaka wanaweza kuchagua jina lingine, lakini yeye ndiye atakayekuwa kiongozi wa jimbo.

Kutakuwa na Judiciary yaani ule usimamizi wa mahakama au sheria za nchi katika kila jimbo. Wabunge pia watakuwa kule pia,

na hawa Regional Assembly members watachaguliwa vipi? Nimependekeza hivi: wabunge wa region, yaani la jimbo, hawa ni lazima wawe ni wenyenji wa lile jimbo. Nikitaka kueleza zaidi si mtu atoke jimbo lingine aje atake kuchaguliwa hapa kama mjumbe wa bunge la jimbo. Ni wale wenyeji wa pale. Na wenyeji wale watapigiwa kure na wale watu wanaishi jimbo hilo. Haijalishi hata kama wanatoka sehemu zingine lakini wawe wanaishi hapo, wana haki pia kumpigia kura mjumbe wa jimbo.

Na hizi serikali za majimbo zitakuwa namna gani? Serikali za majimbo zitakuwa zina uwezo, zitakuwa ziko huru yaani ziko independent, zinajitawala zenyewe kwa kila kitu, isipokuwa kwa upande wa defence, kama nilivyoeleza. Defence ama ulinzi itakuwa ni jukumu la serikali kuu (central govt.) na foreign affairs vile vile, currency, haya yata- achiwa serikali kuu, lakini mambo mengine yote, jimbo lenyewe litajienderesha. Kwa hivyo litakuwa ni autonomous kabisa, halitegemei chochote.

Mambo mengine, administratioin iwe scrapped kabisa, na pahali pake pawe na watu wamechaguliwa na wenye jimbo lile. Revenue: Ukusanyaji wa pesa katika jimbo. Kila jimbo litakusanya pesa zake yenyewe lakini litakuwa katika yale makusanya yamekusanywa litachukua kama robo ya pesa zile kupeleka serikali kuu ili kugharamia ulinzi foreign affairs n.k. hayo yatakuwa yakigharamiwa na serikali za majimbo kwa kutoa robo ya pesa zilizokusanywa. Mwisho kabisa, kutakuwa na tume ya kuajiri watu yaani Public Service Commission. Hii itakuwa huru kabisa, itakuwa yajitemea na itapitishwa na kila bunge kwamba kuwe na tume kama hio. Hii ndiyo itachukua jukumu la kuajiri wale watu ambao wana makazi kubwa kubwa, kama majudge, mahakimu kama tulivyosikia hapa n.k. katika serikali na mashirika ambayo si ya Serikali, sio NGO, hapa ni parastatals. Kutakuwa na team special ambayo itakuwa imetokana na bunge na itakuwa huru kabisa. Isiingiliwe ili kwamba pasiwe na mtu moja kama Rais akawa yeye ndiye anaandika kazi majudge na wale wakubwa wote wanaandikwa na mtu mmoja, la. Tumesema Rais huyo hatakuwa na nguvu hizo hata kidogo. Kwa hivyo mimi nimesema very briefly na hayo ndiyo nilikuwa nayo kuhusu serikali ya mwongozo wa majimbo. Asanteni nyote.

**Com. Lethome**: Aziz Zaro afuatwe na Wilson Ngao, na Charles Wandera akae tayari.

**Zaro**: Hamjambo nyote ndugu. Mimi kwa majina naitwa Aziz Zaro. Napendekeza kwa serikali za majimbo. Na serikali hii pendekezo langu ni kwamba ikabiliane na mambo ya devil worship - kumalizana na kuabundu kwa mashetani.

Jambo lingine ningependa kila Mkenya Katiba hii ihakikishe naishi above powervy line, na kwamba Katiba hii inafanya iwezavyo ili kuwe na joblessness allowance angalau mtu akifikisha miaka kumi na nane kuendelea awe anaweza kupata joblessness allowance na ku-create employement opportunities zile tunaona wengi tunaadhirika na ukosefu wa kazi.

Jambo lingine nataka katiba ya majimbo iwe itazingatia kikamilifu wale akina baba na mama ambao wamezeeka, sio tu wale wamefanya kazi kwa serikali ndiyo wanapata malipo fulani lakini hata wengine. Wangeweka kiwango ama utaratibu wa 'age' fulani ikiwa amepatikana na matitizo ya ugonjwa na hata shida ya poverty awe anaweza kujisaidia. Kwa sababu ya hii shinda ya hali ngumu ya kimaisha wengi wamekuwa hawawezi kujisaidia. Kwa hivyo serikali yetu ya majimbo ihakikishe kwamba

hawa akina baba, akina mama wamezeeka wanaweza kusaidiwa na kitu fulani.

Kitu kingine ni kuhusu kupunguzwa kwa hizi public holidays. Zimekuwa zimeongezeka muda kwa muda. Yule atakayepata urais unaona ameweka siku yake, yule mwingine anaingia anaweka siku yake. Kwa hivyo ningependa utaritibu wa majimbo uwe utapunguza jambo hilo na kuweza kupunguza.

Jambo lingine ni kuhusu corruption. Corruption must go. Corruption imefanya sasa hatuwezi kujiendesha saidi kwa sababu pesa nyingi iko kwa mikono ya watu binafsi na kuacha wale wengine wanapata shida. Kwa hivyo wale watakaopatikana wakifanya mambo ya ufisadi serikali ya majimbo iwe inaweza kuwachukulia hatua iwezekanavyo.

Jambo lingine ningependa serikali ya majimbo iangalie sana mamo ya Aids. Aids imekuea ni ugonjwa amboa uansabaa wengi wanakufa na wengi baado watakufa. Kwa hivyo pendekezo langu ni tuzingalie kikamirifu kuona ya kwamba haya mambo ya ukimwi inakuwa na uangalifu wa sawa sawa ili angalau na sisi siku nyingine hapa duniani tuone ya kwamba janga hili limetuondokea.

Jambo lingine ningependa kuelezea ni kwamba tuhakikishe serikali ya majimbo imeweza kuteua wale ambao wana usomi wa hali ya juu angalau Doctor of Philosophy katika vipawa tofauti tofauti ili wawe wanaweza ku-detect talents za wale youth wadogo na kuweza kuwamotivate na kuwaweka katika line zao, kwa sababu tunaona ya kwamba hapa Kenya kuna vipawa vingine havitiliwi maanani sana lakini kuna vingine vina- chukuliwa muhimu zaidi kuliko hivyo vingine. Kwa hivyo ningependa hao ambao katika serikali ya majimbo wataweza kuteuliwa kufanya kazi hii basi waweze ku-motivate. Tutaona hata sisi nasi tutakuwa na uwezo wa kukagua mambo ya maendeleo.

Jambo lingine la mwisho ni kutilia maanani maslahi ya kidini. Serikali iwe inaweza kutenga pesa za kuendeleza Mungu. Hakuumba Waislam pekee yake; hata Wakristo pia Mungu hakuumba Wakristo hata Waislam wale ambao ni budhists n.k. ili hali ya kidini iweze kuzingatiwa iwezekanavyo. Kwa hivyo ninaomba serikali ya kimajimbo iweze kufanya sisi hatuta-result to violence na hatuta-degrade ourselves to hatred, bali tuzidi kupendana na tuone ya kwamba inaji-dedicate fully to our survival in which we can live together happily, in harmony and with equal opportunity. Kwa hayo machache nawaombea Mungu, hii serikali ama katiba ya majimbo iwe na ufanisi wa hali ya juu. Mungu awabariki. Asanteni.

**Ngao**: Asanteni. Kwa majina ninaitwa Wilson Ngao na ninamapendekezo kidogo tu ningetaka kupeana. Ninaunga mkono serikali ya majimbo na ningesema Rais apunguzwe uwezo wake. Uraia uwe wa kijinsia. Mtoto anapozaliwa hapa, yaani tuseme ni mtu kama ameoa mke wa hapa, tuseme ni huyu, wakizaa watoto hapa wale watoto wapewe uraia wa hapa. Katika kitambulisho ningependekeza viwe vya kimajimbo ili uwe na wa uraia. Katiba iruhusu uwezo wa kipekee katika hali za hatari. Vyama viwili. Elimu ya bure kwanzia chini mpaka, tuseme, kiwango cha darasa la nane. Hospitali ziwe za bure. Ikiwezakana

kuwe na kama ma-clinic na kuwe na clinic moja moja katika kila location. Na kala ya katiba ikiwa itawezekana iwe inapatikana kwa maofisi ya chief ama sub-chief. Wenyeviti wa mabaraza wachguliwe na wananchi wenyewe kwa viendi vya miaka tano. Madiwani wawe na elimu kidogo kubwa tuseme elimu kama ya kidato cha nne. Tuwe na kulindwa kwa miti kama vile mnazi ama miti mingine zaidi ya hapo. Kesi za mashamba tuziwachie wazee wa kijiji. Civic education ifundishwe mashuleni. Haki za kibinadamu zidumishwe. Ufisadi ukomeshwe. Kuwe na tume ya kuajiri kwa kila mkoa. Na mwisho madawa ya kulevya yawe kando, yakomeshwe. Hayo ndiyo machache niliyo nayo kwa hivyo, asanteni.

**Wandera**: Mimi kwa majina naitwa Charles Juma Wandera. Nimekuja kutoa mapendekezo haya kwa niaba ya kikundi cha wale waliokuwa wanafundisha katiba- facilitators – wa Kenya Nut Growers Association Kaloleni Constituency. Kulingana na hao waliokuwa wanafundisha hiyo katiba chini ya cheti cha Kenya Nut, walipendekeza katiba ijayo lazima iwe na utangulizi utakaomwelezea yule anayoisoma awe ataelewa anasoma nini. Na iwe itaeleza muda wa hiyo Katiba utakaotumiwa.

Pili, wakazungumza sheria kuu ya katiba. Wanasema katiba, kama sheria kuu, isibadilishwe na bunge. Maana ni chombo ambacho kinatungwa na watu wengi kwa maoni ya raia.

Tatu, wakazungumzia uraia. Wanasema uraia katika nchi yetu ya Kenya yule ambaye ni mzaliwa Kenya; baba, mama ni mzazi wa Kenya, huyo apewe uraia bila maswali. Bali, mtoto mwenye amezaliwa na mzazi mmoja ni muhimu ya kupatikana uthibitisho kuwa babake au mamake, je kama si mzaliwa Kenya yuko tayari kukaa kama raia wa Kenya ndiposa huyu mwanawe aandikwe kama raia wa Kenya?

Waalimu walizungumzia muda wa serikali na wakaonelea, wakapendekeza kuwa kwa wakati huu wakaona wangependekeza serikali ya mseto na iwe na Rais na Waziri Mkuu. Ambapo Rais awe ata tawala taifa na Waziri Mkuu awe kiongozi wa serikali.

Kisha wakazungumzia kuhusu bunge. Wakasema bunge lipewe mamlaka ya kuunda tume ya kupinga ufisadi. Corruption. Na iwe itaeleza kikatiba, mgombea kiti cha Urais, wakapendekeza awe mgombea wa miaka kati ya 35-65. Maana wanasema umri au uzee zaidi unadhuru fikira za mwanadamu.

Wakazumgumzia habari za serikali za mitaa. Wakasema Mayor na Diwani wachaguliwe moja kwa moja na raia, na kipindi cha utawala wakaona miaka miwili na waende kwa vipindi viwili. Tume ya uchaguzi, wakasema mamlaka haya, ni heri yapewe bunge maana Katiba ilioko ilimpa Rais mamlaka zaidi ya kuchagua tume ya uchaguzi, ama kuchagua mawaziri, ama kuvunga bunge. Ambayo sana hii inachangia katika kura zilizo huru na haki. Maana muajiriwa humuhudumia yule ambaye amemuajiri. Sasa tume hii kuhakikisha kwa vyovyote vile isipofanya vyema kupendekeza yule ambaye alichagua tume hiyo, kuwa wahofia kazi yao.

Kuna swala la ardhi. Wakasema kuwa ardhi ndiyo kitu muhimu au haki muhimu ya mwanadamu. Na wakapendekeza mzaliwa wa Kenya ni lazima Katiba ichangie kwa kumpa ardhi mtu huyu. Kama mzazi au baba ni mzaliwa wa Kenya. Katika ardhi wakasema heri maswala ya ardhi iwachwe katika serikali ya mitaa na kuwe na baraza maalum ili kuwa itashughulikia kesi kama za mashamba.

Kisha wakapendekeza land title deeds za mashamba (cheti cha kumilikia shamba) heri kipatikane katika serikali ya mitaa na kwa urahisi na kwa njia timilifu.

Wakazungumzia habari ya vibali vya yule anayestahili kupiga kura. Wakasema miaka kumi na nane na kuendelea. Halafu wakazungumzia uwezo wa utumizi wa mali ya uma. Wakasema uamuzi huu ama uwezo huu ni heri upewe bunge.

Kisha mwisho hao waalimu wakazungumzia kuhusu wale waliokuwa wanafanya kazi ya waalimu wa katiba. Wakasema wanachangia kupigania corruption, kupinga ufisadi, ilahali wenyewe wanalalamika kuhusu malipo yao. (**clapping**)

**Com. Lethome**: George Dadu?

**Dadu:** Macommissioners ambao tuko hapa Kaloleni, na wazazi wote mumekuja, nitazungumza machache kwa maana niko na memorandum nitapeana hakuna haja ya kupoteza wakati. Isipokuwa nitaongeza kidogo. Mimi kwa jina naitwa Dadu George. Mimi ndio ninasimamia human rights Kilifi. Na tuna bahati kwamba shughuli hii ya kurekebisha Katiba imefika mwaka huu ambao nayo human rights limeingia kuwakilisha Kilifi District. Tuliyozungumza yote hapa ni kuhusu mambo ya human rights vile inavyopigania, tunataka utawala mwema na yale yote tulikuwa tunataka Katiba irekebishe sitayatoa hapa. Nitataja yale ambayo hayako kwa sababu memo nitaiwacha hapa. Nitaongeza tu kitu kidogo kwamba serikali yetu sasa imeshaunda tume ya human rights. Shirika letu la human rights ni shirika la kujitegemea, "NGO". Kitu nitaomba ni kwamba ile tume ya serikali iweze kuwakilisha pia mashinani mahali kama hapa, divisional headquater. Tuwe na afisi ya tume hiyo ya serikali ya human rights ili na sisi ambao tunawakilisha haya mashirika ya kujitegemea, tuweze kuwasiliana, tuone vile tutagawanya mawazo na tutaenda kwa mashinani ki namna gani. Shirika hili la huma right ambalo linawakirishwa hapa, si la kukosoa serikali kwa sababu wengi wanafikiria kuwa kila ukisikia human rights kuna ushirikiano.

Nilikuwa nataka kupendekeza kwammba wakati wengi wamezungumza hapa wametaja majimbo. Okey, majimbo twaitaka bila shaka. Lakini mimi ningependa kupendekeza serikali ya mseto na labda nieleze sababu kidogo. Ni kwa sababu hii dunia yetu inakuwa kidogo, sasa dunia hii tunaiita 'global village'. Ni kijiji kidogo. Watu wanakuwa wengi, dunia inakuwa ndogo. Na si ajabu pia hapa hii East Africa Community mtakuta kama tunaungana. Sasa ikiwa sisi tutarudi nyuma tuanze kujikata kata tuwe na vijimbo vidogo vidogo, I don’t know whether we are moving forward or we are going backward.

Ninapendekeza serikali ya mseto ya pamoja badala ya kujikata kata katika majimbo ilikwamba tuwe tutaenda na dunia hii

ambayo inakuja kwa kuungana. Tunaendelea upande wa muungano.

Jambo lingine ambalo nitalizungumzia kwa kiasi kidogo ni kuomba katiba iwe itafikiria sana kuhusu kuwapunguzia wanabiashara, hasa wa upande wa uchukuzi, makodi. Ili kwamba matajiri waweze kupata nafasi ya kupanua kazi zao na wananchi kupata nafasi ya kuandikwa kazi. Kwa sababu ukiangalia kama hivi sasa matajiri ambao tuko nao hapa, magari mengi yamelala kwa sababu ya kushidwa na kodi na wananchi wengi wameacha kazi, wako manyumbani.

**Com. Lethome:** Tafadhalini tusikizaneni. Kuna fujo fujo kidogo, haya.

**Dadu**: Kwa hivyo sitaongeza zaidi ni hiyo tu ya kodi za magari zipunguzwe na tuwe na afisi ya mashinani ya human rights. Kwa hivyo kwa hayo machache haya mengine mutayasoma mbele.

**Majimbo**: Haya asanteni. Kama mlivyosikia majina yangu yametajwa naitwa Paul Majimbo. Niko hapa nawasilisha maoni ya kikundi kilichokutana kujadili. Kwa hivyo kwa maoni ni kwamba Katiba ya sasa ya nchi imekuwa fumbo. Yaani hivyo ni kusema jamii ya Wakenya wengi hawajui Katiba ya sasa.

Na tukapendekeza kwamba vile ambavyo tumefahamishwa kwamba Katiba ya sasa haina utangulizi. Basi Katiba ya sasa lazima iwe na utangulizi. Kwenye utangulizi sharti ielize kuwa Katiba ilitugwa na akina nani ambao ni jamii ya wa Kenya. Inalinda haki za akina nani ambao ni jamii ya Wakenya wote, itekelezwe na akina nani, yaani utawala wa nchi na Wakenya wenyewe, na kwa namna gani. Katiba itekelezwe na kuheshimiwa, yaani kuwe na uhuru wa utekelezaji. Na kwenye utangulizi ieleze wazi kwamba ni hatia kukiuka Katiba hiyo. Katiba ikiwa sheria au kanuni zilizojadiliwa na kukubaliwa na jamii kwa pamoja, sharti umuhimu wake ushambazwe kwa kutayarisha nakili ambazo zitasambazwa kwa wananchi wote kwa ufahamu zaidi.

Umuhimu wa Katiba. Katiba sharti ifanye jamii ya Wakenya wawe kitu kimoja. Katiba ilinde haki miongoni mwa jamii ya Wakenya. Katiba lazima ilinde usalama na idumishe amani miongoni mwa jamii ya Wakenya. Katiba lazima ilinge uchumi wa jamii.

Uwezo wa Katiba. Uwezo wa Katiba hauwezi kuwa mkamilivu bila kuwa na uhuru wa kutekeleza na kuheshimu Kabita. Katiba inayoundwa sasa ikiwa inatokana na maoni ya Wakenya wenyewe bunge lisiwe na uwezo wa kubadilisha katiba bila kushauriana na wananchi. Hivi ni kusema tume ya sasa ya kurekebisha katiba haina budi idumu kikiwa chombo cha mawasiliano juu ya maswala ya kikatiba.

Ikiwa Katiba inalinda haki za watu wote, kusiwe na mtu yeyote ambaye atakuwa juu ya sheria. Mabadiliko kwenye maongozi

ya nchi. Waziri Mkuu ahusike na maswala ya maendeleo ya nchi kwa jumla. Waziri ahusike na usalama wa ndani ya nchi.

Rais wa nchi. Rais atawale nchi kwa vipindi viwili pekee, anapochaguliwa kwa kura ya siri pekee. Rais ahusike na utawala wa taifa. Hivi ni kusema abaki amri jeshi mkuuu wa vikosi vyote vya usalama na awe ni yeye pekee anaweza kutangaza na kuongoza majeshi kwenye vita kupambana na uvamizi wa nchi.

Uhabiri wa vyuo vikuu: uhabiri wa vyuo vikuu utoke mikononi mwa Rais hadi kwa waziri mkuu atakaye-simamia usalama wa ndani wa nchi. Utawala wa nchi umerithi ukoloni kutoka kwa wabeberu na hivyo basi mnyonge hana haki. Wananchi wamenyanyaswa haki zao ama amenyimwa haki. Mnyonge hana sauti na hivyo basi hana uhuru wa kutekeleza Katiba kupata haki.

Mabadiliko kwenye utawala. Viongozi wote wanaosimamia utawala wa nchi sharti wachaguliwe kwa kura ya siri kuimarisha heshima na utekelezaji wa kikatiba. Kulinda haki za watu: Hali hii itafanya vikosi vyote vinavyotekeleza mkono wa sheria vikisimamiwa na viongozi waliochaguliwa na wananchi haswa kutoka kwa maeneo wanayotoka kuheshimu haki za wananchi. Badala ya wakuu wa mikoa, tuwe na viongozi wa majimbo, Ma-governor, watakaochaguliwa na mkoa mzima. Governor atakuwa mkuu wa utawala wa mkoa, hali itakayawezesha utawala na wananchi kuishi kwa amani. Pia governor ahusike na maendeleo ya mkoa wake.

**Zabibu:** Asanteni. Mbele yenu ni Tecla Zabibu kutoka Mabayanyundo. Na ningependa kuwakilisha vijana wa Secondary School Youth Association na swala la kwanza ni mitihani ya lugha katika uchaguzi wa wabunge. Sisi jumia ya vijana wa Secondary School Youth Association kutoka Karafungo location, Kaloleni Division, Kilifi District, tunapendekezo letu la kutaka katiba mpya itakayoundwa iondoe mitihani ya lugha katika uchaguzi wa wabunge. Na badala yake Katiba hiyo iweke masharti ya kuhitumu kielimu kwa wagombea wote katika uchaguzi. Yaani katika wale wote wanaogombea viti vya katika ubunge wawe wamesoma mpaka university, katika elimu ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Swala la pili. Kuhitimu kwa wagombea viti vya umaya na udiwani. Tungependa pia kutoa pendekezo la kutaka Katiba mpya iweke masharti ya ugombea viti vya umaya na udiwani kwamba yule atakaye kugombea kiti cha umaya ama udiwani awe na elimu ya kiwango cha university itakayomwezesha kusimamia kikamilifi shughuli za kiutekelezi na za kifedha katika hali iliyo bora zaidi katika maendeleo kulingana na hali ya kisiasa ya kumiliki mambo. Hapa tukapata mzee mmoja akatwambia ya kwamba Councillor sio lazima wawe wamesoma kwa sababu kuna wengine ambao wako na hekima. Lakini sasa tukiona huyu mzee yuko na hekima tutakuta hata kama yuko na bibi kumi anaweza akaongoza vizuri. Je, akielimishwa si anaweza akafanya very great things? Lakini tukisema yule, hekima ile ile si lazima apelekwe shule, je ataweza akatusomesha kweli? Atatuangalia aseme, ah, huyu ni mwerevu. Tosha hayo. Kwa hiyo ningependelea kwamba ukiwa na uongozi wowote ambao mtu anataka asimamie watu ama asimamie jumia fulani, awe na elimu ya kuongeza ule ubora wake wa kiakili. Aweze kufikiria kwa kiwango cha kielimu. Si kwamba ni mwerevu ni basi anaongea sana. Sivyo.

Swala la tatu. Kuhitimu kwa wagombea kiti cha Urais nchini. Tungependa kutoa pendekezo letu kutaka Katiba mpya ya nchi iweke masharti ya kuhitimu kwa mgombea kiti cha Urais. Maendeleo ya nchi yoyote ile inategemea ujuzi na elimu ya viongozi wake kuelewa mambo ya kimaarifa haswa katika maswala ya ki-jamii, kiuchumi, kisiasa n.k. Kwa sababu tunataka kuendeleza Kenya yetu to the stage of industrialised country, there is no way mtu ambaye hakusoma anaweza akafikiria kiundani jinsi ya kuwalinda kuendelesha nchi yetu. Awe amefikia university. Ni hayo tu asanteni.

**Kadede:** Kwa jina naitwa Peterson Kadede. Na mimi yangu ni mapendekezo. Mimi nimependekeza serikali ya majimbo. Na nimependekeza serikali ya umoja na serikali ya majimbo. Serikali yetu ya umoja tunaikataa kwa sababu ya mambo yake. Hata hawa Commissioners wamekuja hapa kuchukua maoni lakini wale waalimu waliofundisha civic education hawajalipwa kitu chochote. Na wanalalamika mpaka leo. Kwa hivyo tunaonelea tukipata serikali ya majimbo itaangalia zaidi watu wake wa jimbo lake. Maanake waalimu wametoka katika jimbo hili na waliofunzwa ni wa kutoka jimbo hili. Kwa hivyo mimi nimependekeza serikali ya majimbo.

Na serikali ya majimbo upande uchaguzi wake. Tunataka kuwe na mwaka wa uchaguzi kwa sababu nimeona taabu ya wale watu ambao wanaenda kupiga kura anaenda kusimama muda mrefu akingoja mmoja ameingia ndani na kule kuna madebe matatu la Diwani, Mbunge na Rais. Kwa hivyo anasimama pale, yule mtu mpaka ahojiwe mara tatu. Ndio nikasema kuwe na mwaka wa uchaguzi. Madiwani wachaguliwe mwezi wa nne; iwe ni siku ya uchaguzi wa Madiwani na Wabunge wachaguliwe mwezi wa nane iwe ni siku ya uchaguzi wa wabunge. Na Rais achaguliwe mwezi wa kumu na mbili. Kila mmoja awe na kipindi chake. Kupumzisha ule msongamano wa watu kwenda kupiga kura kushinda pale mchana kutwa. Kwa hivyo upande wa uchaguzi katika mambo yetu ya serikali yetu ya majimbo, tunaomba kuwe na mwaka wa uchaguzi.

Na kuna mambo ya haki za wazee. Kuna wazee wengine ambao wameoa, wamezaa na watoto wao wamepotelea Mombasa huku, anabaki huku (inaudible). Na chakula kikiwa kimeletwa cha msaada ni cha mwezi mmoja. Kinaletwa pale unapata kibaba kimoja. Halafu chakula cha msaada kimekwisha. Kwa hivyo ningependekeza serikali yetu ya majimbo iangalie wazee wetu wale ambao wana umri wa zaidi ya miaka sitini wawe na mshahara watakuwa wakilipwa na serikali kusaidia mambo yao.

Na kuhusu uandikishaji wa, huu uchaguzi wa Rais wa kimataifa. Uchaguzi ule uwe namna hii tulivyopendekeza. Ikiwa Rais kwa sasa ametoka jimbo la Rift valley kipindi chake kikiisha, Rais yule atakayechaguliwa atoke jimbo lingine kama jimbo la pwani. Na uchaguzi uwe namna hii. Wale watakaogombania kile kiti cha urais wote wawe wametoka Mombasa, kwa mfano jimbo la Pwani. Wachaguliwe hao kama ni watatu, ni watano, kila chama kitapeleka muwakilishaji wake wa urais. Wachaguliwe apatikane wa kutoka jimbo lile. Lakini sasa tukitoa wa jimbo hili, wa jimbo lile, tutakuwa tunapeleka kile kiti cha urais upande mmoja. Kwa hivyo uchaguzi wa Rais uwe unatembea kwa kila jimbo ikiwa kipindi chake kimekwisha. Kipindi hiki tuko na Rais ametoka Pwani kikiisha kipindi chake tutoke kwenye Rais aliyetoka upande mwingine. Kwa hivyo uchaguzi ule wa Rais uwe unatembea kwa majimbo.

Na nikimalizia ni kuhusu mambo ya uraia. Raia wa jimbo awe ni mzaliwa wa jimbo. Na mtu anayeweza kumiliki ile title deed awe ni mzaliwa wa jimbo lile lile. Kwa sababu tukisema yeyote atapewa karatasi ile ya kumiliki ardhi, hii jimbo letu tutaliuza. Maanake watakuja wenye pesa tutawauzia na watapata haki wao, sisi tutabaki kama ma-squatter. Kwa hivyo mtu anayepewa cheti kile cha kumiliki ardhi awe ni mzaliwa wa jimbo lile. Kwa hayo machache asanteni. (**clapping**).

**Com. Lethome:** Sasa kabla hatujaendelea, kuna jambo ambalo tangu asubuhi linakaririwa, kuhusu mambo ya waalimu wa civic education kutolipwa. Na sisi kama tume hupenda kufanya kazi wazi wazi. Hatutaki mtu yeyote awe gizani. Kwa hivyo tuna district coordinator ambaye ni mwakilishi wetu katika wilaya ya Kilifi, yuko hapa, Bw. Daniel, kidogo tunataka kumpa dakika mbili, tatu, ajaribu kututoa taka macho kuhusu jambo hilo la civic education. Ataeleza kidogo.

**Daniel:** Asante sana Ma-commissioner na wananchi wote wa Kaloleni Constituency ambao muko hapa. Nataka kuchukua fursa hii kueleza jinsi ya matumizi ya fedha ambazo zimekuja kwa minajili ya civil education. Macommissioners wako hapa na wanaelewa vizuri sana. Pesa ambazo zimekuja kwa civic education za kwanza zilikuwa ni 47,000/= for every constituency. Halafu tukaletewa zingine ambazo ni 50,000. Na 47 na 50 thousands, jambo la kwanza tumekuwa na workshop kama mbili na workshop hiyo ya kwanza ilifanywa Kilifi Institute of Agriculture, na walikuja civic education providers, na kila kikundi kilileta watu wawili tuliwagharamia na lunch, pamoja na ticket yao ya kurudi. Tulipea kia provider 200 wakati huo, na wako hapa, wengine na watasema ni kweli ama ni uongo na tuna record. Tukafanya ingine tena amabayo ilikuwa katika county council wakaja vile vile. Halafu kuna ingine ilifanywa na Macommissioners ikabidi civic education providers, pia tukawapatia 200 za kurudi. Bali na hivyo baada ya pesa ndiposa tuje kuwalipa ile kazi na claims zao, tumekuwa tukilipa kadri ya uwezo ambao tuko nao. Kwa sababu kwa mfano nikizungumzia Kaloleni Constituency pekee yake tuko na makundi kama, Kenya Nut Growers, tuko na World Revival tuko na mitengo miwili moja ni program, moja ni project. Sasa katika makundi haya, tukumbuka katika elfu zile zile kwa mfano hamsini zilizokua ni lazima uwape wagawanye. Kunacho kikundi kimoja ambacho tayari kimeleta claims za karibu 35,000. Kikundi kimoja peke yake. Kikundi kingine kimeleta claims za jumla ambazo tushalipa mwanzo 10,000 wanaleta claims za 23,000. One of the integral group World Revival wamekuja tumelipa zaidi ya another eight, nine there halafu na Kenya Nut, sasa niambieni, ukiangalia total ya zile pesa tumelipa kila kikundi karibu 97,000 zimekwisha na deni bado zinabaki pale pale na Macommissioners hawa kufikia leo ni kwamba deni bado liko pale. Na shinda hiyo si kwa Mombasa wala Kilifi, ni nationalwide.

Kwa hivyo (inadible) mimi nawaambia, iwapo pesa zitakuja tunalipa. Zikija mara moja tunalipa. Na office yenu kama tunavyosema Macommissioners iko wazi. Mtu yeyote na aje, tuko na recored pale Kilifi County Council, nitamfungulia vitabu vyote wana-sign wenyewe, wanaweka ID card number, na pesa wanachukua. Mje muone total ya zile pesa tunazolipa. Although hii Kilifi tumelipa an excess of 1000 ambazo tumechukua kutoka kwa Zanze Constituency kwa sababu ya kurekebisha shida ile iliyokuwa pale.

Bahari pia vile vile nimelipa an excess of 2,600 kutoka kwa mfuko wa Zanze ili kutakua shida. Zanze hivi sasa imebakia na karibu 14,000 ambazo wakija nitalipa 14,000 nao wabakie watu wa Bundani. Na shida hii ni Kenya nzima. Lakini tume inajitahidi vyovyote iwezavyo. Ikiwa itaweza, wanaweza kuwalipa pole pole. Lakini hiyo ndioyo hali, hakuna pesa inayoliwa tuna record, tuna supervisors wana-check. Nafikiri ni hayo tu.

**Com. Lethome:** Haya yamesemwa na huyu mwakilishaji wetu hapa, tuna wahakikishia, ni hivyo hivyo. Pesa ambazo zimetoka katika tume mpaka sasa kugharamia shughuli za civic education katika kila sehemu ya uwakilishaji bungeni, constituency, ni elfu tisaini na saba pekee yake. Sisi wenyewe kama Macommissioners tunajua hazitoshi kabisa. Kwa sababu kuna constituency zingine tumekwenda unakuta, kuna civic education providers ishirini na watano. Makundi ishirini na matano. Hebu niambie ukigawanya elfu hamsini kwa makundi ishirini na tano, inakuwa ni elfu ngapi? Elfu mbili. Wengine nauli peke yake ya kutoka pahali moja mpaka pengine, pesa hizo hazitoshi. Na ukiangalia constituency moja, tunazungumza juu ya constituency mia mbili na kumi. Kwa hivyo hilo ni tatizo ambalo hata sisi Macommissioners tunajua. Na ndio maana tukitoka sisi wenyewe wiki tatu kwenda kuzunguka pia kusaidiana na wale wanaosomesha civic education ili kazi hiyo tuweze kuifanya sote. Kwa hivyo tunajua kuna huo upungufu, wala upungufu haukutokana na District Coordinator, unatokana na upungufu katika Kenya nzima.

Kwa hivyo ni upungufu ambao tunaujua sisi uko na wale ambao wanadai tume itashughulikia. Na kama nilivyowaambia hakuna tume ingine ambayo ina u wazi kama hii yetu. Sisi mpaka makadirio yetu ya pesa tunazotumia ilichapishwa kwenye gazeti. Haipiti mahali popote, ilichapiswa kwenye gazeti kuonekana. Pesa ni ngapi zimeingia na ni ngapi zilotolewa. Kwa hivyo sisi yule bwana, kama kuna lawama yoyote, asilaumiwa yeye, ilaumiwe tume, na tume inajua ni kwa nini kumetokea upungufu kama huo. Kwa hivyo tungependa kuhakishia hivyo. Tunaendelea, Mariam Ali? Haya endelea.

**Kintu**: Mimi ninaunga mkono… jina langu ninaitwa Gerishom Marua Kintu. Mimi ninapendekeza uongozi wa majimbo maana uongozi tuliokuwa nao kutoka hapo wa chama kimoja unachelewesha Kenya nzima kutosheleza mahitaji ya Kenya nzima. Lakini ikiwa ni uongozi wa majimbo itakuwa rahisi jimbo kutekeleza mara moja mipango yake. Kwa maana hata utona kuna utafiti ambao unafanyika kila jimbo kwa kutazamia dhamani yake, ndani ya ardhi kuna madini gani. Lakini hata yakionekana si rahisi kuchimbwa hata kupatikana. Sasa kwa sababu kuna mahitaji mengi ya kila sehemu si rahisi ya kila jimbo. Sasa serikali ikiwa ya majimbo, kila jimbo litaweza kutekeleza mambo yake.

Na hospitali pia, hospitali ikiwa moja majimbo matatu inaumiza watu. Nigetaka serikaloi ya majimbo ijayo ijaribu kila sehemu ambayo, tuseme, kwa kila chief watatu kuwe na clinic ambayo itatuletea madawa ya wananchi. Na hizi schools pia, secondary school mbali mbali na hata hizi university pia hatuna hata moja hapa. Tupate angalao moja.

**Kahindi:** Jina langu naitwa Raphael Kahini. Asante Commissioners kwa kunipa wakati huu. Kwa sababu mengi yashazungumzwa na wenzangu na hii memorandum nitaiwacha hapa, nitapitia tu kidogo kidogo.

Kwanza serikali ya majimbo yataweza kupanga mipango ya jimbo na hivyo kuharakisha maendeleo. Rais awe amri mkuu wa majeshi. Rais asiteue Majudge bali Majudge wateuliwe na bunge. Waziri mkuu awekwe pale …….. waziri wa afya yupo. Sheria ya ardhi ambayo tulirithi kutoka kwa wakoloni ichunguzwe. Kwa sababu ardhi ni ya wananchi na serikali ya wakoloni ilichuka nafasi hiyo kufanya ardhi iwe yao. Hivyo ndivyo basi tunapewa title deed, kuonyesha kwamba hii ardhi ina mwenyewe. Unapopewa title deed ardhi ni ya serikali. Kwa hivyo napendekeza mambo ya ardhi yarudishwe kwa wenyenji. Unapokaa ndiko kwako. Halafu katika mizozo ya mipaka irudishwe tena kwa wazee wa vijiji. Tume ile ya DO tumeziona hazifanyi kazi. Ukweli unabadilishwa unakuwa uongo. Tushaona kesi ambazo zina judgement ya kortini na mwingine kuwastaki kwa wazee hao, ile judgement ya kotini inabadilishwa na mambo yanakuwa mengine. Kwa hivyo hapo kuna undanganyifu fulani, kwa hivyo hizo tume ziondolewe.

Uhuru wa kidini wa kuabudu. Katika Katiba ya sasa uhuru wa kuabudu uko. Lakini taabu moja ni kwamba haina kipengele cha ku-guard ule uhuru. Kwa sababu mimi ninapokuwa ni muumini wa kwenda kanisani siku ya jumamosi, na tajiri agundue kwamba mimi nimeingia imani ya kwenda kanisa siku ya jumamosi. Ninapomba ruhusa ya kwenda kazini jumamosi wataanza kusema wewe ukiwa hutakuja kanisani nitakufuta kazi. Hivyo hata binadamu hapo haipatikani hata uhuru wa kuabudu haupatikani. Kwa hivyo kuwe na kipengele cha kwamba muajiri anayeweza kukufuta, muajiri huyo aweze kushtakiwa na kupelekwa kortini.

Halafu la mwisho kabisa ni rushwa. Wafanyi kazi wote kutokea ngazi za mashinani hadi ngazi za Rais, atakaye-patikana akila rushwa aadhibiwe vikali na zile pesa ama rushwa yote ikiwa itapatikana na mali ya magendo, hiyo mali iweze ikaitishwa. Na washtakiwa ambao watapatikana wakihonga ama akihongwa basi achukuliwe hatua za kisheria. Asanteni.

**Com. Lethome:** Shumaa M. M. tafadhali dakika zako mbili, ili tuweze kwenda mbio mbio.

**Sumaa:** Majina yangu naitwa Shumaa Munga. Na nina mapendekezo yafuatayo. Kwa vidokezo kwanza wabunge wawe na siku za kufanya kazi angalao nne, ambazo watakuwa wanawajibika na kama ni watoke kule bunge basi ni waombe ruhusa kama mfanyi kazi mwingine.

Pili, elimu: pendekezo langu ni kwamba wenye kusimamia elimu nao pia wawe watoto wao wanasomea hapa nchini hata kama ni kupewa nafasi ya kuwa wasome bure. Kwa sababu gani? Hivi sasa kuwa kuna mgomo unakuja lakini wale wanaosimamia watoto wao wanasoma nje. Wale watoto wa wananchi ndio watakosa kwenda shule. Na ndio maana wanaweza wakawa stubborn kiasi hicho kwa sababu, pili pili usiyoila ya-kuwashia nini? Hawashi kwa hivyo hawajali.

Ninapendekeza pia hawa wabunge mshahara wao uwe unaonyesha ile mapato ya mwananchi wa kawaida. Kwa sababu hivi sasa yule mwananchi wa Kenya kwa mwezi labda mapato yao ukifanya average ni mia nane. Na wao zao ni elfu, labda mia sita

in total. Kwa hivyo ingekuwa ni fraction isizidi may-be 200% of the per capita income of the ordinary citizen. Yaani ikiwa mwananchi anapata mia nane kwa mwezi, basi yeye iwe inaweza ikafika kama elfu ishirini. Kwa sababu hiyo ndio wananchi hataweza kununuliwa na Wabunge. La sivyo, basi mwenye shida hawezi akamjua mwenya njaa. Wabunge wapenda kujinufaisha wenyewe na haitasaidia.

Lingine ni kwamba kuna kazi ambazo zinapewana za serikali kama kutengeneza barabara ama kama nyinyi Macommissioners. Hizi kazi ziwe na wakati. Na kwa mfano sasa kunaongezwa wakati Macommissioners. Ilikuwaje wakapanga mpaka wakati huu na sasa waongezwe? Kama ni uongezwe gharama ni ishikwe na nani? Kwa mfano kama babarara ya Mombasa- Nairobi ilikuwa ni iishe mwaka jana, sijui mwaka juzi, haijamalizika mwananchi anataseka, contractor amekula pesa, serikali imetulia. Ingetakikana katika katiba ijayo mtu asipomaliza kazi yake kwa wakati ambao ametaja yeye mwenyewe na wamekubaliana, basi mtu huyo awe anawajibika kulipa ile gharama ambayo imesababiswa na kuchelewa kwake.

Nikimalizia au kuongezea ni kwamba wale wanaochaguliwa ki serikali kwa mfano kuongeza mashirika ya kiserikali au kusimamia kazi za kiserikali, wawe wanaelimu inayofanana na kile wanachosimamia. Kwa mfano si vizuri mtu aliyekuwa mwanajeshi kusimamia afya, na yule anayesimamia, pengine, kitu kingine awe hana elimu ya kufnana na hiyo. Ndio maana unakuta hata watu wanasimamia mambo ya mazingara na yeye mwenywe na elimu ya kimazingara. Ndio kuna uharibifu huo. Kwa hivyo, watu wakichaguliwa mtu awe ana hiyo elimu ya kusimamia lile jambo analolisimamia. Labda nitamalizia tu hapo kwa sababu ya wakati. Asanteni.

**Com. Lethome:** Douglas Mkany Gaga.

**Mkanyi:** Kwa majina yangu naitwa Douglas Mkanyi Gaga kutoka pale Jibani. Yangu ni mapendekezo. Kwanza ningependekeza serikali ya kimajimbo. Na katika kupendekeza serikali ya kimajimbo basi ningesema sababu lakini wakati hautaki. Nitaendelea kupendekeza. Kwa hivyo niendelee kupendekeza ama nitoe sababu?

**Watu**: Endelea.

**Mkanyi:** Sawa. Nitaenda pia kwa elimu. Elimu tumesema sisi wote iwe ya bure na imekuwa haiwezekani. Lakini tunalilia kama serikali itakuja ile tuitakayo elimu iwe ya bure. Kutoka kwa chini kabisa nursery hadi university. Vile vile pia tungependekeza kila lacation iwe na shule mbili au zaidi kwa watoto mayatima, kutokana na hali tuliyo nayo sasa kwa sababu watu wengi wanakufa sasa wazazi wawili kwa ugonjwa tulio nao wakati huu.

Tukienda kwa mambo ya ujenzi, haswa wamabarabara na madaraja, tungesema tender zile kwa sababu ni kuchaguliwa ni nani watashirikiana na serikali ndiyo huwa sometimes zina - fail. Kwa hivyo tungesema wahusishwe wenyeji kule wale ambao wako na hiyo barabara karibu kule. Wakakuta ni watu gani ambao wachukuwe ile tender.

Nikienda kwa mahospitali, mahospitali tungependelea hasa kwa kila location iwe angalao na dispensary moja ya kiserikali. Na badala ya zile shilingi ishirini ishirini, ambazo ingekuwa inatolewa kwa sababu ya mambo sijui, ya madawa, serikali itoe zile huduma bure. Kwa sababu kuna wengine ambao hawajiwezi.

La mwisho kabisa naingilia ardhi. Ardhi ningesema isiuzwe bali ikodishwe. Kwa yule atakokishwa ghali basi awe na muda wa miaka thelathini au thelathini na tatu na baadaye aachie mwenye kumkondisha ile shamba. Ndiyo tutaachana na mambo ya u-squatter. Ningeenda zaidi lakini kwa sababu muda hautaki, hiyo kidogo nafikiri itatusaidia.

**Com. lethome**: Asante sana Kalachu?

**Kalachu:** Jina langu naitwa Samson Kalachu. Mimi natoka Kambe. Mambo mengi yamezungumzwa hapa sitayatoya isipokuwa nitataja yale ambayo yameachwa.

Serikali ambayo ningelitaka ifanywe ni federal system yaani majimbo. And they were not specific or federal system. Ziko federal system nyingi. Kwa hivyo ikiwa imekubaliwa ni majimbo, tuchague ya aina gani; kama ni ya Canada, ya America, ya Germany ambayo ita-suit our country.

**Com. Lenaola**: unataka gani wewe?

**Kalachu**: I am not a technician. Nataka nyumba lakini nitamwita fundi anijengee nyumba ile. Sio eh?

**Com.Lenaola** : Sawa.

**Kalachu:** umeelewa hivyo? Na upande wa power, katiba ya sasa is above the law. Nataka awe within the law. Na, pendekezo tu hilo. Tukienda upande wa judicial system katika upande wa locations hakuna well organized system ya watu wakikosana, iko maguguni kule. Kuwe at least other deparments huwa na extensional officers mpaka grasroot levels. Twakata kuwe na trained people ambao watasaidia kupatanisha watu kwa sublocations.

Jambo lingine ni la uchumi. Watu wengi wametaja tembo la mzani. Tembo ya mnazi nafikiri sio haramu. I don't think in our law it is saying it's a …..eh? ni haramu? Kama si haramu ningependekeza iwe si haramu na wananchi waruhusiwe kufanya wapedao. Kama ni bottling watu wanasema kwenye bottling and its something already done … (inaudible) Kwa hivyo ni mambo ya kuji-implement tu. Ikiwa inatufanya huru sisituko tayari, uko ujuzi wakutosha pia katika chupa za kama beer, na nini hii iko uwezekano. Na ni uchungu mwingi sana wa hapa Kenya……. Ah ….. wa hapa federal policy. Coast is a part of Kenya isn't it.

**Com. Lenaola**: Haya endelea

**Kalachu**: Jambo lingine nilikuwa nafikiria pengine katika our country kuna mtu anaitwa Ombudsman I don’t know how we call him in swahili. Lakini tunataka mtu kuwa naki…… mmoja ametaja kuwa na commissinal….. something like that. Ambayo kama mtu amekosewa anaweza kutowa, wanatoa report bila kuogopa, kama ni President kama ni nani, kama ni nani, anatoa hiyo. Hiyo itakuwa inasaidia. Na jambo lingine hii … ah … mambo mengi yametajwa. Corruption. Tunazo wakati wa election wale wanapigania ubunge wana corrupt wananchi. Nafikiri hiyo system iachwe. Mtu akihonga wapiga kura achukuliwe hatua. Asante.

**Com. Lenaola**. Darius Nzombo

**Nzombo**: Kwa majina naitwa Darius Nzombo Malani kutoka Maadani. Ningependekeza kuwa serikali iwe ya majimbo.

Pili, zile pesa zote ambazo zitakusanywa na jimbo ziwe kutakuwa na alisimia kumi na tano ambayo itapewa wale ambao hawana kazi na wale ambao mshahara wao ni wa chini, elfu moja mia tano. Ni hayo tu, asanteni.

**Com. Lethome:** Asante sana Darius. Mdali Mwelu?

**Mwelu**: Kwa majina najulikana kama Mdali Mwelu na ningependa kupendekeza yafuatayo. Kwanza ningependa napinga hiyo serikali ya majimbo bali ile serikali tunayopenda kuwa nayo ni ile serikali ambayo inaweza ku-take care of its people.

**Com. Lenaola**: Ya ina gani?

**Mwelu:** Serikali ambayo inaweza kutoa elimu ya bure, kutoa chakula kwa watu wake na kutoa security nzuri kwa watu wake. Hiyo ndio nasema. Halafu jambo lingine, tundependa nitaguzia upande wa university. President asiwe Chancellor wa university za Kenya. Bali wale ambao ni vice chancellor wawe ndiyo watakuwa Chancellors. President awe anakwenda ku-preside over graduation pekee yake lakini asiwe Chancellor. Upande mwingine kuhusu university wale registrars, charmen of departments na wale ambao watakuwa chancellors wawe wanachaguliwa na hiyo univerity senate. Sio mtu tu alale huko na aje aseme pengine, ndiye university executive kwa sababu akifanya hivyo, adminstration ya college itakuwa mbaya na hii ndiyo inaleta 'strike' kila siku. Kwa kuchukuwa mtu ambaye hajui administration ana force mambo mengine university ambayo wanafunzi hawataki na hii ita-minimize strike in universities. Nimemalizia.

**Com. Lethome**: Joseph Ngala?

**Ngala**: Kwa jina naitwa Joseph Ngala. Natoka Kayapungo, Ngalameni sub-location. Mimi pamoja na kule ninakotoka wezangu, tunataka serikali ya majimbo. Kila jimbo liwe na mamlaka kamili ya kusimamia na kutekeleza mahitaji yake.

Pili, kila jimbo liwe na majeshi yake pamoja na walinda usalama wa aina zote.

Tatu, tunataka kuweko na makao makuu ambapo wajumbe fulani kutoka katika kila jimbo watakuwa wakikutana na kujadiliana kuhusu mambo ya sehemu zao wanazotoka. Hivi ikiwa katiba itakuwa ya majimbo, serikali hizi za majimbo zitakuwa kila jimbo lina- weza kufanyia bidii watu wake ambao wako nao pale na shinda zao zote ambazo ziko pale ili kufanya mambo yawe nafuu. Maanake kila mmoja analia kazi hakuna, umaskini, magojwa hayana madawa, maanake serikali inajaribu sana lakini kurusha mkono huku na kule saa zingine inakuwa ni kazi ngumu. Lakini ikiwa kila jimbo linajaribu kufanyia kazi sehemu yake itakuwa ni rahisi zaidi kwa wananchi wapate nafuu. Ki-elimu, kimatibabu, na kiuchumi pia kwa jumla. Asanteni.

**Com. Lethome**: Asanti Sana Bw. Joseph Ngala. Ulikuwa umetoka nje wewe. Nimejaribu kuita … hauone kani. Karibu. Ninakupa dakika moja. Kila mtu dakika moja moja.

**Karissa:** Kwa jina naitwa Japhet Karissa. Nimesoma mpaka university na ninaomba kuwa viongozi wote leaders of the country, wawe watachukua jukumu katika office ya education. Wawe watatoa vitabulisho vya waalimu.

**Mohammed:** Mimi kwa jina naitwa Mohammed Mwindali. Mimi nina mapendekezo yafuatayo. Kwanza ningependa Serikali itoe uhuru wa dini kamili. Hii yawezekana kwa kuandika waalimu wa dini katika mashule, primary mpaka secondary.

Jambo lingine ni umilikaji wa ardhi serikali ihakikishe kuwa wale ambao hawana ardhi wamepatiwa ardhi. Na iwe ni makosa kwa mtu kumiliki ardhi ambayo haitumii.

Jambo lingine tunataka katiba iruhusu ikiwezekana wananchi wapate uwezo wa kupeleka hoja zao katika bunge moja kwa moja, kama Mbunge wao hafanyi kazi kama walivyopenda.

Jambo lingine, tungetaka pia Katiba iwape wananchi uwezo ambapo wamemchagua Mbunge au kiongozi na wakaona kuwa hawafai, ikiwa itapatikana asilima themanini ya wakaazi wa pale ambao waweza kutia sahihi, basi wapeleke mapendekezo na waweze kufanya kura ya kuchagua kiongozi mwingine.

Jambo lingine nataka serikali ihakikishe ya kuwa zile pesa za settlement trustee fund, yaani pesa za kuwapa makao wananchi kama ilivyo katika mwaka wa sitini na tatu tulipokuwa tunapata uhuru, ningependa fedha kama hiyo itumike ili kumaliza tatizo la u-squatter.

Jambo lingine ni kumalizia kuwa katiba ilazimishe serikali kutimiza ahadi zake kulingana na policy papers zile ambazo nimezitaja. Asanteni.

**Com. Lethome**: Sasa nafikiri pahali tilipofikia (inaudible) haya umetuweka sana.

**Kalama**: Ombi langu ni kuhusu …..

**Com. Lethome:** Jina? Ili tuweke kwa record.

**Kalama:** Ah Kalama A John. CCC secretary, Kaloleni. Tunajua kwamba kuna national fund for the disabled. Mukikumbuka vizuri Mwenye Kiti Matiba ….

**Com: Lethome**: Joe King'ori.

**Kalama**: Aha… Joe Kingori. Ningependekeza fund hii igeuzwe iwe revolving fund ili kuwanufaisha members ambao wanakuwa kwa fund hii. Kwa mfano tunaweza tuka identify kama ni bank fulani, branch ya bank fulani kwa kila district ili wawe wanaweza kuenda na kukopa pesa kwa uwezo wao. Vile ilivyo hivi sasa zinamalizikia hapo kati kati haziwafikii. Asante.

**Com. Lethome**: Na tukimalizia sina budi kuwashukuru nyote ambao mko hapa. Na ningependa kuwajulisha kwamba wale waliojiandikisha leo kuzungumza wamefika idadi ya mia mbili na nane. Hao ni watu wengi sana kulingana na uzoefu wetu sehemu nyingine. Ni watu wengi sana wamejiandikisha, na waliopata nafasi ya kuzungumza ni watu themanini. Kutoka katika sehemu hii pekee yake. Kwa hivyo ni idadi kubwa hata kuliko ile tuliyoipata jana Mariakani. Lakini tungependa wale niliwaomba wachache fikisheni ujumbe kwa watu wengine kuwa huu sio mwisho wa kutoa maoni. Hata baada ya sisi kurudi Nairobi una nafasi ya kuandika maoni yako na kuyawakilisha either moja kwa moja, kitabu hichocha huku kina anwani yetu moja kwa moja kupitia kwa anwani yetu au kupitia kwa ofisi ya mwakilishi wetu katika wilaya. Kwa hivyo usiende ukanyamaza na maoni yako kwa kuwa tume imerudi Nairobi. La! Toa maoni yako na yatapokelewa mpaka mwisho wa kazi hii maoni yatazidi kupokelewa. Kwa hivyo ha kikisheni watu ujumbe huu. Na tungependa kuwashukuru sana tunajua kulikuwa na upungufu wa civic education lakini yale ambayo mumeyatoa hapa mtayaona yakirudi kwenu pia kwa lugha ya kisheria. Kuwa maoni haya mumeyatoa hakuna hata moja ambalo litapuuzwa. Yote tutayaandika kwa lugha ya kisheria na yatawarudia. Nawa- shukuru nyote kwa subira zenu na wale vijana ambao wemesaidiana na mwakilishi wetu hapa, kutuletea viti na mambo mengine, tunawashukuru Mungu awabariki. Na kama tulivyo anza tulikaribishwa na mwenyeji wetu Bi. Priscilla ambaye ni Councillor hapa. Tungependa pia kabla hatujaondoka atoe vote of thanks kisha atamuita mmoja wenu atufungie kwa maombi. Tunashukuru wale wote wameshirikiana nasi. Asanteni na Mungu awabariki.

**Bi. Priscilla**: Kabla sijaongea chochote (not clear) lakini kuna serikali limetoka mbali limeandikwa Bishop Robert and

Anna.

Mimi kusema kweli nawashukuru sana commissioners; mumekuwa wakaimu kweli………….. Kwa hivyo poleni kwa kazi ngumu lakini nashukuru sana.

**Maombi**: Tunaenda kuomba. Mungu mwenyezi baba uishiye hapo juu, tunashukuru kwa vile umetuweka wazima tangu kuzaliwampaka wakati wa leo. Tunatoa shukrani kwa kufanya kazi kwa ajili ya taifa lako hili la Kenya. Kazi hii inakuwa ngumu lakini (inaudible) kwa nguvu hata wafanyi kazi wamefanya kazi (inaudible) na hii ni shukurani kubwa….

Mkutano huu tunamalizia leo, tunauweka mikononi mwako. Hata tunaweka mikoni mwako sisi wote ambao tunasafiri huko mabarabarani kwenda manyumbani kwetu. Commissioners hawa watasafiri kule ambako wanakwenda, tunaomba sasa vyombo watasafiria (not clear) ukavitakase na ukawabariki, ukawapenda na upendo wote (inaudible). Naita Baba ukatulinde, ukalinde pia jamii zetu, kupata hali, Baba ukatufanyie kazi sisi wote. Tunaomba hayo tukiamini kwamba mahali wewe uko, na nikaliita jina la Baba, la Mwana Yesu Kristo, Mungu Baba nakuamini. Amen.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**